ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 28 Septemba, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid)alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani ya Kauli ya Serikali kuhusu Zoezi la Uondoshaji wa Mifugo katika Maeneo Yasiyoruhusiwa.

Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, naomba kuwasilisha hati mezani Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar Namba 8 ya Mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 11 ya Mwaka 2009 na Kuweka Masharti Bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar Namba 8 ya Mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 11 ya Mwaka 2009 na kuweka Masharti Bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, ahsante.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 2

Utekelezaji wa Agizo la Mhe. Waziri

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mwezi Aprili 2016 Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, alifanya ziara kwa wafanyabiashara na kuagiza risiti zinazotumika ziandikwe majina ya watu wanaolipa, ili kudhibiti ulipaji wa kodi hizo zisipotee.

(a) Vipi utekelezaji wa suala hilo unafanyika hadi hivi sasa.

(b) Je, ni wafanyabiashara wangapi ambao wamebainika kufanya biashara bila ya kulipia ushuru katika maeneo ya wazi, katika eneo la Darajani baada ya Mhe. Waziri kufanya ziara katika eneo hilo.

(c) Je, kwa nini serikali inawatoza ushuru wafanyabiashara katika maeneo yasiyoruhusiwa kwa shughuli za biashara ikiwemo wafanyabiashara wanaouza samaki, nje ya soko katika maeneo ya maegesho na wapita njia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 2 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa suala hili unaendelea kufanyika kwa kuandika jina la mfanyabiashara nyuma ya risiti, ili kupunguza ukwepaji wa kodi. Hata hivyo, hatua za uchapishaji wa vitabu vipya ambavyo vitakuwa na nafasi ya kuandika jina la mfanyabiasara zinaendela kuchukuliwa.

(b) Baada ya zoezi langu tulibaini wafanyabiashara wanane (8) kufanya biashara bila ya kulipia ada zinazostahili na Baraza la Manispaa limechukua hatua ya kuwatoza ada hizo pamoja na faini.

(c) Kimsingi serikali kupitia Baraza la Manispaa halitozi ushuru wa aina yoyote katika maeneo ya wazi ambayo hayaruhusiwa kufanya biashara. Eneo la pekee ambalo linaruhusuwa kwa muda maalumu kufanya biashara ni eneo la nje ya Soko la Darajani, kuanzia saa 11 jioni kila siku na hili lilibainika katika ziara yangu nilipowauliza

wafanyabiashara hao na kukiri kwamba hawatozwi ada na Baraza la Manispaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa imani yake aliyoonesha kuwaachia wafanyabiashara kuanzia saa 11 jioni, ambao ni wanyonge kupata riziki zao mpaka usiku. Ninakupongeza sana Mhe. Waziri na uendelee na msimamo huo na ndio uungwana. Baada ya maelezo hayo pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa wafanyabiashara wanalipa ushuru na kodi, lakini mazingira wanayofanyia kazi hayaridhishi ikiwemo Soko la Samaki na Kuku. Je, fedha zile zinazokusanywa zinakwenda wapi badala ya kufanyiwa utaratibu, yaani kulifanyia angalau ukarabati kwa kweli Soko la Samaki hali hairidhishi pamoja na kwamba samaki ni mtamu, lakini hali hairidhishi na isije ikawa kama hadithi uliyonipa kipindi cha nyuma kwenye Soko la Mnada, pale mpaka leo shimo halijazibwa na watu wanachangisha fedha shilingi elfu mbili (2,000) kuingia na kuelekea kwa Shamshu.

(b) Serikali imekuwa ikihamasisha vijana kufanya kazi, lakini tumeshuhudia Baraza la Manispaa na Askari wa Vikosi vya SMZ wakikimbizana na wafanyabiashara hao na wengine hata kupoteza mitaji yao. Je, unatoa kauli gani kwa wafanyabiashara wadogo tukishuhudia kule Tanzania Bara Mhe. Rais akisema hata njia au barabara zifungwe, ili wafanyabiashara wapate kujiendeleza. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, munapouliza jaribuni kuuliza kwa ufupi kidogo, kwa sababu mukiuliza kwa urefu munawapa wakati mgumu kidogo. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Usiwalinde bwana wee ...

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika,

(a) Natambua kwamba wafanyabiashara wa Soko la Kuku na Samaki wanalipa ushuru kulipia sehemu wanazofanyia biashara. Lakini fedha wanazolipa ielewekе kwamba hazifiki hata thuluthi ya matengenezo ambayo yanahitajika kufanywa ndani ya maeneo hayo ya Soko la Kuku na Samaki. Kwa hivyo, serikali kupitia Baraza la Manispaa ni

chombo ambacho kinatoa huduma zaidi kwa wananchi na sio kufanya biashara, hivyo serikali itatafuta namna ya kuweza kuyafanyia ukarabati maeneo hayo, ili yaweze kuridhisha kama tunavyotarajia.

(b) Serikali inao mpango mkubwa sana wa kuwatunza na kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na kuweza kuwaweka katika maeneo maalumu, ambayo yamepangwa na serikali na yale ambayo yataandaliwa na kupangwa na serikali baadaye, kwa ajili ya kuweza biashara katika mazingira yaliyo bora zaidi kuliko mazingira ambayo wanafanyia biashara hivi sasa.

Hata hivyo, kwa yeyote yule mfanyabiashara mdogo hawezi kuwa na kisingizio cha umasikini tukamuacha akavunja sheria. Kwa maana hiyo, tutakachofanya kwa yule anayevunja sheria, lazima tutamdhibiti na itabidi tumuelekeze, ili aweze kufuata utaratibu wa kufuata sheria. Lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba mazingira mazuri yatawekwa na serikali, ili kuwafanya wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kujitegemea.

Mhe. Sulemain Makame Ali: Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na jitihada zake nzuri anazozifanya Mhe. Waziri, lakini kumetokea utitiri mwingi wa vile vitabu vya risiti kwa wenzetu wa Manispaa. Je, huoni utitiri ule wa vitabu vya risiti ni kupotea kwa mapato.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba unikumbushe jina lake Mhe. Mwakilishi limenipita.

Mhe. Spika: Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba hakuna utitiri wa risiti katika Mabaraza ya Manispaa. Isipokuwa kilichopo ni kwamba utaratibu uliokuwa ukitumika ni kutumia risiti ambazo zilikuwa zinanunuliwa katika maeneo tofauti.

Lakini utaratibu wa sasa ni kwamba Mabaraza yote ya Manispaa na Halmashauri yatatumia risiti maalumu ambazo zimekubaliwa na Wizara ya Fedha kwa maana ya Hazina na *ZRB*. Kwa hiyo, nataka nimuhakikishie kwamba tatizo hilo kama lilikuwepo, basi hivi sasa halipo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi bado natanguliza shukurani au pongezi kwa Mhe. Waziri kupitia watendaji wake katika Halmashauri na Manispaa zetu juu ya ukusanyaji wa mapato.

Swali langu lipo hapa, mapato ni nyenzo za kuendesha Manispaa au Halmashauri, lakini mkusanyaji wa mapato anatakiwa awe na maneno mazuri ya kumhamasisha mfanyabiashara, ili alipe kwa hiari yake. Sasa kwa kuwa kunatokea makosa mfanyabiashara amechelewa kwenda kukata leseni, lakini baada ya kumuelekeza unakwenda kumshambulia kwa matusi au kutumia silaha na kumchukua mtu yule na kumpandisha kwenye gari utajijua mbele ya safari.

Je, Mhe. Waziri watendaji kama hawa ambao tunawajua na ushahidi upo atawachukulia hatua gani za kuwaelimisha, ili waache mambo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nataka nikubaliane naye kwamba sisi tunaotoza ushuru au tunaokusanya mapato kwa wananchi tunatakiwa tuwe na busara na hekima katika kufanya kazi zetu kwa upande mmoja, lakini kwa upande wa pili kwa wafanyabiashara nao wanatakiwa hekima hiyo tutakayoitumia sisi, basi na wao pia wawe nayo kwa kufuata sheria. Kwa kweli, si busara hata kidogo na wala sisi hatupendi kwa shughuli zetu kuzifanya kwa kupeleka askari wenye mitutu ya bunduki, na kwa kadri iwezekanavyo tutajaribu kutofanya jambo hilo. Lakini pale inapobidi, kuna wafanyabiashara wengine sugu, basi tutatumia nafasi ya kupeleka walinzi wa amani katika kumchukulia hatua au kumshurutisha kufuata sheria kwa yule ambaye hataki kufuata sheria bila ya shuruti. *(Makofi)*

Nam. 193

Ukosefu wa Maeneo Maalumu kwa Ajili ya Huduma za Maegesho ya Magari Pamoja na Vyombo Vyengine

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Nchi yoyote duniani ina utaratibu wa kutenga maeneo maalumu ya maegesho ya huduma za magari na vyombo vyengine vya moto, kwa nini Zanzibar tunashuhudia barabara kuu kugeuzwa *parking* na wahusika kutozwa fedha katika maeneo yasiyokuwa rasmi.

a) Je, ni vigezo gani wametumia Baraza la Manispaa kukushanya fedha katika maeneo yasiyokuwa *parking* kama vile mbele ya jengo la Bima, Madema, Mlandege, nyuma ya ukuta wa Rais Mstaafu Mhe. Ali Hassan Mwinyi, mbele ya uso wa Mji wa Darajani, na Malindi soko la Samaki.

b) Je, hatua ya kuruhusu maeneo yasiyokuwa ya maegesho na kugeuzwa maegesho kunasaidia nini katika kupanga Mji wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 193 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Uwekezaji wa maegesho ya magari (*parking)* katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar kunatokana na kuondosha msongamano wa uwekaji wa vyombo vya moto ovyo na kuweka utaratibu mzuri wa uwekaji wa vyombo hivyo, ili kuufanya mji uwe katika haiba nzuri pamoja na kuweka usalama wa vyombo hivyo, huku Baraza likisubiri mpango mkuu wa mji ambao utakuwa unaonesha maeneo halali ya maegesho ya magari au *parking*, ili kuondosha changamoto hizo.

b) Baraza limeamua kufanya hivyo kutokana na ongezeko kubwa la vyombo vya moto hapa mjini. Hata hivyo, Baraza linakiri tatizo hili litapungua baada ya ujenzi wa ukanda wa Darajani, yaani Darajani *corridor*, ambao utajumuisha ujenzi wa maegesho ya kisasa na kukidhi haja iliyopo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri pia nimshukuru kwa kukiri kwamba msongamano unaendelea, lakini nafikiri Wizara yake inachangia msongamano, kwa sababu huku tunashuhudia kuwa wanataka kuondosha msongamano na huku serikali inazidisha msongamano.

Kwa kuwa Mhe. Waziri hatua ya kuondosha msongamano mbele ya barabara kama vile pale mbele ya Afisi ya Manispaa, hivi kweli kuna ubinadamu kuweka *parking* pale, *Grand Palace Hotel* msongamano wa bandari tunaujua kama ni kwa uchochoro wake tulionao na bandari yetu iko barabarani tena pale watu wanateseka. Mhe. Spika, kuna harufu na hilo naomba Mhe. Waziri alifuatilie Polisi Jamii ndio wanaochangisha fedha za pale.

Vile vile, Soko la Samaki Malindi ni vitu vya ajabu na wenyewe wenye mamlaka ya barabara wanapiga kelele tena kuna mvutano kati ya Manispaa na Mfuko wa Barabara *UUB*. Je, unatoa kauli gani kwa ajili ya kumaliza msongomano huu, ikiwa tunazuia msongamano, lakini nyinyi ndio munausababisha msongamano kwa kufanya *parking*, kwa sababu hizi *parking* za ajabu kwani ziko *town centre*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, uliza swali na wala usituhutubie.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Je, ni lini wizara yako itashirikiana na mwenye dhamana ya barabara kuliko kuja ukavamia tu sehemu za kufanya *parking*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza serikali haisababishi msongomano. *(Makofi)*

Pili wizara yangu haifanyi mambo kwa utashi wake peke yake, isipokuwa kila tunachokifanya tunafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi zote za serikali ambazo zina mamlaka kwa mujibu wa sheria zilizopo za nchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi aelewe kwamba Mabaraza ya Manispaa yanatekeleza sheria za nchi za taasisi mbalimbali kwa mujibu wa sheria Nam. 7 ya Serikali za Mitaa, 2014.

Mhe. Spika, la pili msongamano unakuja kutokana na mahitaji ya wananchi na maendeleo ya nchi ya hivi sasa. Mji wetu ulijengwa karne nyingi sana zilizopita, sasa hivi tunashuhudia kwamba wananchi wengi wamehamasika kuwa na vyombo vya moto na wote wanakimbilia kwenye Makao Makuu ya Serikali iliyopo Mji Mkongwe na *center* ya biashara ambayo kwa kiasi

kikubwa karibu asilimia 90 iko katika maeneo ya Mji Mkongwe. Sasa ili kudhibiti msongamano ndio maana nilipokuwa nikijibu swali mama nilisema pale tu utakapokamilika mpango mkuu wa mji wa *master plan* ya Mji wa Zanzibar pamoja na kurekebisha eneo la Darajani *Corridor* tutaweza kwa kiasi kikubwa kuweza kupunguza msongamano. Sasa suala la Malindi na suala la wapi, mimi nadhani utaratibu wa kuondosha *parking* katika eneo la bandari serikali imefanya jambo la maana kuondosha msongamano ambao ulikuwepo pale. Ahsante sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kuweza kunipa nafasi hii, napenda nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa lengo la serikali na wizara yako ni kuhakikisha tunatengeneza maegesho mazuri na kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu na abiria. Nini kinasababisha maegesho yale ya magari ya kule Pemba hususan Wilaya ya Chake-Chake kuchelewa kumalizika. Na je, ni lini yatamalizika ili kuwaondolea usumbufu madereva na abiria wetu wa Wilaya ya Chake-Chake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza kinachosababisha msongamano katika Mji wa Chake-Chake ni lile lile nililolisema mwanzo. Ni watu wetu kufanya shughuli zao kwa mazoea hasa madereva na utingo kutofuata maelekezo ya taasisi zetu baada ya kuwaelekeza kwamba sasa maegesho yatakuwa maeneo fulani na ikawa wanang'ang'ania kubaki katika maeneo fulani. Hata hivyo, serikali kupitia Baraza la Mji wa Chake-Chake linao mpango madhubuti sasa ambao wewe mwenyewe Mhe. Mwakilishi nadhani umeanza kuona harakati za kupunguza msongamano ule baada ya kutengeneza maeneo ya maegesho ya magari ambayo Baraza la Mji la Chake-Chake limeyaandaa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza na mimi ningempongeza kwa baadhi ya kazi ambazo wameanza kuzichukulia hatua kufanya vizuri yeye Mhe. Waziri pamoja na Mkuu wa Mkoa wake. Ningeomba kuuliza swali la ziada lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa nchi nyingi hasa zilizokuwa ndogo duniani na kupata matatizo ya *parking* na kusababisha foleni ya magari, ni lini wizara yako itafikiria kujenga katika maeneo ya Mjini *parking* za ghorofa.

b) Kwa kuwa nchi yetu kipato ni kidogo na uwezo wa wananchi ni mdogo na wananchi wanachajiwa 500 kwa saa moja kwa *parking* yoyote au 1000 kwa muda wa saa moja. Je, wizara yako itafikiria lini kuweka *package* ya *fees* za *parking* kama mfano mtu anataka ku-*park*

kwa kutumia maeneo kwa siku nzima ndani ya mji labda mkaweka *package* 2000 au 5000 yaani asichajiwe tena kule kulipa sasa hivi anakwenda kwengine anachajiwa tena, anakwenda kwengine ukimaliza muda anachajiwa tena ikasababisha usumbufu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, serikali kupitia Mradi wa Darajani *Corridor* itaanza kujenga jengo moja la mwanzo lenye *parking* za ghorofa pale Darajani.

Pili, serikali kupitia Mkoa wa Mjini Magharibi na Manispaa zake inao mpango kabambe wa kutengeneza utaratibu wa kisasa wa kuyatambua magari ambayo yanaingia katika mji, na utaratibu huo utajumuisha lile suala ambalo amelisema Mhe. Mwakilishi la kuweza kuweka mashine za kuweza ku-*control* kwa yule mtu ambaye anaweza akalipa kwa wiki, akalipa kwa mwezi, akalipa kwa mwaka katika kuzitumia *parking* ambazo zitakuwa zimewekwa kwa mujibu wa utaratibu tutakaokubaliana na makampuni ambayo yataingia mkataba na serikali.

Nam. 64

Tatizo la Kuvuja kwa Mapato

Mhe. Simai Mohammed Said (Kny: Mhe. Salma Mussa Bilal) - Aliuliza:- Kumekuwa na uvujaji mkubwa wa mapato katika nyanja mbali mbali hapa nchini hasa kupitia wafanyabiashara.

Ni lini mfumo wa *electronic* utaanza kutumika ili kuhami mapato ya nchi kupotea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Nam. 64 la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa nieleze kuwa swali hili halijakaa vizuri sana, halijawekwa wazi na anapozungumzia mfumo wa *electronic* sina hakika kama anazungumzia vifaa vya *EFD's* au anazungumzia mfumo wenyewe.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu taasisi za ukusanyaji wa mapato, *TRA* na *ZRB* zimekuwa zikitumia mifumo tofauti ya kielektroniki. Kwa mfano, *TRA* imekuwa ikitumia mfumo wa *ASYCUDA ++* kwa usimamizi wa mapato ya Forodha. Lakini vile vile *TRA* imekuwa ikitumia mfumo wa *E-TAX* kwa kodi ya mapato. Kwa upande wake *ZRB* inatumia mfumo wa *ITAS* kwa usimamizi wa mapato.

Vile vile huwa tunatumia mfumo wa *IFMS* (*Intergrated Financial Management System*) kwa kukusanya mapato ya mawizara. Sasa kama anakusudia mfumo huo mifumo hiyo ipo, la kama anakusudia mashine za *EFD's* ni juzi tu hapa tumebadilisha sheria kwenye zile sheria mbali mbali, yale mabadiliko ya sheria ya sheria mbali mbali *Miscellaneous Amendment Act* na ndani yake mlikuwa na sheria ya biashara Nam. 14 ya 2013. Sasa kifaa hiki *EFD's* kimeingizwa ndani ya sheria kwa ajili ya kuweza kutumika.

Mhe. Spika, na hivi sasa tumo katika hatua za kukamilisha kanuni, kanuni ziko kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuanza kutumika vifaa hivi. Pia tuko katika utaratibu wa kununua *EFD's machines* 1000 katika mwaka huu wa fedha 2016-2017.

Mhe. Spika, iwapo anazungumzia mfumo nieleze kwamba mfumo unaandaliwa wa *E-TAX* kupitia mradi ambao utapata ufadhili wa Benki ya Exim na tuko katika hatua nzuri ya kukamilisha mradi huo. Lakini niseme tu katika hizi mashine za *EFD's* hazina lengo la kukusanya mapato peke yake, lina lengo la ku-*modernize* biashara yenyewe, kwa sababu mbali ya kukusanya mapato mashine za *EFD's* zitamsaidia mfanyabiashara kwanza kuweka kumbukumbu zake, kujua mauzo, vile vile kujua *stock* aliyonayo kwa ajili ya kuingiza *stock* mpya. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri ningependa nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu cha (a) na (b).

a) Sambamba na majibu aliyoyatoa tunajua kwamba kuna taasisi nyingi ambazo amezizungumzia katika mfumo mzima alioutaja kama mfano wa *IFMS* pamoja na suala la kutumia hizi Electr*onic Fiscal Devices* (*EFD's*) ili ziweze kutumika katika pande zote mbili, sekta binafsi pamoja na *public* pia kwa upande mmoja. Je, serikali itafanya mpango gani wa kuhakikisha kwamba katika uunganishaji wa suala lote zima hili la kutumia hizi *EFD's* na kutumia huu mkonga wa *fiber optic* ambao umeigharimu serikali zaidi ya dola milioni 18 na hadi hivi sasa

hakuna lolote ambalo linalofaidika juu ya hili hasa ukizingatia kwamba zaidi ya taasisi 86 za serikali zilikuwa ziunganishwe na hakuna lilokwenda.

b) Kwenye mfumo mzima wa *E-government* ambao serikali ilikiri kuanzisha katika miaka michache ya nyuma iliyopita, na nina uhakika katika mfumo mzima wa kupokea na ulipaji wa mapato ya kodi utahitaji kutumia mfumo wa kuweza kuweka *data* na kumbukumbu za wateja au wafanyabiashara pamoja na serikali kwa ujumla. Je, katika mfumo huu wote wa *E-government* pamoja na huu wa mfumo wa kutumia *Electronic Fiscal Devices* watafaidikaje wakati huku tayari mkonga wenyewe umeshaathirika. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, katika jibu nililolitoa katika swali mama nilieleza kwamba serikali iko katika maandalizi na hatua za mwisho za kukamilisha Mradi wa *E-government* na mradi huu ndio utakaotumia *fiber optic.* Mradi uko katika hatua nzuri, ni suala sasa hivi la *finance agreement* kuwa-*signed* na *signing* itafanyika na Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini baada ya kukamilika *process* hiyo kutakuwa na *all landing agreement* baina ya SMT na SMZ kwa ajili ya kuanza mradi huu. Ningemuomba Mhe. Mwakilishi asuburi ni muda mchache tu uliobaki kutakuwa na mradi huo, lakini vile vile tutakapokuwa na mradi huu tutaweza sasa kuunganisha ile *last mile connectivity* ya taasisi mbali mbali 84 kwa mujibu wa mkataba wa serikali na Zantel na ndipo hapo tutakapoweza kuwa na matumizi sahihi ya mkonga wetu.

Nam. 118

Kubuni Njia Mpya za Ukusanyaji Mapato

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha kodi maalumu ya miundombinu (*Infrastructure tax*) na fedha hizo kuingizwa kwenye mfuko maalumu (*Infrastructure Fund*).

a) Je, mfuko huo maalumu (*Infrastructure Fund*) umepokea kiasi gani cha kodi ya miundombinu hadi kufikia mwezi Machi, 2016.

b) Je, serikali imejipangia vipi kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 kama ifuatavyo:-
Kwanza kwa kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa mnamo mwaka wa fedha 2015/16 serikali imeanzisha kodi maalumu ya miundombinu (*infrastructure tax*) kwa lengo la kuimarisha miundombinu kwa kutumia vianzio vya ndani. Serikali pia ilianzisha mfuko maalumu *(Infrastructure Fund*) kwa madhumuni ya kutunza fedha hizo.

a) Katika mwaka wa kwanza wa ukusanyaji wa kodi za miundombinu hakuna fedha zilizoingizwa katika mfuko wa miundombinu. Badala yake fedha hizo zilizofikia bilioni 16.5 zilitumika moja kwa moja kwa ajili ya uendelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Spika, ili kutimiza matakwa ya sheria, utakumbuka kuwa nilipowasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016 - 2017 niliainisha pia miradi ambayo itanufaika na fedha za Mfuko wa Miundombinu kwa mwaka huu 2016 – 2017.

b) Kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017, serikali haijapanga kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, na hili tulilieleza wakati tulipokuwa tukiwasilisha bajeti ya serikali. Lakini Mhe. Spika, kwa mwaka huu tumejipanga kuviendeleza vyanzo viliopo kwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kama ifuatavyo:-

I. Kuanzisha mfumo wa pamoja wa usimamizi wa kodi kwa kuzingatia maeneo (*Block Management System*);

II. Kuweka miongozo na kanuni kwa mtu wa tatu (*Agent, tax consultant and Audit and Accounting Firms*) kwa ajili ya kutoa mashirikiano katika kupata taarifa za mlipakodi; na

III. Kusimamia ulipaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje kwa kuzigawa bidhaa hizo kulingana na namba maalumu, wingi na ubora wa bidhaa hizo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza maswali ya nyongeza yenye (a) na (b).

a) Kwanza nataka kujua sababu zilizopelekea hizi bilioni 16.5 kutokuingizwa katika mfuko wa miundombinu kama sheria ilivyotaka.

b) Ni sababu zipi zilizopelekea makusanyo hayo ya 2015-2016 yasifikie asilimia 100 ya bilioni 18 zilizoidhinishwa na Baraza lako la Wawakilishi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza mwaka 2015 – 2016 ndio mwaka ambao tulitakiwa kuanzisha kodi hii, kwa hivyo kodi ilikusanywa na ilikusanywa kabla ya kuanzishwa mfuko wenyewe kisheria. Kwa hivyo, kulikuwa hakuna mfuko, na kwa namna hiyo fedha zile zilizokusanywa zilitumika moja kwa moja katika miradi ya miundombinu. Sasa hiyo ndio sababu kuu.

Vile vile kuhusu suala la kwa nini hatukufikia asilimia mia moja, niseme tu kwamba si kila makisio tunafikia asilimia mia moja, yale yalikuwa makisio tungeweza kufikia asilimia mia moja au tungeweza kupindukia asilimia mia moja lakini wakati mwengine chini ya hapo hutokezea lakini huwa inatupa mafunzo ya kuzingatia katika mwaka unaofuata.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana mimi ningempongeza kwanza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuanza kutumbua tumbua wale wanaokula fedha.

(a) Kwa kuwa amekiri kuna fedha bilioni 16 zimeshatumika kwenye miundombinu, je, wizara yake imehakikisha vipi kwamba zile fedha zimetumika kikamilifu kama wizara yake ilivyopendekeza zitumike.

(b) Wizara yake itawapa nguvu zaidi vipi wale taasisi ya udhibiti wa fedha za serikali ili kuhakikisha kwamba hizi fedha zinazotumika vibaya wanazishughulikia ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba arudie lile la (b)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante. Kwa kuwa wadhibiti wa mahesabu ya serikali wanakuwa nguvu yao wakati mwengine ni ndogo wanapohitaji *documents* au wanapohitaji nguvu ya kwenda kusikiliza sehemu huwa kunatokea vikwazo wakati mwengine.

Je, ananihakikishia vipi kwamba atakuwa nao pamoja kuhakikisha kwamba wanachokitaka katika kufuatilia zile hesabu au kuchunguza anasaidiana nao bega kwa bega.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza kabisa tuna utaratibu maalumu wa kufuatilia matumizi ya serikali. Kwa hivyo, huu utaratibu uko kisheria unafuatwa na pale ambapo kunatokea kasoro zozote tunaweza tukazibaini na zoezi hilo linafanyika na tutaendelea kulifanya.

Vile vile swali lake la (b) kwamba tunakaaje na hawa watu wanaoshughulika na udhibiti wa ukusanyaji wa mapato. Tayari Wizara ya Fedha na Mipango imeshaanza kazi hiyo. Hivi karibuni tulikuwa na kikao maalumu cha Wahasibu Wakuu wote wa mawizara yote na taasisi zote, lakini vile vile tumekaa na watu wa *ZRB*, tutaendelea kukaa mpaka na wakusanyaji wa mapato, lengo letu kwanza kubaini changamoto ziliopo katika sekta mbali mbali na lengo kuu baada ya kuzibaini changamoto hizo basi tuzipatie ufumbuzi unaostahiki.

Mhe. Spika, lakini kama tutakavyokumbuka wakati nawasilisha Bajeti ya Serikali lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha tunaongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mwaka huu hatuna vyanzo vipya lakini vyanzo viliopo tuhakikishe kwamba mapato yote yanakusanywa kikamilifu. Vile vile kuna mikakati maalumu ambayo niliisema wakati nawasilisha Bajeti ya Serikali ya kuhakikisha matumizi yanayofanyika yanafanyika kwa usahihi na kwa ukamilifu wake na hakutakuwa na uvujaji au ubadhirifu wa mali za umma.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuwanasihi wale wote wanaohusika kwa namna moja au nyengine kubadilika, na kwamba serikali haitamvumilia yeyote yule atakayekwenda kinyume na taratibu na miongozo ya matumizi na usimamizi wa mapato. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha, utulivu na lugha ya kistaarabu kabisa. Naomba na mawaziri wengine waige mfano wa Waziri wetu huyu wa Fedha na Mipango. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mfuko huu wa Miundombinu, na kwa kuwa Zanzibar miundombinu yetu mingi mibovu. Je, tunategemea lini Mfuko huu kuboresha ile miundombinu ambayo tunayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, ni kwamba kwanza serikali imeweka makusudi fedha hizi zitumike kwa miundombinu kwa kujua umuhimu wa miundombinu nchini kwetu.

Pale mwanzo ulipoanzishwa Mfuko huu ilifikiriwa kwamba asilimia 75 za fedha zinazokusanywa ndio zitumike kwa miundombinu na asilimia 25 zitumike katika Mifuko mingine. Lakini serikali sasa imeamua asilimia yote 100 itatumika kwenye miundombinu. Pamoja na hivyo, bado fedha hizi ni kidogo kulingana na mahitaji, lakini kama tulivyosema katika mwaka wa fedha huu wa 2016/2017 fedha hizi zitatumika kusaidia ujenzi wa miundombinu katika maeneo mengi ikiwemo barabara hasa ile barabara ya Chake Chake/Wete na Ole, Kianga; lakini kupeleka umeme vijijini hasa Kisiwa cha Fundo, pia itasaidia sekta ya elimu, kilimo kwa maana ya umwagiliaji maji na vile vile uvuvi.

Mfuko huu utaongezeka pale tu hali ya uchumi wetu utakapoimarika na serikali inachukua juhudi kubwa zaidi kuhakikisha kwamba uchumi unaimarika ili na Mfuko huu uweze kukua zaidi na uweze ku-*finance* shughuli nyingi zaidi za kimiundombinu. Mheshimiwa ahsante.

Nam. 155

Serikali kusitisha Kuingiza Mchele wa Mapembe

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante sana kunipa nafasi kuweza kuulisa swali asubuhi hii ya leo, tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuchimbe mafuta yetu kwa salama na amani pia amjaalie Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi afya njema. Sasa swali langu Nam. 155 naomba lijibiwe.

Imebainika kuwa hapa Zanzibar kumekuwa kukiingizwa mchele kutoka Thailand, Dubai na kwengineko. Mchele huo unasadikiwa kuwa ni mbovu na unahatarisha maisha ya watumiaji jambo ambalo linaweza kuchochea ongezeko la maradhi mengi nchini.

Kwa kuwa chakula hujenga afya bora kwa mlaji. Je, ni lini mchele wa mapembe utakatazwa kuingia nchini.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba nijibu swali Namba 155 la Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ilibainika kwamba hapa Zanzibar kumekuwa kukiingizwa mchele kutoka Thailand au Dubai na kwengineko. Mchele huo unasadikiwa kuwa ni mbovu na unahatarisha maisha ya watumiaji.

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu ya serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni kuhakikisha kwamba bidhaa muhimu za chakula (Mchele) zinapatikana bila ya usumbufu. Tunapenda kujuilisha kwamba Mapembe ni moja kati ya jina la biashara *"Brand Name"* linalotumiwa na wafanyabiashara wanaoingiza mchele nchini. Hata hivyo, napenda kujuilisha kwamba, kwa upande wa Zanzibar kwa sasa hakuna mchele wa mapembe, isipokuwa ipo Michele mingine ambayo inatumiwa na wananchi wa kipato cha chini kama vile mchele wa aina ya *Tulip*, Chapa ya Mpunga, *Sunflowers* na mwengineo.

Vile vile naomba kujuilisha kwamba, mfanyabiashara yeyote atakayeingiza mchele nchini ni lazima aambatanishe na cheti cha afya *"Certificate of health"* kutoka nchi aliyonunua bidhaa hiyo. Hata hivyo, mchele unaoingizwa nchini ni lazima ufanyiwe uchunguzi wa kimaabara kama unafaa kwa matumizi ya binaadamu kabla ya kuingizwa katika soko.

Mchele wowote unaoingizwa sokoni huwa tayari umeshafanyiwa uchunguzi wa maabara na Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi (*ZFDB*) na unakuwa hauna madhara kwa matumizi ya binaadamu.

Aidha, tunaomba kujua kama yeye Mheshimiwa ameuona mchele ambao haufai kwa matumizi ya binadamu na upo sokoni basi tunaomba wizara yangu ipewe taarifa ili iweze kuchukua hatua muafaka.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kuhakikisha kwamba wizara yake kupitia vitengo vinavyohusika kusimamia usalama wa wananchi wetu katika chakula.

Pili, niwapongeze watendaji wake kwa kufuatilia mambo mbali mbali ya kuhakikisha kwamba vyakula vibovu haviingii katika nchi yetu.

Je, kwa kuwa swala la mchele kutoka nje tuseme haya Mapembe maana wote unaitwa Mapembe, wizara ina mpango gani wa kuwahamasisha wafanyabiashara wetu hapa Zanzibar kwa kuwa mchele wa Mbeya Kyela ni rahisi kwa sasa hivi; wakafanya ushindani wa kuleta mchele huo kwa wingi ili upungue bei. Wizara ina mpango gani wa kuhamasisha wafanyabiashara hao hasa tukizingatia kwamba mchele wa Mbeya unapendwa zaidi kuliko mwengine katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, miongoni mwa sera tuliyokuwanayo tunayoifanyia kazi sasa hivi ni kuona kwamba tunaruhusu au tunashajihisha biashara ambayo itawawezesha wananchi wetu kupata vyakula kwa bei nafuu. Pia tunataka kuzungumza na Serikali ya Muungano kuona kwamba hii biashara ya mchele kutoka Bara kuja Zanzibar inawekewa utaratibu uliokuwa mzuri na unaofahamika.

Tatizo liliopo ni kwamba, mchele unaotoka Bara ulivyokuja gharama yake ilikuwa kubwa kwa sababu ya usafirishaji, jambo ambalo nataka tuzungumze na wenzetu wa Wizara ya Biashara Bara kuona kwamba kunakuwa na utaratibu wa kutoka ulipozalishwa huu mchele mpaka unafika Zanzibar kwa utaratibu ambao utawawezesha wafanyabiashara wa Zanzibar kupata mchele kwa wakati na pia mchele ambao safi na ambao utakuwa na bei inayoridhisha. Mpaka hapo utapoweza kuwa utaratibu wa aina hiyo bado naona wananchi wataendelea kupata mchele kutoka Thailand na Vietnam. Kwa sababu ndio ambao wafanyabiashara wetu wamejikita kununua mchele wa aina hiyo. Sio rahisi kazi hiyo, lakini tutajaribu kuzungumza na Wizara ya Biashara na tumetia katika *plan* yetu ya mwaka huu ili biashara ya Bara ya mchele huu uweze kuwafikia wananchi. Mchele mzuri, mchele unazalishwa kwa wakati lakini pia tunataka mchele ambao utakuwa safi kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwenye *budget speech* nilisema wafanyabiashara ni watu wasio na dini, dini yao ni *profit* na kitabu chao ni ghilba.

Mhe. Spika, tumekuwa tukishuhudia kila uchao hapa Zanzibar wafanyabiashara wanapoingiza vyakula kama mchele, sukari na unga wa ngano kila siku unazidi bei na haupungui, hata Mwezi wa Ramadhani ambapo serikali ilipunguza baadhi ya mambo lakini bado bidhaa za vyakula Zanzibar ziliendelea kupanda bei.

Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri, wizara yake ina mkakati gani wa kurudisha au kuiweka tume ya bei iweze kufanya kazi na kuweza ku-*regulate* bei za vyakula hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli wakati wa *budget speech* yangu nilipokuwa najibu hoja za Wajumbe hoja hii ya kuwa na tume ya bei Mheshimiwa aliileta katika kikao hicho. Na mimi nikamjibu kwamba, sasa hivi uchumi tuliokuwa nao ni uchumi huria tunakwenda katika utaratibu huo ambao wafanyabiashara kwa kutumia uwezo wao na fedha zao wananunua bidhaa kuleta katika nchi yetu.

Pia nilimwambia kwamba, katika kupitia kitengo chetu cha Kumlinda Mlaji tunapanga bei elekezi, hatumuachii tu mfanyabiashara aje alete bidhaa zake auze anavyotaka yeye mwenyewe. Tunafanya hivyo kutegemea na viashiria vitatu. Kwa mfano, tunaangalia bei iliyoko duniani sasa hivi kama serikali inataka kuagiza mchele, tunaangalia bei ya mchele huko kunakozalishwa mchele ni kiasi gani, natoa mfano wa mchele. Baada ya hapo tunaangalia na gharama zake, gharama za kusafirishia mchele au chochote kile kutoka nje kwa mfano kutoka Thailand kuja Dubai au kutoka Thailand kuja Zanzibar, tunaangalia bei, lakini pia tunaangalia gharama za ndani. Mchele ukifika hapa kuna gharama za ndani anatakiwa azilipe mfanyabiashara. Kwa hiyo, tunaziangalia zote na tunasema kwamba hii ndio bei elekezi ya vyakula vyetu.

Sasa kimetokea nini kipindi hiki chote tulichokuwa nacho? Kipindi hiki Mhe. Spika, ni kwamba bei za vyakula mwanzoni mwa Mwezi wa Ramadhani ilikuwa bei ilitulia sana kwa sababu ununuzi wa vyakula hivi kule nje ulikuwa haujaingiliwa. Katikati baada ya Mwezi wa Ramadhani kukaingia utaratibu kwamba China walinunua vyakula hasa mchele na sukari, walikwenda wakanunua vyakula vyote Vietnam na nchi nyengine. Kwa hiyo, pale ndio bei ikapanda ikawa kubwa zaidi hasa ya sukari na bei ya mchele. Kwa sababu kukiwa kuna wanunuzi wengi hilo sasa ni suala la soko huria, kulikuwa kuna *demand* kubwa yaani kulikuwa kuna watu wanataka vitu vile kwa wingi basi na bei nayo vile vile inapanda. Lakini kama ikiwa watu hawavitaki vitu vile bei inashuka huo ndio utaratibu wa biashara duniani kote, na sisi watu wa Zanzibar tujue hilo kwamba biashara huko ulimwenguni kunakuwa na mabadiliko kwa sababu bei zinabadilika kwa hali hiyo.

Kwa hiyo, tunacho kitengo chetu cha kumlinda mlaji moja ya jukumu lao kitengo hiki ni kuhakikisha kwamba tunapita katika maeneo na tunaangalia bidhaa, kabla mfanyabiashara hajaagiza lazima kwanza apewe kibali na kitengo chetu hiki cha Wizara ya Biashara, akipewa kibali kinamuwezesha anapokuwa

tayari kuja kuuza tuje kuzungumza na sisi kuona bei ambayo inauzwa inakwenda kwa mujibu wa zile gharama zake zilizokuweko, haturuhusu mfanyabiashara achukue *super profit* ili awaumize wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa inasemekana kwamba mchele wa Mapembe bado unaendelea kuingizwa katika nchi yetu lakini pia bado unaendelea kuuzwa madukani isipokuwa wanabadilisha rangi ya mifuko tu na nembo. Je, Mhe. Waziri katika kuutambua mchele huu wa Mapembe wanatumia sifa gani ili kuweza kuutambua.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilizunguka maghala yote yalioko Zanzibar na tukaangalia sikuona *packet* hata moja iliyokuwa ya Mapembe. Kuna kampuni moja ilikuwa na Mapembe ya zamani waliya-*phase out* wakayauza yote. Kama nilivyosema sasa hivi kuna *Tulip, Sunflower* na kadhalika, si kweli kwamba wafanyabiashara wanabadilisha *package* na kutia Mapembe ndani yake. Kwa sababu tumewaambia na tumeweka mkakati mchele unatakiwa uletwe hapa hata kama huu wa bei nafuu lazima ufikie usiwe wa muda mrefu. Kuna malalamiko mengi ya Mapembe kwamba mchele ulikuwa mbaya, mchafu na umekaa muda mrefu. Kwa hivyo, mchele ukiangalia sasa hivi mwingi wao ulioko Zanzibar sasa hivi ni mchele ambao unatoka Vietnam kwa muda ambao sio mrefu wa kusababisha kuwa na mavumbi na kuwa na uchafu.

Vile vile kama ana taarifa na kama ana ushahidi kwamba kuna duka wamebadilisha *package* na kutia Mapembe basi ningeomba ushahidi wake atuletee ofisini na tutakwenda kulifuatilia hilo. *(Makofi)*

Nam. 150

Tatizo la Kuingiza Mapato kwa Uwanja wa Gombani

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Uwanja wa Gombani hivi sasa umekabiliwa na tatizo la kuingiza mapato ya ziada ukiachia waingiaji wa kuangalia mpira wa miguu tu.
Je, wizara haioni umuhimu wa kutengeneza milango ya maduka na maghala na kuyakodisha kwa wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:- Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake nambari 150 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kawaida kwamba katika viwanja vingi vya michezo katika nchi mbali mbali hujengwa maduka kama ni vitega uchumi vya kuendeleza maeneo hayo na pia maduka hayo husaidia kutoa huduma kwa watu wanaofika katika viwanja hivyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Uwanja wa Gombani, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imepokea ushauri huo. Hivyo, tutauzingatia ili hatimaye Uwanja huu wa Gombani uweze kupata mapato. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu yake Mhe. Waziri, lakini Uwanja wa Gombani umegharimu fedha nyingi sana na sio rahisi kuujenga tena uwanja kama ule, hofu yangu usije ukapotea kama Hoteli ya Mkoani ya Serikali na ile ya Wete.

(a) Je, serikali imejipangaje kuulinda uwanja huu ili usije ukapoteza haiba yake.

(b) Je, serikali imejipangaje kurudisha gharama zilizotumika na kupata faida kwa uwanja huo au ni shamba la bibi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imegharimika kwa kujenga uwanja ule. Nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali imejipanga kuchukua hatua ya kuulinda na kuuhifadhi uwanja ule ili tuone kwamba serikali haipotezi mapato katika uwanja ule.

(b) Mhe. Spika, nataka nimuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba serikali kwa kurudisha gharama zilizotumia katika kuujenga ule. Hiyo gharama niseme kwamba imesharudi zamani kwani huu uwanja umejengwa kwa gharama na umeshughulikiwa. Kwa hiyo, niseme kwamba kutokana na ushughulikiaji wa uwanja huu na kutunzwa na nikiwa ni shahidi kwamba ni juzi tu serikali imesimamia na kutia *tartan* katika uwanja huu na sasa hivi tumo katika marekebisho ya upakaji wa rangi kwa kuboresha huu uwanja na kuziona hizi gharama hazipotei na

serikali ipo pamoja na wananchi kuona kwamba huu uwanja bado unaendelea na kuwa na gharama. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, lengo la serikali la kuanzisha viwanja vya michezo si kupata faida ya moja kwa moja kwa maana ya fedha bali lengo ni kuimarisha suala la michezo nchini na hasa hasa kuendeleza vipaji vya vijana wetu ili wajenge uwezo mkubwa katika suala la michezo, tukiamini michezo yenyewe licha ya kwamba ni sehemu ya kuimarisha uchumi lakini pia ni sehemu ya kujenga afya za wananchi.

Kwa hivyo, lengo kubwa si kupata faida ya kifedha, lengo kubwa ni kuendeleza michezo nchini na serikali inaelewa kwamba kwa wakati wa sasa si rahisi kwa mapato yanayotokana na kuingia katika viwanja mbali mbali kwa wananchi wanaoshuhudia shughuli za michezo itakuwa zinakidhi gharama zilizotolewa. Lakini nia ya serikali kuendeleza michezo, hivyo tutaendelea kujenga viwanja kwa nia ya kuimarisha michezo na siku zote serikali itachukua hatua mbali mbali ya kuvilinda viwanja hivyo.
Hata hivyo, bado tunaomba wananchi wengi waende katika kushuhudia shughuli mbali mbali za michezo katika viwanja vyetu ili kuchangia uwezo wa kuimarisha viwanja hivi. (*Makofi*)

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini uwanja wa Gombani umekuwa na utaratibu wakati wa sherehe za Mfunguo mosi au mfunguo tatu nje ya uwanja ule hukodishwa kwa shughuli za sikukuu na mapato ya maeneo yale hayajulikani yanakwenda wapi.

Je, ni utaratibu gani wa feha zinazopatikana katika ukodishwaji wa maeneo yale wakati wa sherehe za Mfungo mosi na mfunguo tatu zinakwenda wapi, na kama hazijulikani je, anatwambia nini kuhusiana na mapato ya ukodishwaji wa maeneo yale ya Uwanja wa Gombani nje?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika kwanza Mhe. Mwakilishi akumbuke kwamba kuanzisha viwanja vya michezo vya muda katika uwanja wa Gombani ilitokana na tatizo la utengenezaji wa Uwanja wa Michezo ulipo Tibirinzi, na kwa sasa kwa kuwa kiwanja kile kimekuwa tayari na kizuri na napenda Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza *ZSSF* kwa kazi nzuri ya kutengeneza kiwanja kile.

Kwa hivyo, sasa wananchi wanatumia kiwanja cha Tibirinzi kwa ajili ya shughuli za sikukuu. Hata hivyo, mapato yake kwa njia moja au nyengine

yaliyokusanywa yalikuwa chini ya Manispaa ya Chakechake. Kwa hiyo, wao walioanzisha ndio waliokuwa na haki ya kukusanya mapato hayo, na kwa vyovyote vile kutakuwa na gharama zinazolipwa kwa uwanja na naamini zitakuwa zinafanywa hivyo ili kutekeleza wajibu wa kila mmoja katika kutekeleza suala zima la kuimairisha shughuli ambazo zinapangwa. (*Makofi*)

Nam. 45

Utaratibu wa kutoa Pencheni kwa wazee Pemba

Mhe. Mussa Foum Mussa - Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa swali kama hili langu mimi limeshajibiwa na Mhe. Waziri na kwa kuwa hivi sasa wazee wanaendelea kupata vizuri pencheni, kwa hivyo naomba kuliondoa swali langu Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa kwa kuondosha hilo swali.

Nam. 91

Uimarishaji wa Huduma za Kinga na Tiba kwa Wanyama

Mhe. Shamata Shaame Khamis - Aliuliza**:**

Katika kipindi cha miaka mitano ya sasa Serikali imeahidi kuviimarisha vituo vya utafiti na huduma za Kinga na Tiba na kuwapatia wafugaji wetu huduma za upandishaji wa ng'ombe kwa sindano ili kupata mbegu bora.

(a) Je, ahadi hii ya Serikali itaanza utekelezaji wake lini.
(b) Je, ni vituo vingapi vinakusudiwa kuimarishwa katika kisiwa cha Pemba.
(c) Kwa kuwa Serikali imekusudia kuimarisha huduma ya upandishaji ng'ombe, Je, Wizara yako inafahamu kuwepo kwa changamoto ya usafiri kwa wapandishaji wa ng'ombe wa sindano hasa katika Wilaya ya Micheweni, na je, imejipanga vipi kuiondoa changamoto hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano ya sasa ahadi hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanza utekelezaji wake kwa kuviimarisha vituo

vya utafiti na huduma za Kinga na Tiba na kuwapatia wafugaji huduma bora za upandishaji wa ng'ombe. Juhudi za kuvifanyia matengenezo vituo vya utafiti na huduma za Kinga na Tiba ili viendane na hali halisi ya utoaji wa huduma katika mazingira bora ya kuridhisha kwa lengo la kuleta tija kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla zinaendelezwa.

Mhe. Spika, hadi sasa vituo viwili vya huduma za Kinga na Tiba Pemba vimefanyiwa matengenezo vikiwemo Konde, na Kengeja. Aidha, katika kudhibiti magonjwa hasa yatokanayo na kupe wizara pia imelifanyia matengenezo makubwa josho la Makangale ili huduma za kukogesha ng'ombe zifanyike katika mazingira bora na salama. Kwa upande wa uchunguzi wa maradhi ya mifugo Maabara mbili za Chake Chake na Wete zilifanyiwa matengenezo kwa ajili ya kutoa huduma za uchunguzi wa maradhi ya Mifugo.

Mhe. Spika, wizara inafahamu suala la uhaba wa usafiri kwa wapandishaji wa ng'ombe kwa sindano katika Wilaya ya Micheweni, hata hivyo wizara imeshakamilisha mchakato wa manunuzi ya vipando (Pikipiki 9) ambazo zitasambazwa kwa watendaji wa Wilaya za Unguja na Pemba kwa kusaidia kupunguza tatizo hili. Ahsante sana.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, je, katika kisiwa cha Pemba vipo vituo vingapi vya utafiti na vile vile vituo vingapi vya Kinga na huduma za tiba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, vituo kwa Pemba vipo sita na unapokuta *AHPC* basi hapo hapo unakuta utafiti pamoja na tiba na kila kitu.

Nam. 168

Kuimarisha kilimo cha mboga mboga nchini

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza**:**

Kwa kuwa vijana wengi wa vijijini wameanza kuonesha jitihada ya kulima kilimo cha mboga mboga kwa lengo la kujikwamua kimaisha.

a) Je, Serikali ina mpango gani katika kuwapatia mikopo isiyo na riba ili waweze kujiimarisha katika kilimo hicho.
b) Nini mipango ya serikali katika kuwawezesha wakulima hao kulima kwa njia ya "*Greenhouse*".

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 168 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli vijana wengi wa vijijini wameanza kuonesha jitihada ya kulima kilimo cha mboga kwa lengo la kujikwamua kimaisha, hali hii imepelekea kuondoa dhana ya kuwa kilimo ni ajira ya wastaafu na wazee. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi za kuwawezesha kwa kuwapatia elimu, teknolojia na mikopo nafuu.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Idara ya Mikopo inawapatia wakulima vijana mikopo isiyo na riba ili waweze kujiimarisha katika kilimo hicho na taasisi binafsi kama (UWAMWIMA) pia inawapatia wakulima mikopo nafuu. Changamoto iliyojitokeza wakulima ni wagumu kulipa hiyo mikopo.

Mhe. Spika, kilimo cha '*Greenhouse'* katika uzalishaji mboga kibiashara ni teknolojia mpya hapa Zanzibar. Hivyo serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Taasisi binafsi (TAHA, UWAMWIMA na ZAIDI) zimekuwa zinatoa taaluma na kuwawezesha wakulima matumizi ya teknolojia hiyo mpya ya kuzalisha kwa '*Greenhouse'*.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Waziri vijana kama tunavyojua ajira ni ngumu na haipatikani kwa urahisi. Lakini pia tunajua kwamba vijana wengi sasa hivi wamejikubalisha katika kilimo hichi cha mboga mboga. Lakini pia tukizingatia kilimo hichi kimeonekana kwamba kwa sasa kina kipaumbele zaidi na soko lake limeongezeka katika mahoteli lakini pia katika jamii kujua umuhimu wa mboga mboga.

Je, Mhe. Waziri unawaahidi nini vijana kushirikiana nao na kuwapa mafunzo zaidi kuweza kukithamini kilimo hichi pia kuwapatia nyenzo zaidi ili kuweza kukiendeleza kilimo hichi ili waweze kufaidika na wajikwamue katika suala la umasikini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nimefurahi sana kwamba vijana sasa wamejiingiza katika suala hili la kilimo. Vile vile katika kuwasaidia vijana tuliwashauri wajiweke vikundi halafu wapitie Wizara ya Uwezeshaji kuwasaidia kwa kupata mikopo na pia kuitumia Wizara ya Kilimo Maliasili kwa ajili ya kupata taaluma zaidi.

Vile vile kupitia mradi wa *MIVARF* utakapojenga kituo cha *Agro processing* basi pia tutawasaidia katika yale mazao yao ili kuweza kuyasindika na kuyasarifu wanavyotaka.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, vijana wengi wamehamasika na kulima kilimo hicho cha mboga mboga na sehemu nyingi hususan mimi ni Mwakilishi wa Jimbo nimepita jimboni kwangu kuangalia vijana wanalalamika kuhusu masuala haya ya kuwezeshwa.

Ni vijana wangapi wamepatiwa mikopo ambao ni wakulima wa mboga mboga?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa vile jibu lake ni la takwimu vijana wangapi wamewezeshwa katika kupatiwa mikopo hii basi nitaomba nimjibu jibu lake kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, katika kipindi cha nyuma kidogo Mhe. Waziri alituahidi kwamba tutakuwa katika kipindi cha miaka mitatu hatuagizi tena chakula.

(a) Sasa serikali ina mpango gani kuvisaidia vikundi hivi vidogo vidogo ambavyo vimeshajiweka katika mpango wa kujiendeleza kifedha na miundombinu.

(b) Watatumia sekta gani kuondoa tatizo hili la kutoagiza chakula kutoka nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 41 naomba akipitie Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba swali lijibiwe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Sarahan ni maarufu jembe lisilo mpini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, serikali imeendeelea kuchukua jitihada mbali mbali katika kuimarisha kilimo nchini ili tuweze kujitosheleza kwa chakula ndani ya nchi na bado mikakati mbali mbali inaendelea kuendelezwa ili kujiimarisha kwa kilimo.

Hivi sasa Waheshimiwa Wawakilishi watakuwa ni mashahidi serikali imechukua hatua kubwa kutoa pembejeo mbali mbali kwa zaidi ya asilimia 75% ya gharama ikifidiwa na serikali kwa ajili ya kuendeleza kilimo nchini.

Vile vile imechukua hatua mbali mbali kusaidia mbegu na mipango mingi ya uanzishwaji kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuendeleza wakulima. Hata hivyo, barabara mbali mbali za vijijini zimejengwa msingi wake mkubwa ni kuimarisha kilimo nchini ili tuweze kujitosheleza kwa chakula. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili serikali itaendelea kuchukua kila hatua kuhakikisha tunajitosheleza kwa chakula hatua kwa hatua.

Nam. 99

ZAWA kuhamisha Pampu za Maji Vijijini

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza**:**

Ni kwa nini ZAWA wamekuwa na mpango wa kuhamisha pampu (*water umps*) katika vijiji na kupeleka maeneo mengine huku ikisababisha usumbufu kwa maeneo husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 99 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la ubadilishaji wa pampu katika visima ni miongoni mwa kazi za kawaida kwa Mamlaka ya Maji katika maeneo ya Mijini na Vijijini, ambapo aidha hutolewa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na baadae hurejeshwa au hutolewa pampu kongwe na kuingizwa pampu nyengine mpya, na zinapotokea hali hizo Mamlaka ya Maji hufanya jitihada za haraka za kufanya marekebisho au kununuliwa mpya ili kuondosha usumbufu kwa wananchi katika maeneo husika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, kwa kuwa katika mradi wa maji uliotengenezwa katika jimbo langu la Tunguu katika kijiji cha Unguja Ukuu ilibainika kwamba pampu iliyokuwepo ambayo ukisukuma maji katika vijiji vya Kaepwani, Unguja Ukuu Kaebona, Pindini, Uzi, Ng'ambwa pamoja na Kikungwi. Na *pump* hiyo iliondoshwa na hadi hivi leo wananchi katika maeneo hayo niliyoyataja husika wamekuwa wanapata maji mara hawapati, mara hayatoki na moja katika usumbufu ni *issue* ya *pump*.

(a) Mhe. Naibu Waziri ananiahidi ni lini hiyo *pump* iliyotolewa hapo itaweza kurudishwa ili iweze kusukuma maji.

(b) Jimbo langu la Tunguu limekuwa na taasisi nyingi za Serikali na pia limetajwa katika Hotuba ya Mhe. Rais alipokuja kuzindua Baraza katika mpango mzima wa mji mpya. Na wananchi wanaoishi katika maeneo ya Bungi pamoja na Tunguu, Binguni, Mtakuja, Dunga Kiembeni pamoja na Dunga Kinyongo kote katika maeneo hayo wamekuwa na hasa matatizo ya maji miaka nenda miaka rudi, na masuala haya yote kwa mfano katika eneo la Tunguu hasa mfereji wa maji ya mvua hawaji kuona ni ndoo kwenda mbele miaka yote.

Je, Mhe. Naibu Waziri kwa huruma kabisa na baada ya taarifa zote hizi. Ni lini atahakikisha hawa wananchi katika vijiji hivi hizi *pumps* zinawekwa ili wananchi waweze kupata maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ninapenda sana afahamu yeye na Waheshimiwa Wawakilishi wengine wote na wananchi kwa ujumla kwamba ni sababu mbili tu ambazo zinapelekea *pump* kuondolewa katika kisima husika.

(a) Kupungua kwa uwezo wa uzalishaji wa kisima husika ama *pump* yenyewe kuharibika. Sasa nimwambie kwamba katika eneo lake ambalo kalitaja hatuna taarifa ya kwamba imeondolewa hii *pump* ingawa tulifanya ziara pamoja naye tukasikia hivyo, lakini haikuwa sahihi.

(b) Kwamba lini tutafanya mpango wa kuhakikisha *pumps* zinapatikana katika visima vinavyohusika. Nimwambie kwamba utaratibu unaendelea na tushafanya ziara katika jimbo lake pamoja naye. Kwa hivyo baada ya harakati hizo kukamilika *in shaa Allah* watafanikiwa kupata *pump*.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo hili la *pump* linaendelea siku hadi siku katika maeneo mengi ya hapa Zanzibar. Je, ni lini Serikali itafanya mpango wa kununua *pumps* ambazo zilizo bora ili tuone kwamba huduma hii inaendelea muda hadi muda.
Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kama ifuatavyo.

Siku zote Serikali ipo makini kununua *pumps* zilizo bora.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza Mhe. Spika, nimeshtushwa na jibu la ghafla ambalo hatukutegemea sote lakini limekwisha hilo. Swali langu hapa Mheshimiwa.

Mhe. Spika, tatizo la maji ni kero kubwa ambayo inatuadhibu katika nchi hii na mimi ninasema tu kwamba katika Jimbo langu la Kijitoupele silali, sina raha, hasa nikizingatia kwamba maji yapo huduma haitolewi ipasavyo.

Je, Mhe. Naibu Waziri kutokana na kadhia hii inayoniadhibu kwenye jimbo langu ambayo ipo inaendelea mpaka sasa hivi kwenye eneo la Shehia ya Meli Nne, Meli Nne Uzi, Tomondo Uzi na Kwarara. Hawa watu wanapata adha wakati kisima kipo pale Meli Tano yaani mashine ya maji kimechimbwa na aliyekuwa Mbunge (Haji Sereweji) na Shamshi Vuai Nahodha aliyekuwa Mwakilishi wakati huo jimbo hilo. Hivyo Wizara ina mpango gani wa makusudi kuliondoa tatizo hili wakati maji yapo wananchi wangu wa Taveta hawapati maji na Meli Nne hawapati saa ishirini nne, kuna nini? Nataka jibu Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kabla sijaomba ruhusa ya kumjibu naomba muongozo wako. Suala mama tunazungumza *pumps* lakini hata hivyo ukiniruhusu nimjibu basi nitamjibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kama una majibu mjibu.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kuna sababu nyingi zinazopelekea wananchi wasipate maji, wakati baadhi ya wakati au kabla ya hapo walikuwa wanapata. Miongoni mwa sababu hizo ni uungaji kiholela usiofuata utaratibu, unapelekea kupunguka kasi kwa maji kufika kwenye sehemu husika.

Lakini pili visima wakati mwengine vinapungua uzalishaji. Halikadhalika inapelekea yasifike maji kikamilifu. Lakini tumefanya jitihada nyingi na tunaendelea na ninamuahidi kwamba nitaendelea kufanya jitihada naye kuhakikisha maji tunayapatia ufumbuzi wa kudumu.

Ahsante sana.

Nam. 134

Kuvuja Kwa Tangi La Maji La Mtambile

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha – Aliuliza:

Tangi la maji la Mtambile kwa muda mrefu linavuja, jambo linalopelekea kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika kwa wananchi wanaotumia tangi hilo. Na Serikali imeshuhudia kuvuja kwa tangi hilo tokea lilipoanza tatizo hilo.

(a) Je, kuendelea kuliacha hivyo bila kufanyiwa matengenezo hatuoni kuwa ni kutokuithamini miundombinu yetu.

(b) Je, ni lini Serikali italifanyia matengenezo tangi hilo ili kupunguza usumbufu wa huduma ya upatikanaji maji kwa wananchi wa eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe.Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba tangi la maji la Mtambile linavuja na kupelekea wananchi wa Mtambile kupata huduma ya maji kwa upungufu.

Mhe. Spika, Wizara yangu inalifahamu vizuri jambo hilo na pia ninalithibitishia Baraza lako tukufu kwamba Wizara yangu inaithamini sana miundombinu ya maji na inafanya kila inavyowezekana kuitunza na kuiendeleza miundombinu hiyo kwa Unguja na Pemba, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji mzuri wa huduma za maji kwa wananchi wote. Uvujaji wa tangi la Mtambile ulianza kidogo kidogo kutoka mwaka 2011. Aidha, uvujaji huo

umekuwa ukiongezeka kwa kadri siku zinavyoendelea. Jitihada za kurekebisha tangi hilo ili kuzuia uvujaji wa maji zilifanyika mara kadhaa kadri kwa haja ya kufanya ilipotokea. Hata hivyo, matengenezo yaliyofanyika hayakudumu kwa muda mrefu.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imo katika kuandaa utaratibu wa kulifanyia matengenezo tangi hilo hatua kwa hatua kama ifuatavyo.

Kulijenga upya bomba la maji la nchi mbili kwa kuweka bomba la nchi sita kutoka kisimani na kuliunganisha na bomba za usambazaji maji kwa wananchi. Lengo la kazi hii ni kuwezesha wananchi kupata huduma ya maji kwa wakati na matengenezo ya tangi hilo. Kazi hii tayari imeshaanza kwa kukusanya mabomba ya maji.

Kukusanya vifaa vya ujenzi wa tangi kulingana na tathmini iliyofanywa, asilimia 90 ya vifaa vya kufanyia marekebisho tangi hilo vitapatikana hapa hapa Zanzibar na asilimia iliyobaki inatarajiwa kupatikana Dar es Salaam. Kuanza kazi za ujenzi mara vifaa vya kufanyia ukarabati wa tangi hilo vitakavyopatikana.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Moh'd Mgaza Jecha kwa swali la nyongeza. Ameridhika Mheshimiwa. Mheshimiwa Doholo.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Shumba Viamboni kwenye Jimbo langu la Tumbe Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) ilichimba kisima na Kamati ya Maendeleo ya Shehia ile pale Shimbo Viamboni waliambiwa wajenge kibanda kwa ajili ya kuwa kisima kile kifanye kazi. Hadi leo kisima kile hakijafanya kazi wala wananchi wa pale hawapati maji.

Ni lini sasa Wizara yako italiona hili na kuona kwamba wananchi wa pale kisima kile kinaendelea kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nina hamu sana ya kufika katika eneo husika kwa ajili ya kuona hiyo shughuli na nilimpigia simu wakati nipo Pemba kwa bahati mbaya sana hatukukutana kwa ajili ya kwamba twende tutembelee kwenye jimbo lake kuangalia changamoto mbali mbali ikiwemo hilo la maji. Basi *in shaa Allah* tutafanya ziara ya kwenda kuangalia na tutizame jinsi ya kulitatua, ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kama unavyolifahamu Jimbo la Nungwi, katika majimbo ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ni Jimbo linaloongoza kwa matangi mengi ya maji na visima vingi havipungui vinne. Lakini mpaka leo hii ninavyokwambia muda huu niliosimama hapa katika jimbo ambalo lina usumbufu wa maji hakuna kama la Nungwi.

Mhe. Spika, tumehangaika sana akiwemo na Mhe. Mwakilishi wangu wa jimbo na tunajitahidi sana kwenda mbio kuhusiana na suala hili, lakini bado tunashindwa na ukizingatia matangi yetu yale yote yamejaa maji *full* na mpaka wale watengenezaji wanashindwa jinsi kufanya kule wakapata kupunguza yale maji ili maji yakaja mitaani, hatujui tatizo ni nini.

Je, Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri unatuahidi vipi kutusaidia juu ya tatizo hili ili tuweze kunufaika na sisi katika Jimbo letu la Nungwi pamoja na wananchi wetu wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ninakubali kwamba kuna upungufu na hii inatokana na mahitaji makubwa ya maji. Kama tujuavyo kwamba Nungwi imekua, lakini hata hivyo nimwambie basi kwamba kupitia Mwakilishi wa Jimbo husika tayari tumekutana, kaja ofisini kwangu tumekaa, kwa sababu Jimbo la Nungwi limepakana na Jimbo langu la Kijini, baadhi ya changamoto tuna-*share* kwa pamoja. Kwa hivyo bado haijafika siku tu ya kwenda kuangalia na kutizama namna ya kutatua. Lakini ninamuahidi kwamba siku ambayo tutakubaliana na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi tutakushirikisha ili tushirikiane kwa pamoja.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza niipongeze Serikali kwa kuja na utaratibu wa kuhifadhi maji katika matangi na kuwasambazia wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja kwa Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo.

Kwa kuwa katika matangi haya hasa lile la Welezo na Kijichi, maji mengi yanayotoka na yanayofika katika matangi yale yanatoka katika vile visima vya Mwembemchomeke, Kimara, Misufini, Kinuni, Kianga na vile vya Chamani. Na mpaka hii leo Serikali kwa makusudi kabisa imeshindwa kurudisha miundombinu kutoka kwa matangi yale kuwarudishia maji wananchi wa Jimbo la Mwera.

Je, ni upi sasa mkakati wa Serikali katika kuhakikisha miundombinu ile ya maji inatoka katika matangi yale na inarudi katika kuwahakikishia wananchi wangu wa Jimbo la Mwera kwa ujumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli hutokezea pale ambapo kwa sasa vipo visima maeneo ya pale yakawa yanakosa maji. Lakini katika ziara zangu nimegundua kwamba mara nyingi visima vinakuwepo kabla na miundombinu yake inayopita katika sehemu husika na vijiji vinavyofuata. Sijawa na uhakika kamili katika eneo lake kama ni *case* hii.

Nimuahidi tu kwamba tutapanga ratiba na yeye tutembee katika jimbo lake tutizame tatizo ni nini na namna ya kulitatua ili tushirikiane kwa pamoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha lakini kwa kuwa Kanuni inaniruhusu naomba nitumie muda uliobaki tulimalize swali la mwisho lililobaki ili tuweze kupunguza maswali tuliyonayo. Kwa hivyo Katibu tuendelee.

Nam. 34
Vifaa Vya Kisasa Vya Kupakulia Mizigo Bandari ya Malindi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**
Kwa kuwa Bandari ya Zanzibar ni moja ya sehemu muhimu sana katika ukusanyaji wa mapato hapa Zanzibar. Na kwa kuwa imeonekana kuwa huduma

za upakuzi na upakiaji wa mizigo zinachelewa sana kutokana na uhaba wa vifaa, na hivyo kupelekea meli kuchelewa sana kuteremsha au kupakia mizigo. Na kwa kuwa kutokana na usumbufu huo umepelekea kurundikana makontena mengi baharini na hivyo baadhi ya kampuni kutaka kususia kuleta meli zao Zanzibar.

a) Je, Serikali haioni kuwa kutokuimarisha huduma za bandari ni kuikosesha Serikali mapato mengi.

b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta vifaa vipya na vya kisasa ili kurahisisha huduma za bandari.

c) Je, mpango wa usafirishaji kutaka kuanzisha kodi ya Zanzibar *Port Conjuction Fee* haioni kuwa ni kuongeza gharama kwa wafanyabiashara na kuongeza ukali wa maisha kwa mwananchi wa kawaida.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe.Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kama ifuatavyo;-

Mhe. Spika, kwanza napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa tatizo la kurundikana makontena bandarini linatokana na sababu zifuatazo:-

1. Ufinyu wa Bandari yenyewe ambapo kuna Gati moja tu inayohudumia Meli kubwa za kigeni yenye uwezo wa kufunga meli moja tu kwa wakati mmoja.
2. Ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena na mizigo mengine.
3. Wenye meli kuleta meli zao kwa pamoja wakati Bandari ya Malindi ina gati moja inayoweza kuhudumia meli moja kwa wakati mmoja.
4. Upungufu wa vifaa vya kutosha vya kuhudumia makontena pamoja na wafanyabiashara kuchelewa kuondoa mizigo yao bandarini.

(a) Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha huduma za Bandari ya Malindi kwa mujibu wa uwezo wa kifedha uliopo, kwa mfano mwaka 2014/15 ilivunja mabanda ya

zamani ya Afisi Bandarini ili kupata eneo zaidi la kuhifadhia makontena ambapo kiasi cha eneo la mita za mraba 3,000 lenye uwezo wa kuweka makontena 500 lilipatikana baada ya kuliimarisha eneo hilo kwa kuweka sakafu ya zege.

Aidha, mwaka 2014/15 Shirika lilinunua Tagi kubwa yenye uwezo wa kuhudumia meli kubwa za mizigo ili kuimarisha huduma za meli. Pamoja na hatua hizo, Wizara yangu inaona suluhisho la kudumu la tatizo hilo ni kupata Bandari mpya katika eneo la Mpigaduri.

(b) Katika kuimarisha Bandari za Malindi na Mkoani, Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari limefanikiwa kununua vifaa mbalimbali vya kuhudumia mizigo ndani ya mwaka wa Fedha 2015/16, vifaa hivyo vimegharimu kiasi cha T.shs.Bilioni 11.03**.** Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na Kreni 2 ambazo zote zimeshafika, *Terminal Tractor 2, Trailer 2, Reach stacker 2, Fork Lift 3* na *Empty Handler 1* ambavyo baadhi yake tayari vimeshapokelewa pamoja na maboya saba na *solar* 7 na taa.

Vile vile ninapenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kupitia Baraza lako Tukufu kwamba *Reach Stackers* zetu nazo zishakaribia kuwasili kwani kesho tu tunatarajia kuzipokea bandarini. (*Makofi*).

(c) Pamoja na changamoto hizo, Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inaendelea na taratibu zake za kuwahimiza Wafanyabiashara na wenye Meli kuondoa makontena yao kwa wakati. Aidha, hivi karibuni Serikali ilikaa pamoja na wenye meli na kujadiliana juu ya ada iliyowekwa na wenye meli *("Congestion Surcharge"),* ambapo wenye meli walikubali kuiondoa ada hiyo mara tu msongamano wa meli utakapopungua bandarini.

Kuhusu kuanzisha kodi ya *Zanzibar Port Congestion Fee* ninapenda Mhe. Mwakilishi kwamba Shirika la Bandari halina nia ya kuanzisha kodi ya namna hiyo, kwani inajali maslahi ya wananchi wake.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza ninampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu majibu yaliyokuwa fasaha yasiyo shaka ndani yake, na vile vile shukurani za pekee ninampongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bandari, kwa sababu haya yote aliyojibu Mhe. Naibu Waziri hayana shaka, mimi mwenyewe nimekuwa shuhuda kwamba kweli vyombo vimefika na ninapongeza sana katika hilo.
Swali langu la ziada linakuja. Kama unavyofahamu kwamba katika kipindi kilichopita cha bajeti tulizungumzia kadhia nzima ya mrundikano wa

makontena ndani ya bandari, na si muda mkubwa ukatoka uamuzi kwamba tukapewa eneo la kuegesha makontena yetu katika kiwanja cha Bwawani kwa muda wa miezi sita.

Je, Serikali imejipangaje baada ya kumalizika miezi hiyo ambayo inategemewa mwezi wa Disemba kuna na njia mbadala kwa kuondoa kontena zile ili kuondosha usumbufu kama ambao uliojitokeza mwanzo kutokana na msongamano wa makontena bandari.

Suala la pili. Kama unavyosema bandari ni sehemu muhimu sana katika maisha ya Wazanzibari, lakini bandari hiyo sasa hivi imekuwa na mrundikano au mkusanyiko wa taasisi mbali mbali zisizopungua kumi na tatu ndani ya bandari ile. Ama mionzi sijui, kuna *ZBS*, kuna Bodi ya Afya na nyenginezo. Imekuwa inatoa usumbufu kwa wafanyakazi wa bandari pamoja na wafanya biashara. Je, kama Serikali tatizo hilo imelionaje na italitatua vipi ili kuweza kuwatatulia matatizo wafanyakazi wa bandari ile pamoja na wafanyabiashara wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kusema kweli kama tunavyojua na kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba, tunajua kuwa kunakuwa na mrundikano wa makontena, lakini kama nilivyosema kwa hivi sasa tuna eneo la Bwawani pale, na kweli msongamano umepungua kwa kiasi kikubwa, na hivi sasa tumejipanga kwa hatua mbili. Kwanza hivi sasa tumeshalitafuta eneo ambalo iwapo mwekezaji mwenyewe atalitaka eneo lake, basi kuna eneo la kwenda kuweka hayo makontena ambapo tutaweza kuyahifadhi makontena yale.

Pili, tuko katika mpango wanasema wa kuangalia, kama, je, huu utaratibu wa kuanzisha bandari kavu utakuwa una faida kwetu. Iwapo utakuwa na faida kwetu basi hatutosita kuendelea na huu mpango. Lakini napenda kumuarifu tu kwamba hivi sasa tuko katika hatua ya awali ya kuwaachia wataalamu wetu watuletee, wenyewe wanasema kwamba uchambuzi yakinifu, baadae tuupeleke katika vikao vinavyohusika, likiwemo Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kujengewa hoja na kupitiwa kabisa. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Swali la pili sasa, napenda kumjibu kuhusu kuwepo kwa taasisi nyingi. Kama unavyojua kwamba bandari ni sehemu ambayo kuna huduma za aina tofauti zinapatikana, kuna Taasisi ya Zimamoto, kuna Taasisi wanasema za Afya, kuna Taasisi ya Kilimo pale kuhusu mambo ya bidhaa zinazoingia. Kwa hivyo, huu

ni mpango tu ambao unakuwepo, na wafanyakazi kusema kweli mimi kila siku huwa niko nao karibu, kama alivyosema mwenyewe pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari. Iwapo kutakuwa na tatizo basi sisi tutakaa kama wizara ili kuhakikisha kwamba hayo matatizo anayosema Mhe. Mwakilishi ambaye pia ni mdau mkubwa wa Bandari basi tunayatatua ipasavyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nimekuona Mhe. Maryam Thani Juma kwa swali la nyongeza.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa swali mama limeeleza kwamba Bandari za Zanzibar ni moja ya sehemu muhimu sana katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, wanaitegemea sana Bandari ya Wete ukizingatia wafanyabiashara wengi wanatumia bandari hii kwenda kufanya biashara Tanga kuja Pemba na Unguja kuja Pemba.

Je, ni sababu gani zilizopelekea hadi leo Bandari hii ya Wete kutoanza ujenzi au kuanza matengenezo. Je, serikali haioni tunaikosesha mapato serikali yetu. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, nadhani unaweza kulijibu, ni swali jipya lakini naomba ulijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Sawa, naweza kulijibu.

Ahsante sana Mhe. Spika. Ni kweli kabisa kwamba tunakiri kwamba Bandari ya Wete ni bandari muhimu sana katika kuendeleza usafirishaji kwa upande wa Pemba. Hivi sasa Shirika la Bandari limeshaanza matengenezo kwa zile sehemu ambazo ilikuwa zamani zikituama maji, na tumeshatumia takriban shilingi milioni zaidi ya 200.

Vile vile tunaendelea na mazungumzo na mwekezaji ambaye ameonesha nia ya kutaka kuwekeza katika bandari ile ya Wete, kwa sababu ya kufunga meli zake pale, tupo katika hatua nzuri ya mazungumzo na ninamuhakikishia kwamba mazungumzo hayo yataleta tija ili baadae ile Bandari ya Wete itumike kwa

vyombo vinavyokwenda Tanga hadi Mombasa vile vile, kwani baadae tuna *route* ambayo tunataka sisi tuitumie, wacha ile ya sasa hivi ya Maendeleo kwenda Tanga. Pia vyombo hivi vya *Sea Link* ambavyo mwekezaji wake ndio anataka kuwekeza pale, ana nia ya kutumia ile sehemu kwa ajili ya meli zake kwenda sehemu nyengine zaidi, kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa wananchi wetu, hasa wale wa Pemba wanaokwenda Tanga na Mombasa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji, lakini nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha, mazuri na ya ufuatiliaji wa kazi. Nina swali moja dogo tu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa umekiri kuwa kuna ufinyu wa bandari, na kwa kuwa kuna mpango wa muda mrefu usiofikia kikomo wa kujenga Bandari ya Mpigaduri imekuwa hadithi. Je, ni lini bandari hiyo itajengwa.

(b) Kwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji alipata kuumwa na kichwa muda mwingi kwa kuweka makontena sehemu ambayo tumepewa miezi sita. Je, ni sehemu gani mbadala ambayo serikali imeweka, ili wafanya biashara waishi kwa matumaini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sisi kama alivyosema mwenyewe tunajua kwamba Bandari ile ya Malindi sasa hivi imekuwa finyu na Mhe. Rais amekuwa kila siku akilizungumza suala hilo na akisisitiza.

Ni hivi karibuni tu walikuja wataalamu kutoka China ambao walichukua *sample* ya udongo na kwenda kuangalia aina ya udongo uliopo pale.

Vile vile wataalamu na viongozi wakuu wa Benki ya Exim kutoka China ambao ndio watatupa mkopo, wamekuja juzi na hivi karibuni tu tulikuwa katika sherehe za kutimiza miaka 66 ya Jamhuri ya Watu wa China na Mhe. Balozi mdogo wa China ametuahidi kwamba ile miradi yote mikubwa ambayo nchi yake imeingia mkataba na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi wataitekeleza kikamilifu. Nina imani kubwa sana kwa mradi wa Mpigaduri wakati wowote utaanza, na sisi wizara tumetenga milioni 400 za kuanzia katika kuweka eneo lile sawa.

Kuhusu eneo ambalo wapi makontena yatawekwa. Sisi kama nilivyosema kule eneo la Mpigaduri kuna eneo kubwa sana tu ambalo sisi tumesema iwapo mwekezaji mwenyewe wa hoteli ya Bwawani atalichukua eneo lake, tutakwenda kuweka makontena yetu kule Mpigaduri. Kwa hivyo, namuondoa shaka na vile vile nawaondoa shaka wananchi kwamba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, iko tayari kutetea maslahi ya wananchi wake na kuhakikisha kwamba inatekeleza yale iliyoahidi kwa kupitia ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015/2020, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umemalizika, kabla hatujaendelea naomba nitoe matangazo machache.

Kwanza kabisa naomba nitambue uwepo wa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, ambaye bila shaka yuko hapo, kwa sababu Mhe. Waziri muda sio mrefu atatoa kauli ya serikali kuhusu jambo ambalo linamgusa yeye pia.

Waheshimiwa Wajumbe, jambo jengine ni kwamba kesho tulikuwa tumepanga kuupitisha mswada wetu ule wa katiba, lakini baada ya hapo kwenye ratiba yetu tunazo kanuni, lakini itakumbukwa kwamba kabla ya kuletwa kwa kanuni hizo tulikubaliana kwamba tufanye semina turidhishane sote wajumbe wote pamoja na serikali, lakini kwa bahati mbaya sana tulikosa muda wa kufanya hivyo, kwa sababu shughuli zilikuwa zimejibana mno. Kwa hivyo, ningependa sana kupendekeza kwamba kanuni tuziondowe kwenye shughuli za kesho, tubakiwe na suala la katiba, mpaka hapo tutakapoweza kukaa pamoja kwenye semina, ili kuweza kujiridhisha, kwa sababu kanuni hizo ndizo ambazo tutakuwa tunazitumia kwa ajili ya kuendeshea shughuli zetu humu ndani.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo nina matangazo mawili. Tangazo la mwanzo ni kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambaye anaomba kamati yake ikutane kwenye ukumbi wa hapo juu, mara baada ya kumalizika kwa hizi shughuli. Kwa hivyo, kamati ikutane kwenye ukumbi namba 3 hapo juu, wanasema baada ya kauli ya serikali.

Pia naomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambao na wao wanaombwa na Mwenyekiti wao wakutane saa 4:30. Ni leo hiyo

Mimi napenda kutahadharisha tu kwamba, jaribuni kuangalia na *quorum* humu ndani ya ukumbi kabla hamjaitisha hiyo mikutano ya wenyeviti wa kamati, kwa sababu hizi shughuli zinazoendelea pia ni muhimu. Kwa hivyo, aidha iende

kamati moja kwanza baada ya kurudi ifuate na hiyo ya pili. Baada ya matangazo hayo sasa katibu kwa shughuli inayoendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 63, nataka niisome nafikiri utakuwa umeshaifahamu Mhe. Spika. Sijui nina haja ya kuisoma au utakuwa umeshaifahamu kanuni ya 63.

Mhe. Spika: Enhe, endelea na hiyo *issue* yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwanza. Hapa si muda mrefu umepokea kauli ya serikali, lakini kipindi kilichopita na vizuri Mhe. Spika, nilikuwa na Hansard hii aliyoitoa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

"Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku kabla ya kufunga Baraza hili tutaleta taarifa, siku zilizobaki ni kidogo, karibu tutamaliza, nina hakika hili tutalileta".

Habari hii ya ng'ombe serikali ilijifunga katika kikao kilichopita wataileta, lakini nashangaa imekuja muda huu. Nataka muongozo wako Mhe. Spika, serikali ilikuwa, sijui tuseme ilikwenda likizo au ilikuwa imepumzika au vipi, huku wame...

Mhe. Spika: Yaani sijakufahamu Mhe. Jaku Hashim kwamba kauli iondolewe mezani sio hutaki kuisikia au vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, labda nizungumze kidogo kidogo ili upate kunifahamu.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita serikali iliji- *commit* kwa kupitia chombo hiki humu ndani. Kwa Hansard ambayo ninayo ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani saa 8:30 mchana, tarehe 27/06/2016, nilihoji humu ndani Mhe. Spika, na wewe shahidi ulikuwepo. Serikali iliji- *commit* ikasema kwamba, 'hatutomaliza kikao kile itakuja na kauli ya serikali kuhusu suala la ng'ombe, lakini nashangaa imekuja leo, na sijui utaratibu unasemaje katika hili Baraza letu. Kusema kweli au kusema lugha pengine.

Mhe Spika: Nimekuelewa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ni kweli serikali ilitaka kufanya hivyo wakati ule, lakini hatukuwa na nafasi kwa shughuli hiyo sisi tunaopanga shughuli za Baraza, nafasi tumeipata sasa hivi. Kwa hivyo, kauli

hiyo utaisikia sasa hivi. Baada ya hapo naomba tuendelee na shughuli zinazofuata. Katibu. *(Makofi)*

KAULI ZA SERIKALI

Kauli ya Serikali Kuhusu Zoezi la Uondoshaji wa Wanyama Katika Maeneo Yasiyoruhusiwa Katika Manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha kauli ya serikali kuhusu zoezi la uondoshaji wa wanyama katika maeneo yasiyoruhusiwa katika Manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na taifa kwa jumla. Tumuombe Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema atupe uwezo wa kuyatekeleza yale yote ambayo tumepanga kuyatekeleza katika mwaka huu wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba uniruhusu niwasilishe kauli ya serikali kwa mujibu wa kanuni ya 43(1),(2), mpaka (3) toleo la Aprili, 2012. Kifungu hiki kinanipa uwezo wa kuwasilisha kauli ya serikali katika Baraza kuhusiana na jambo ambalo serikali inahitaji kuliarifu Baraza katika kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake. *(Makofi)*

Madhumuni ya Kauli hii

Mhe. Spika, madhumuni ya kauli hii ni kuliarifu Baraza la Wawakilishi kuhusu zoezi lililofanyika na linaloendelea kufanyika la kuwaondosha wanyama katika maeneo yasiyoruhusiwa ndani ya Manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi na katika Mabaraza ya Miji Pemba. Kwa hivyo, naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watoe mashirikiano ili zoezi hili liweze kuendelea kama ilivyokusudiwa na serikali.

Chimbuko la Taarifa hii

Mhe. Spika, chimbuko la taarifa hii ni ahadi ya serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais aliyoitoa katika Baraza la Tisa, Mkutano wa Pili wa Baraza la Wawakilishi, ahadi hiyo ilitolewa kufuatia hoja za Waheshimiwa Wawakilishi, wakati wa mjadala wa kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya

Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango juu ya zoezi la uondoshwaji wa wanyama katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mhe. Spika, katika hoja zilizotolewa wajumbe walitaka serikali kuwasilisha Barazani taarifa rasmi, ili kuelezea taratibu za zoezi zima lilivyoendeshwa ili kuondoa manung'uniko miongoni mwa wafugaji na wahusika wengine.

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, zoezi la kuwaondosha wanyama katika maeneo yasiyoruhusiwa ni zoezi endelevu, zoezi hilo lilianza tarehe 26/05/2016 na litaendelea kufanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Kwa kuwa wajibu wa kusimamia na kufuata sheria za nchi ni jukumu la kila mmoja wetu, hivyo basi kwa kuhusiana na zoezi hili serikali kwa kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imedhamiria kusimamia utekelezaji wa sheria hizi, ili kurejesha nidhamu katika miji na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, utekelezaji huu wa sheria umekuja kutokana na kukithiri kwa uvunjifu wa nidhamu kwa baadhi ya wafugaji, katika maeneo tofauti ya manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi na miji yetu ya Pemba. Jambo hili linapelekea uchafuzi wa mazingira, kuharibu haiba ya miji na mara kadhaa kusababisha misongamano barabarani na hatimaye ajali zisizo za lazima.

Aidha, matukio kadhaa ya kihalifu yamekuwa yakiripotiwa ambayo husababishwa moja kwa moja na kuwepo kwa wafugaji wa wanyama hao, hususan ng'ombe na punda. Matukio hayo ni kama vile wizi wa vifaa vya ujenzi, kama matofali, mawe na kadhalika, migogoro baina ya wafugaji na wakulima, uharibifu wa miundombinu ya umeme, maji, majengo, ugomvi na kujeruhiana kwa kutumia mapanga miongoni mwa makundi ya waendesha magari ya ng'ombe na punda.

Mhe. Spika, kwa jumla zoezi la kuwaondosha wanyama katika maeneo yasiyoruhusiwa, limefanyika kwa mafanikio makubwa, ni nadra sana kwa sasa kuona mifugo ikizagaa barabarani na kwenye maeneo mengine yasiyoruhusiwa mjini. Mwanzoni kulikuwa na changamoto za kutoitikiwa vyema agizo hili la serikali, kwa kiasi kikubwa changamoto hiyo ilisababishwa na mazoea ya kutokufuatwa sheria, na ingawa pia kulikuwa na madai kuwa, wafugaji na wamiliki wa mifugo hawakupatiwa taarifa za kutosha juu ya zoezi hili. Hata

hivyo, juhudi za makusudi zilichukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa za kutoa taarifa kwa umma juu ya uamuzi huu wa serikali.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa zoezi hili yapo mafanikio mengi ambayo yamepatikana yakiwemo kama hivi ifuatavyo.

(a) Wananchi kuanza kubadili tabia na kuamini kuwa sasa uondoaji wa wanyama ni jambo la kisheria na lazima lifuatwe.
(b) Kupungua kwa wanyama katika maeneo yaliyokatazwa.
(c) Kukamatwa kwa jumla ya wanyama 146, kati ya hao ng'ombe 99, punda 19 na mbuzi 28
(d) Kupungua ajali za barabarani zinazosababishwa na wanyama hao.
(e) Kuanza zoezi la muitikio wa wananchi kuwakomboa wanyama wao, ambao hadi sasa jumla ya ng'ombe 45 na punda mmoja wamegombolewa na wamekabidhiwa wenyewe.
(f) Kupungua kwa kiasi kikubwa uchimbaji ovyo wa mchanga uliokuwa ukifanywa na vijana wa magari ya ng'ombe na punda.
(g) Kuhuika kwa vipando pamoja na bustani katika maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuvishukuru na kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa waliyoifanya wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo. Vikosi hivi vilifanya kazi bila ya kuchoka katika mazingira magumu yaliyokosa ushirikiano. Busara na ustahamilivu viliwasaidia sana kukabiliana na changamoto walizokumbana nazo, mpaka leo sisi sote tunaamini kuwa serikali imefanikiwa katika zoezi hili.

Aidha, nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wote walioitikia wito wa kuondosha wanyama wao, katika maeneo ya mijini Unguja na Pemba, nawaomba waendelee kushirikiana na serikali katika kusimamia jambo hili, hasa kwa kutoa taarifa juu ya wale wachache ambao bado wanaendelea kuhalifu agizo hili la serikali.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, itaendelea kushirikiana na wahusika wengine mbali mbali ikiwemo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika kuwajengea mazingira wezeshi wafugaji wetu huku tukiendelea kutunza haiba ya miji bila ya kuhitalifiana.

Shukurani

Mhe. Spika, mwisho naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ustahamilivu wao wa kuniruhusu kutumia muda wao katika kuileta kauli hii ya Serikali mbele ya Baraza.

Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla wameelewa nia ya Serikali katika utekelezaji wa zoezi hili na tutasaidia kuwaelimisha wananchi zaidi ili zoezi hili liende vizuri kama ilivyokusudiwa. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Kanuni ya 43(1) kanuni za Serikali inasema Kiongozi wa Shughuli za Serikali au Waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo Serikali inawajibika, baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya kamati juu ya kauli hiyo.

Kauli za aina hiyo 43(2) zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika, katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambao umewekwa na Kanuni ya 27.

43 (3) Hakutakuwepo na majadilino yoyote kuhusu kauli yoyote itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii. Lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika, kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo kwa madhumuni ya kueleweshwa zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo.

Baada ya maelezo hayo, baada ya kusomwa humo kwenye Kanuni, naomba sasa nichukue nafasi hii kumkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ambayo inahusiana na suala hili ili kama ana maelezo kidogo.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Wawakilishi, kwa bahati mbaya sana labda nitatoa maoni yangu sio ya kamati, kwa sababu hatujakaa kama kamati kujadili taarifa hii.

Kwa hivyo naomba tu basi nirudie kwamba mimi nitoe kama maoni yangu halafu na wajumbe wangu kama wanayo maoni watoe baadae kama na wajumbe wengine kwa mujibu wa kanuni watoe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani sasa hivi umetusomea kanuni kuhusu hoja hii ambayo iliyowasilishwa na kwenye kanuni hii, baadae inaeleza kwamba Mwenyekiti anatakiwa awasilishe ripoti ya kamati.

Sasa kamati haikukaa, Mwenyekiti anasema anawasilisha maoni yake, na katika hoja yoyote inayoletwa kitu kikubwa sisi tunaangalia ripoti ya kamati. Je, walimhoji vipi Waziri, walikubaliana vipi na maoni ya kamati ili na sisi tuweze kuunga mkono yale maoni ya Kamati na kuweza kutia nyama.

Mhe. Spika, sasa hili suala naona kama limekuja kinyume nyume. Mimi ushauri wangu naomba hii hoja tuipokee halafu tuiagize kamati ikae na Wizara waijadili, halafu tupate angalau mapendekezo ya Kamati na sisi tupate muda halafu tuje tuulize maswali, vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, itakuwa tumetunga kanuni halafu tunazikiuka sisi wenyewe.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa labda kwa sababu Mwenyekiti alisema anataka kutoa mawazo yake yeye, mambo yote haya yanafanyika kwa idhini ya Spika kwa sababu inaweza kutolewa kauli hapa kwa mujibu kama itakuwa nimefahamu na isipate maswali.

Lakini kwa idhini yangu nilitaka kuwaruhusu watu wawili watatu waulize maswali tu ili kupata ufafanuzi, lakini kwa sababu mnavyotaka nyinyi sasa mkakae kama Kamati kwanza na hiyo kauli tunakubaliana kwamba hapana swali lolote litakaloulizwa kuhusiana na kauli hii mpaka baada ya kamati kwenda kulifanyia kazi.

Basi baada ya makubaliana hayo mimi nitaruhusu hilo ambalo Waheshimiwa Wajumbe mnaliomba la kamati kwenda kulifanyia kazi kwamba baada ya hapo tutatafuta ili tuje tulifanyie kazi suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika mimi nakubaliana kabisa na ushauri wako, lakini kwa kuwa taarifa hii imeshawasilishwa ningeomba wajumbe waipokee, halafu kama kuna jambo lolote lile la Kamati siku nyengine lifanyike, lakini tuipokee taarifa hii kwamba imeshawasilishwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nadhani hii taarifa imeshapokelewa kama nimewafahamu, wao wameshaipokea *(Makofi)*

Sasa naomba niwahoji wale wote ambao wanakubaliana na kupokea taarifa hii iliyoletwa na Serikali wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria wa kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Nam.8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam.11 ya 2009 na Kuweka Masharti Bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Spika, kwanza, sina budi kutanguliza shukrani kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa wazima wa afya na salama na kuendelea na kazi hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Pili, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Mswada huu mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Wizara yangu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza mswada wa Sheria ujulikanao kama "*A bill for an act to amend the State University of Zanzibar Act. No. 8 of 1999 as amended by Act No. 11 of 2009 and to provide for better provisions and other matters concerned therewith*" wenye lengo la kutunga Sheria ya kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 11 ya mwaka 2009 na kuweka masharti bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo katika kuunganishwa kwa baadhi ya Taasisi za elimu ya juu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako kwamba, Wizara yangu itazingatia kwa dhati michango ya Baraza lako ambayo itasaidia sana katika kurekebisha Mswada huu.

CHIMBUKO LA MSWADA

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kutekeleza azma yake ya kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo cha elimu ya juu kinachotambulikana ulimwenguni *(Centre of Excellence in Higher Education)*. Azma hii imekuja kwa kuzingatia umuhimu wa elimu bora katika kila ngazi, lakini pia kwa kuzingatia umuhimu wa mchango wa elimu ya juu katika kuleta maendeleo ya nchi katika karne hii ya 21.

Katika kufanikisha hili, mara tu baada ya kuingia madarakani, Serikali ya Awamu ya Saba ililifanyia utafiti suala la kuimarisha Elimu ya Juu Zanzibar kwa kuzingatia uwepo wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, na taasisi mbali mbali za Elimu ya Juu za Serikali ambazo zilizoanzishwa chini ya Wizara mbali mbali kwa ajili ya kutoa mafunzo juu ya nyanja za taaluma zinazohusika na Wizara hizo. Taasisi hizo za Serikali za Elimu ya Juu ni 7 kama zifuatavyo:

- Chuo cha Taaluma za Afya chini ya Wizara ya Afya,
- Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo ya Kizimbani *(KATI)* chini ya Wizara inayohusika na kilimo,
- Taasisi ya Maendeleo ya Utalii *(ZIToD)* chini ya Wizara ya inayohusika na Utalii,
- Taasisi ya Uongozi wa Fedha *(ZIFA)* chini ya Wizara inayohusika na Fedha,
- Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume chini ya Wizara inayohusika na Elimu,
- Chuo cha Uandishi wa Habari chini ya Wizara inayohusika na habari, na
- Chuo cha Kiislamu cha Mazizini kilicho chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Tutakumbuka kwamba taasisi hizi zilianzishwa kabla ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa lengo la kupata rasilimali watu kwa ajili ya nyanja husika.

Mhe Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinatakiwa kuanzisha Skuli (Vitivo) katika fani ambazo tayari zinasomeshwa na taasisi za Serikali. Kwa mfano, *SUZA* inatakiwa kuanzisha:-

- Skuli (Kitivo) cha Kilimo;

- Skuli (Kitivo) cha Sayansi za Afya na Tiba (ambacho kimeanzishwa mwaka 2013/2014);
- Skuli (Kitivo) cha Biashara;
- Skuli (Kitivo) cha Uandishi.

Pia baada ya kuidhinishwa na Mkuu wa Chuo kama ilivyo sheria ya Chuo, SUZA inatakiwa pia kuanzisha vitivo vinavyofuata ambavyo vimeainishwa katika Gazeti la Serikali:

- Skuli (Kitivo) cha Uhandisi wa Mafuta na Gesi *(Petroleum Engineering)*
- Skuli (Kitivo) cha Utalii *(Tourism and Hospitality Management)*
- Skuli (Kitivo) cha *TEHAMA (Computing, Communication and Media)*

Mhe. Spika, hapa naomba ieleweke vyema kwamba hapa Skuli haina maana ya Skuli tuliyoizoea kama Skuli zetu za kawaida, bali inamaanisha Kitivo cha kitaaluma katika Chuo Kikuu kwa maana ya *faculty*.

Mhe. Spika, Serikali iliteua wataalamu mbali mbali ndani ya nchi kufanya utafiti huo, na kuishauri Serikali juu ya kuimarisha Elimu ya juu Zanzibar. Wataalamu hao walifanya utafiti huo kwa umakini sana kwa muda wa karibu miaka miwili, na kutoa mapendekezo yake kwa Serikali. Katika mambo ambayo Kamati hiyo iliyagundua ni kwamba Mipango Mikakati ya taasisi nyingi hizi za Serikali ni kutanua wigo na kutoa masomo ngazi ya Shahada, kuwa Vyuo Vikuu. Mfano wa taasisi zenye lengo hilo ni Chuo cha Taaluma za Afya, Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo ya Kizimbani *(KATI)*, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume *(KIST)*, na Taasisi ya Uongozi wa Fedha *(ZIFA)*, na Chuo cha Kiislamu *(CCK)*.

Mhe. Spika, Hali hii kama itaachwa, tujitazame miaka mingi ijayo, tujaalie 10, au hata 20, basi Zanzibar itakuwa na vyuo vikuu vyengine vya Serikali vitano, na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuwa cha sita. Tutakuwa na Makamu Wakuu wa Vyuo Watano, na Manaibu Makamu Wakuu wasiopungua 10, na mabaraza ya Vyuo au Mabodi ya vyuo sita. Vingi ya vyuo hivi havitokuwa chini ya usimamizi wa Wizara yenye mamlaka ya kusimamia Elimu jambo ambalo litakosa udhibiti mzuri wa ubora na viwango vya taaluma zinazotolewa.

Lakini pia, ili kujenga uhalali na kuwa na vigezo vya kuwa vyuo vikuu, taasisi hizi lazima ziongeze masomo na kuna uwezekano mkubwa wa taasisi hizi kuanzisha masomo yanayogongana kati ya taasisi zenyewe, na taasisi na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar jambo ambalo litaifanya nchi yetu ndogo kutotumia vyema rasilimali zake ilizonazo.

Mhe. Spika, Mgongano huo wa masomo yanayotolewa na taasisi hizo na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar tayari umejitokeza na usipodhibitiwa utaendeleza zaidi. Kwa mfano, Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar tayari inakitaka Chuo hicho kuanzisha masomo katika taaluma za Afya, Kilimo, Uhandisi, Biashara na Fedha, na Utalii. *SUZA* tayari imeanzisha masomo katika baadhi ya fani hizo – kama vile Shahada ya Tiba, Shahada ya Afya za Mazingira, Shahada ya Uongozi wa Utalii na Masomo, Stashahada ya Utalii na Urithi wa kale, na imo katika mpango wa kuanzisha Shahada ya Kilimo Hai *(Organic Farming).*

Mhe. Spika, kutokana na haya, utafiti uliofanywa na Kamati ya Ushauri ulipendekeza kwa Serikali kuunganisha taasisi zake za Elimu ya Juu kwa awamu. Kamati ilipendekeza awamu ya kwanza kuzingatia kuunganisha Chuo cha Taaluma za Afya, Taasisi ya Uongozi wa Fedha (*ZIFA*), na Taasisi ya Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*). Kamati pia ilipendekeza mambo mbali mbali ya kufanywa ili kuimarisha *SUZA* baada ya kuunganishwa na taasisi hizo.

Mhe. Spika, napenda kukuarifu kuwa Baraza la Mapinduzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 19 Agosti, 2013 pamoja na mambo mengine Baraza la Mapinduzi liliridhia kuunganishwa kwa baadhi ya Taasisi za Elimu ya Juu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na hatimaye liliiagiza na kuielekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar kwa kushirikiana na *SUZA* na taasisi zitazounganishwa na *SUZA* kuyafanyia kazi mambo yafuatayo:-

1. Kuziarifu rasmi Wizara na uongozi wa taasisi zinazohusika kuhusu maamuzi ya Serikali ya kuziunganisha Taasisi hizo husika.

2. Kuitaka Kamati iliyolifanyia kazi suala la kuziunganisha na *SUZA* baadhi ya taasisi za elimu ya juu kulifanyia kazi zaidi suala zima linalohusu mfumo *(modality)* muafaka wa kuziunganisha taasisi hizo kwa kuangalia hali halisi iliofikwa na kila taasisi.

3. Ishirikiane na Taasisi husika kuanzisha mchakato wa kuifuta sheria za *ZIFA (Act No. 1/2002)* na *CHS (Act No. 10/1998)* na hatimaye kutangaza rasmi kwamba vyuo hivyo vitakuwa ni sehemu ya *SUZA*.

4. Kuanzisha mchakato wa kuirekebisha sheria Na. 8/1999 ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*)

5. Ishirikiane na Kamati husika ili kupata utaratibu muafaka utakaohakikisha kuwa Chuo cha Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*) kinalelewa na *SUZA* kikiwa tayari kimeshaunganishwa na *SUZA* badala ya kulelewa kwa utaratibu wa "kitivo kimya*" (Silent School)*

6. Kuhakikisha kwamba *SUZA* haitayafuta masomo/mafunzo yanayotolewa na Taasisi zinazounganishwa nayo kwa vile masomo/mafunzo yanayotolewa na taasisi hizo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

7. Masomo yanayotolewa na *SUZA* katika ngazi ya shahada yanasajiliwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu (*TCU*) na yanayotolewa katika ngazi ya chini ya shahada (stashahada na cheti) yaendelee kusajiliwa na *NACTE* au *TCU* kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

8. Uongozi wa *SUZA* na Taasisi zinazounganishwa na *SUZA* uimarishwe ipasavyo ili kupata viongozi walio na sifa za kitaalamu na weledi wa kuendesha masuala ya taaluma.

9. Uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Chuo (*SUZA*) uzingatie uwezo wao katika masuala ya taaluma.

10. *SUZA* ishirikiane kwa karibu sana na uongozi wa Taasisi zinazounganishwa na *SUZA* kufanya uchambuzi wa kina utakaobainisha uwezo wa watumishi kisifa na kiuzoefu ili watakaokidhi vigezo vya *SUZA* waweze kuingizwa katika muundo wa Utumishi wa *SUZA*, na wenye uwezo wa kuendelezwa kufikia viwango vya *SUZA* waendelezwe na wale ambao hakuna uwezekano wa kufikia vigezo vinavyotakiwa wapangiwe kazi katika utumishi wa umma kwa mujibu wa sifa zao za kitaalamu, ujuzi na uzoefu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kidogo naomba nimpishe Mwenyekiti ili muweze kuendelea.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia Kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii.

11. Wafanyakazi wa Taasisi zinazokusudiwa kuunganishwa na *SUZA* wapangwe katika ngazi au vyeo vipya kwa mujibu wa kanuni za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Hata hivyo, *SUZA* iangalie uwezekano wa kuliangalia tena sharti la mfanyakazi kuwa na *Ph.D* kama sharti pekee la kufikia cheo cha Mhadhiri Mwandamizi, na ili kuruhusu pia vigezo vyengine muhimu kama uandishi wa idadi fulani ya makala yaliyohakikiwa vyema na wasomi wanaotambulika kimataifa, mchango wake katika kufanikisha malengo ya *SUZA* na kadhalika.

12. *SUZA* ihakikishe kwamba maslahi ya wafanyakazi yanafuata Muundo wa Utumishi *(Scheme of Service)* wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha wafanyakazi wa uendeshaji waliopo katika Taasisi zinazokusudiwa kuunganishwa na *SUZA* na kutoka *SUZA* yenyewe wanaweza kubadilishwa ofisi ndani ya *SUZA* kulingana na uwezo wao kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi za Chuo.

13. *SUZA* ishirikiane na Taasisi zinazokusudiwa kuunganishwa nayo kuunda kamati ya kuweka mambo sawa *(harmonization committee)* itakayojumuisha wajumbe wa Taasisi hizo zikiwemo Jumuiya za Wanafunzi na walimu kwa lengo la kupitia na kuweka mambo mbali mbali yanayohusu uendeshaji wa Chuo.

14. Wizara kwa kushirikiana na *SUZA* iangalie uwezekano wa kuongeza mishahara ya wanataaluma kwa mujibu wa hali ya uchumi na uwezo uliopo, na wakati huo huo kuondokana na tabia iliyojengeka vyuoni kwa wanataaluma kutaka kulipwa kwa kila kazi wanayoifanya Chuoni ikijumuisha kuhudhuria kwenye vikao mbali mbali vya Kamati za Chuo.

15. Kuandaa Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* wa miaka mitatu 2013/2014-2015/2016 na Mpango wa Utekelezaji *(Action Plan)* wa kila mwaka kuhusu namna ya kuziunganisha na *SUZA* taasisi zinazohusika utavyotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliyafanyia kazi masuala haya kwa kushirikiana na *SUZA* na taasisi zote husika. Na hatimaye mapendekezo ya Wizara yaliwasilishwa Serikalini. Kati ya mapendekezo hayo, ni mswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha *SUZA* ambao umetukutanisha leo hii hapa.

Kikubwa cha kuzingatia hapa ni kwamba Mswada huu umefikiwa baada ya kazi kubwa ya utafiti uliofanywa na wataalamu wetu, na ambao uliwashirikisha kwa ukaribu sana wahusika na wadau mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuunganisha Taasisi za Serikali na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar si geni katika Serikali yetu. Tunakumbuka kwamba Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah ambavyo vilikuwa chini ya Wizara ya Elimu, na ambavyo vina historia kubwa sana kuliko vyuo tunavyotaka kuviunganisha na SUZA hivi sasa. Taasisi hizi ziliunganishwa na SUZA ili kuimarisha Chuo hicho na kuondoa migongano ya taaluma zitazosomeshwa.

Ni mwaka jana tu, mtakumbuka Wizara yangu iliunganisha Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa cha Pemba na kuwa ni sehemu ya SUZA.

Mhe Mwenyekiti kutokana na uzoefu wa Wizara wa kuunganisha Taasisi za Serikali na SUZA, tumeweza kuona faida mbali mbali zilizopatikanwa kutokana na hatua hizo ya Serikali. Kwa mfano:

- Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ambayo kwa miaka kama 30 imekuwa ikisomesha masomo ya ualimu na lugha katika ngazi za Diploma, sasa imepandishwa daraja kuwa Kitivo cha Chuo Kikuu na kinatoa taaluma katika ngazi zote mpaka PhD. Kitivo hicho kinatoa PhD ya kwanza ya Kiswahili ulimwenguni inayosomeshwa kwa Kiswahili.
-
- Chuo cha Ualimu ambacho kilisomesha masomo ya Ualimu mpaka ngazi ya Diploma, kwa ajili ya walimu wa masomo ya kawaida ya sanaa na sayansi tu, sasa kimekuwa ni Kitivo cha Chuo Kikuu na kinatoa taaluma mbali mbali za ualimu kama vile ualimu wa elimu mjumuisho, ualimu wa elimu ya awali, ualimu wa michezo, uongozi wa elimu, na kadhalika.

- Kwa kupitia SUZA, uwezo wa wanataaluma umeweza kujengwa zaidi. Kwa mfano taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni haikuwa na walimu wenye PhD. Hivi sasa SUZA inajenga uwezo wa walimu wake 9 kuwa na hadhi za PhD. Hali kama hiyo inaonekana katika Kitivo cha Ualimu cha SUZA ambacho kinaendeshwa na wafanyakazi kadhaa wenye PhD, na wengine wako masomoni.

- Kuondoa mgongano kwa masomo ambayo yangetolewa Chuoni na Taasisi hizo kama zisingeunganishwa

- Kuimarisha ubora wa masomo yanayotolewa, kwani vigezo vya masomo chini ya Chuo Kikuu viko juu zaidi kuliko taasisi za chini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia mafanikio hayo, kwa ufupi faida zitakazopatikana kwa kuunganishwa Chuo cha Taaluma za Afya, *ZIFA* na *ZIToD* na *SUZA* ni kama zifuatazo:

1. Kuwa na Chuo kimoja kilicho imara na chenye kutoa masomo mengi zaidi;
2. Kutoa taaluma zenye ubora zaidi;
3. Kuwezesha kutumia rasilimali chache vizuri;
4. Kupunguza gharama za kuendesha vyuo vingi hapo baadae;
5. Kuepusha vyuo kadhaa kutoa masomo hayo hayo *(duplication);*
6. Kuweza kusimamia vyema elimu ya juu na taaluma zinazotolewa na serikali kwa kuwa elimu ya juu chini ya wizara moja.
7. Kuweza kuvisaidia vyuo vidogo vidogo kuweza kutoa masomo ya juu zaidi.

Mhe Mwenyekiti, katika miaka ya karibuni, nchi wahisani na wafadhili mbali mbali zimekuwa zikitilia mkazo suala la kuimarisha vyuo vikuu katika nchi zinazoendelea kwa kutambua umuhimu wa vyuo vikuu katika kuleta maendeleo ya nchi. Misaada hii huchangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga uwezo wa walimu wetu kwa kuwasomesha kwenye ngazi za juu kama vile PhD, kwa kuanzisha masomo mbali mbali yanayohitajika na jamii, na kununua vifaa mbali mbali kwa kuendeshea masomo hayo.

Uzoefu tulionao ni kwamba kwa vile misaada hii hulenga taasisi zenye hadhi za Vyuo Vikuu, basi licha ya taasisi zetu kutoa masomo katika fani zinazotaka kusaidiwa hupelekea kukosa fursa hizo. Kwa mfano, nchi ya Denmark imekuwa ikidhamini mradi uitwao “Kujenga Vyuo Vikuu Imara” *(building Stronger Universities)* kwa awamu ya kwanza ulihusisha masomo ya afya na tiba. Chuo cha Taaluma za Afya pekee hakikuweza kunufaika na msaada huo, na kililazimika kuungana na SUZA katika kutuma mapendekezo kwa pamoja, na katika hatua ya pili mradi huo, chuo hicho hakikuweza kunufaika kabisa. Mradi huo umeweza kusomesha wafanyakazi kadhaa, na kuanzisha somo la “Shahada ya Sayansi ya Afya za Mazingira” ambayo inatolewa na SUZA.

Mfano mwengine ni misaada ya *USAID* juu ya taaluma za kilimo. *KATI* na Chuo cha Kilimo Kizimbani hulazimika kuungana na SUZA katika kuwasilisha hoja ya kujiunga na miradi ya taasisi hiyo ambayo hutumika kujenga uwezo wa vyuo. Hivi karibuni, Chuo Kikuu cha *Kassel* cha Ujerumani, kwa kushirikiana na Kampuni moja inayohusika na Kilimo Hai walikuwa na azma ya kuanzisha masomo ya kilimo hai hapa Zanzibar kwa kupitia Wizara inayohusika na Kilimo. Kwa vile azma ya wahisani hao ni kuanzisha masomo hayo katika ngazi ya Shahada, mradi huo haukuwezekana kufanywa *KATI*, na badala yake Wizara inashirikiana na *SUZA* kwa kuihusisha *KATI*.

Malengo ya mradi huo pia ni kujenga uwezo wa wafanyakazi wa *KATI* na *SUZA*, kuanzisha somo hilo, na kununua vifaa mbali mbali kwa ajili ya masomo hayo.

Mifano ya miradi hiyo ipo mingi ila la kuzingatia hapa ni kwamba miradi kama hii itasaidia kujenga uwezo wa taasisi hizi kwa haraka zikiwa chini ya *SUZA*.

HALI HALISI NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE

Mhe. Mwenyekiti, kuunganishwa Vyuo ni jambo ambalo limefanywa na nchi mbali mbali. Baadhi ya nchi zimeunganisha vyuo au kubadilisha majina vyuo ambavyo vimekuwepo miaka mingi kabla. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Aalto cha Finland kilianzishwa mwaka 2010 baada ya kuunganisha Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Helsinki kilichoanzishwa tokea mwaka 1849 na Chuo cha Sanaa na Ubunifu cha Helsinki ambacho kilianzishwa tokea mwaka 1871, na Chuo cha Uchumi ambacho kilianzishwa mwaka 1849.

Urusi, wakati ikiwa katika *USSR*, ilianzisha vyuo vya masomo maalumu katika kila jimbo *(state).* Kila jimbo lilikuwa na Vyuo angalau vitano, yaani Chuo Kikuu cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Afya, Chuo Kikuu cha Uhandisi, Chuo Kikuu cha Uongozi, Sanaa, na kadhalika. Kwa ujumla Urusi ilikuwa na vyuo 969. Ikisukumwa na haja ya kupunguza gharama, kwa miaka saba sasa Urusi inatekeleza mpango wa kupunguza vyuo hivyo kwa kuunganisha vyuo katika mataifa yake. Hivi sasa idadi ya vyuo hivyo imefikia 400, na lengo ni kuvipunguza na kuwa 280.

Katika nchi jirani ya Rwanda yenye watu karibu milioni 12, mwaka 2013 vyuo vikuu na taasisi saba za nchi hiyo ziliunganishwa na kufanya Chuo kimoja kiitwacho Chuo Kikuu cha Rwanda. Vyuo na Taasisi zilounganishwa ni:-

- Chuo Kikuu cha Taifa cha Rwanda
- Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Kigali
- Taasisi ya Elimu ya Kigali
- Taasisi ya Kilimo na Mifugo
- Taasisi ya Fedha na Taaluma za Benki
- Taasisi ya Juu ya Umutura Polyteknik
- Taasisi ya Afya ya Kigali

Kwa mujibu wa vyanzo vya taarifa hii, Serikali ya Rwanda ilifanya uamuzi huo kwa lengo la kuimarisha ubora wa Elimu katika nchi hiyo, na kukiwezesha Chuo hicho kuweza kutimiza mahitaji ya nchi na ulimwengu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyogusia hapo awali, hata hapa Zanzibar kuunganisha taasisi na vyuo vya Serikali sio jambo geni. *SUZA* iliunganishwa na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Chuo cha Ualimu cha Nkrumah, na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa cha Pemba.

Cha kuzingatia ni kwamba nyingi ya taasisi hizi za Serikali zilianzishwa kabla ya *SUZA*, na zina malengo yale yale ya *SUZA*.

Chengine cha kuzingatia ni kwamba nyingi ya taasisi hizi hubakia kutoa masomo katika ngazi za Vyeti na Stashahada tu kwa muda mrefu. Kwa mfano *KATI*, *KIST*, Chuo cha Taaluma za Afya, na hata mfano wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah. Taasisi hizi zina muda mrefu lakini bado hazina uwezo wa kutanua masomo yao katika ngazi za juu zaidi ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, hata Taasisi ya *ZIFA* ambayo imeweza kuanzisha masomo katika ngazi ya Shahada kutokana na mahitaji ya viwango vya walimu kufundisha masomo hayo, basi Taasisi hiyo haina uwezo. Kwa taarifa tu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imeagiza kwamba kuanzia mwaka wa masomo wa 2016/2017 unaotarajiwa kuanza mwezi wa Oktoba, masomo yote yanayotolewa na vyuo katika ngazi za shahada na kuendelea juu lazima yapitishwe *TCU*. Walimu wengi wa *ZIFA* wanaosomesha masomo katika ngazi ya shahada hawana vigezo vinavyokubalika na *TCU* kiasi cha kuhatarisha kufungwa masomo hayo.

Ni imani ya Serikali kwa kuunganishwa na *SUZA*, na hivyo kuunganisha nguvu za taasisi hizo, masomo hayo yataweza kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni muendelezo wa kuunganisha Taasisi za Serikali na Chuo Kikuu cha Taifa. Kwa udogo wa nchi yetu, na mahitaji ya kuwa na Chuo Kikuu kimoja imara, na kuepukana na hali ambayo itaigharimu Serikali. Serikali yetu Tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuunganisha Taasisi zake kuwa Chuo kikuu kimoja hapa nchini kwetu.

USHIRIKISHWAJI WA WADAU

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iliunda Kamati ya wasomi kulifanyia utafiti wazo lake la kuunganisha taasisi zake na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Saleh Idrissa, Makamu Mkuu Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ilikuwa na wajumbe kadhaa kutoka Serikalini wakiwemo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Mtaalamu kutoka Wizara Kilimo, na Mtaalamu kutoka Taasisi ya Sayansi Baharini. Kamati hiyo ilitakiwa kufanya utafiti na kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kuziunganisha Taasisi za Serikali za Elimu ya Juu na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Taasisi ambazo Kamati ilizizingatia ni:

- Taasisi ya Uongozi wa Fedha (*ZIFA*),
- Taasisi ya Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*),
- Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya (*CHS*),
- Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (*KIST*),
- Taasisi ya Kizimbani ya Mafunzo ya Kilimo, na
- Skuli ya Uandishi wa Habari.

Kamati hiyo, ilitembelea na kuzungumza na watendaji wa taasisi zote hizo, na pia kuwasiliana na wadau mbali mbali wa elimu ya Juu nchini.

Baada ya kazi ya Kamati hiyo ambayo ilichukua karibu miaka miwili, iliwasilisha mapendekezo yake Serikalini. Kamati hiyo ilipendekeza kwamba Serikali itekeleze uunganishaji huu kwa awamu. Awamu ya kwanza ianze kwa kuunganisha taasisi 3 ambazo:

- Taasisi ya Uongozi wa Fedha (*ZIFA*),
- Taasisi ya Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*), na
- Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya (*CHS*).

Na vyuo vyengine viunganishwe katika awamu nyengine zijazo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha mapendekezo yake kwa Serikali, Kamati hiyo ilipewa kazi nyengine ya kuzungumza na taasisi husika, yaani Taasisi ya Utawala wa Fedha (*ZIFA*), Taasisi ya Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*), na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya (*CHS*), na kuzitaka zitoe mawazo yao juu ya uamuzi huo wa Serikali.

Kamati hiyo, iliwasilisha tena mawazo yake Serikalini juu ya mambo kadhaa ambayo yanahitaji kufanywa ili kuwezesha uunganishaji wa Vyuo hivyo bila ya kuathiri taaluma zinazotolewa katika vyuo hivyo, na kwa kuzingatia taratibu za kutoa taaluma katika ngazi za Vyuo Vikuu.

MATOKEO YA VIKAO VYA PAMOJA BAINA YA TAASISI ZOTE ZINAZOKUSUDIWA KUUNGANISHWA

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na vikao vya pamoja vilivyohusisha viongozi wa Taasisi zote zinazokusudiwa kuunganishwa na *SUZA* katika nyakati tofauti na bado vikao hivyo vinaendelea kufanyika katika kujadili namna bora ya kuratibu na kusimamia masuala ya *programmes* za kitaaluma, rasilimali watu na fedha na usimamizi wa mali zote za Chuo baada ya kuunganishwa kwa Taasisi hizo ili kuleta utekekezaji wa pamoja wa wazo hili la Serikali.

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na kukubaliwa na watendaji wa Taasisi husika katika vikao hivyo yamebainika kuwa tayari yamo katika mswada wa sheria ya mapendekezo, na kwa yale ambayo hayamo inapendekezwa kuingizwa ndani ya mswada huo ili kuuboresha zaidi na kurahisisha utekelezaji wa sheria hii baada ya kupitishwa na Baraza hili. Mapendekezo hayo mapya yamewasilishwa kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii na imekubalika kuzingatiwa katika mswada huu.

Hatua hii itasaidia kurahisisha suala hili baada ya Baraza lako kupitisha Mswada huu.

FAIDA ZA KUUNGANISHWA KWA BAADHI YA TAASISI ZA ELIMU YA JUU - (CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA ZANZIBAR, CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR, CHUO CHA TAALUMA ZA SAYANSI ZA AFYA) KATIKA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Mhe. Mwenyekiti, kupitishwa kwa mswada huu na hatimaye kuwa sheria, itakuwa ni hatua kubwa sana ya kukamilisha maagizo ya Serikali ya

kuunganisha taasisi tajwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *SUZA*. Suala hili likikamilika litakiwezesha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kutanuka na kuweza kutumia miundombinu na rasilimali watu za taasisi hizi kwa ufanisi zaidi.

Tayari tumetaja faida nyingi sana zitakazopatikana kufuatia kuunganishwa kwa Chuo cha Uongozi wa Fedha, Zanzibar, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Zanzibar na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya.

Kutokana na umuhimu wa hili wajumbe wa Baraza lako Tukufu, tunapenda kuzirejea baadhi ya faida muhimu za kuuunganishwa kwa Taasisi hizo kama ifuatavyo:

1. Kuimarisha ubora wa taaluma zitakazotolewa kwa kuzingatiwa muundo wa viwango *(quality assurance)* wa juu unaotumika na *SUZA*.

2. Kuunganisha tasisi hizi na *SUZA* kutapunguza uwezekano mkubwa wa taasisi kadhaa za Serikali kuwa na masomo yanayoingiliana, au masomo ambayo hayahitajiki na jamii lakini taasisi hizo zitalazimika kuanzisha ili kujipatia uhalali wa kuwa Vyuo Vikuu;

3. Masomo kadhaa yanayotolewa *SUZA* kuhamishwa kwenda kwenye vitivo husika:

Ikiwemo masomo yafuatayo yanayotolewa *SUZA* hivi sasa yatahamishwa kwenda katika kitengo kitachoundwa baada ya kuunganishwa Chuo cha Sayansi na Taaluma za Afya:

- *Doctor of Medicine*
- *BSc Environmental Health*

Wanafunzi wanaosoma masomo haya watapata fursa za kutumia miundombinu kama vile maabara iliopo kwenye Chuo hicho hivi sasa na kuleta ufanisi zaidi katika masomo hayo. Maabara hizo hazipo *SUZA*, wala hakuna tegemeo la *SUZA* kupata nyenzo katika mpango wake wa maendeleo wa hivi karibuni wa kujenga maabara hizo.

Vile vile masomo ya utalii yafuatayo yanayotolewa na *SUZA* yatapelekwa katika Taasisi ya Maendeleo ya Utalii, Zanzibar;

- *B.A in Tourism Management and Marketing;* na
- *Diploma of Tourism and Heritage Management.*

4. Masomo yanayosomeshwa *ZIFA*, *ZIToD* yanayohusiana na Taaluma ya Kompyuta (*Information Communication Technology)* yatapata walimu waliobobea zaidi kutoka Idara ya Sayansi za Kompyuta na TEHAMA iliopo *SUZA*;

5. Taasisi zote za Elimu ya Juu Zanzibar zina dhamira za kuwa vyuo vikuu hapo baadae. Kuunganisha taasisi hizi mapema kutawezesha kupunguza gharama za uendeshaji hapo baadae;

6. Kuunganisha kwa Taasisi hizi kutasaidia kuinua viwango na ubora wa masomo wa taasisi zinazounganishwa na *SUZA* hasa kwa vile *SUZA* ina mifumo imara na ubora zaidi ya kudahili wanafunzi na kuendesha mitihani;

7. Kuunganisha Taasisi hizi kutaisaidia Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kuelekeza nguvu zake za utoaji wa ruzuku na misaada mengine mengine mbali mbali inayopatikana katika kuendeleza Taasisi moja tu ya elimu ya juu ambayo ni (*SUZA*) itakayokuwa na uwezo mkubwa zaidi wa utoaji huduma ya elimu ya juu Zanzibar badala ya utaratibu uliopo hivi sasa wa Serikali kutoa ruzuku na misaada mengine muhimu kwa taasisi za elimu ya juu mbali mbali zilizotawanyika.

8. Kuweza kunufaika na misaada inayotolewa na nchi wahisani katika kujenga uwezo wa Chuo katika fani mbali mbali zinazotolewa na taasisi hizi kwa haraka zaidi.

9. Kuweza kunufaika na misaada inayotolewa na nchi wahisani katika kujenga uwezo wa Chuo katika fani mbali mbali zinazotolewa na Taasisi hizi kwa haraka zaidi.

10. Kuweka Elimu ya Juu chini ya wizara moja kutaongeza ufanisi wa Serikali wa kusimamia sekta hii na kuitumia vyema katika kutekeleza mikakati ya nchi kimaendeleo.

CHANGAMOTO

Mhe. Mwenyekiti, katika athari inayotarajiwa kuwa ni changamoto kwa Serikali yetu kufuatia kuunganishwa kwa Taasisi hizi ni kutokea ongezeko la bajeti kwa *SUZA* hasa kwa vile mishahara ya wafanyakazi wa vyuo hivi itabidi iongezwe ili ilingane na mishahara ya *SUZA* ambayo kimsingi ni

mikubwa ikilinganishwa na mishahara inayolipwa kwa watumishi wa Taasisi hizi tatu (3) zinazokusudiwa kuunganishwa na *SUZA*.

MAUDHUI YA MSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR NAM. 8 YA 1999 KAMA ILIVYOREKEBISHWA NA SHERIA NAM. 11 YA 2009 NA KUWEKA MASHARTI BORA PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umegawika katika sehemu kuu mbili zifuatazo:-

1. Sehemu ya Kwanza: Sehemu hii inahusu masharti ya awali, jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.

2. Sehemu ya Pili: Sehemu hii inahusu marekebisho mbali mbali yaliyofanywa kutoka katika sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999, ambayo yanahusu kuongeza wajumbe wa Baraza la Chuo ambao ni wajumbe kutoka katika Wizara ya Afya, Wizara ya Utalii, Chama cha Watu wenye Ulemavu na Mwakilishi kutoka katika Jumuiya ya Wafanyakazi wa kada ya Uendeshaji na Utaalamu ya Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha sehemu hii ya pili ya mswada imeainisha uanzishwaji na kazi za Bodi mbali mbali kama vile:-

Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu. Bodi hii itakuwa na jukumu la kulishauri Baraza la Chuo kuhusu masuala ya ajira na kusimamia rasilimali watu pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wote wa Chuo katika nyakati mbali mbali.

Pia, Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia mambo yote ya fedha za Chuo na kulishauri Baraza la Chuo kuhusu usimamizi mzima wa fedha za Chuo pamoja na kuweka kumbukumbu za fedha na kutoa ripoti mbali mbali za fedha.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya pili ya mswada pia imeainisha uanzishwaji wa bodi ya Ustawi wa Wanafunzi, ambayo itakuwa na jukumu la kulishauri Baraza la Chuo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa masuala ya ustawi na maslahi ya wanafunzi wa Chuo.

Pia, sehemu hii imeainisha ongezeko la Taasisi za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Utalii na Taasisi ya Masomo

yanayohusiana na Usafiri wa Baharini na Bandari *(Maritime)* kuwa ni miongoni mwa Taasisi za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Aidha, sehemu hii imeainisha uanzishwaji wa Kamati za Taaluma kwa kila Skuli na Taasisi ya Chuo ambazo kwa pamoja zitakuwa na kazi ya kuisadia Seneti ya Chuo katika kupitia *programmes* za mafunzo mbali mbali na kushauri namna bora ya kuimarisha masomo Chuoni.

Mhe. Mwenyekiti, pia, sehemu hii ya pili ya mswada imeainisha wakuu wa Idara na vituo mbali mbali vya Chuo katika kada za Taaluma na Uendeshaji. Wakuu hawa watateuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo baada ya kushauriana na Manaibu Wakuu wa Chuo na Wakuu wa Skuli na Taasisi za Chuo. Wakuu wa Idara hao watakuwa na jukumu la kuziendesha na kuzisimamia Idara hizo kwa mujibu wa taratibu za Chuo.

Na mwisho sehemu hii ya pili ya mswada inahusu kuwepo kwa muundo mpya wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ambao utahusisha taasisi zote hizo zilizounganishwa. Muundo huo mpya wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar utahusisha yafuatayo:-

i. Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya (*CHS*) imefutwa na sasa itatambulika kama ni Skuli (Kitivo) ya Tiba na Sayansi za Afya ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar;

ii. Taasisi ya Uongozi wa Fedha (*ZIFA*) imefutwa na sasa itatambulika kama ni Skuli (Kitivo) ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar; na

iii. Taasisi ya Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*) imefutwa na sasa itatambulika kama ni Taasisi ya Utalii ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

PENDEKEZO

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako linaombwa likubali mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 11 ya mwaka 2009 na kuweka masharti bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo ili uwe sheria kamili.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kuunganishwa kwa Taasisi ya Uongozi wa Fedha (*ZIFA*), Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya (*CHS*) na Taasisi ya Maendeleo ya

Utalii Zanzibar (*ZIToD*) katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ni suala la msingi na muhimu sana kwa ajili ya kukuza na kuharakisha maendeleo ya taaluma kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu wote wa Taifa hili kwa ujumla.

Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na mfumo wa kisheria utakaowezesha kufikia malengo ya serikali yaliyokusudiwa kwa ufanisi na utekelezaji mahiri wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili mswada ulio mbele yetu kwa lengo la kuimarisha na hatimaye kupitisha kuwa sheria kamili. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Hoja imetolewa na imeungwa mkono lakini kabla ya kuendelea, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wajumbe ambao wanataka kuchangia mswada huu walete majina yao na sasa hivi nampisha Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake mwingi ambao umetuwezesha kukutana hapa leo kufanya kazi waliotutuma wananchi ya kuwawakilisha na kuwaletea maendeleo. Aidha, nakushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu mswada uliopo mbele yetu. Kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya kamati juu ya mswada huu, Mhe. Mwenyekiti, naomba kueleza kwa ufupi umuhimu wa elimu na mwenendo wake mzima katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, umuhimu wa elimu katika nchi yetu umekuwa ukitiliwa mkazo mara zote na viongozi wetu wakuu wa kitaifa, tokea enzi za Mhe. Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, alipotandika dira vipi kwa muono wake nchi yetu ielekee kielimu na njia za kufikia lengo hilo ikiwemo kutoa elimu bila ya malipo. Waheshimiwa Marais waliofatia pia waliendelea pale alipoachia mwasisi wa Mapinduzi kwa kutoa miongozo yao mipya ikiwemo Sera ya elimu pamoja na kuweka mitaala mipya ya

kufundishia. Kubwa zaidi ni kujenga skuli zaidi za msingi, sekondari, vyuo na kuanzisha vyuo vikuu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inampongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Saba kwa kuanzisha mikakati mipya ya kuiendeleza sekta ya elimu. Lengo kuu ikiwa ni kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa ni bora, yenye manufaa na yenye kwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu hasa suala zima la kuwatayarisha vijana kuweza kujiajiri wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nchi nyingi zinazoendelea duniani kama Korea, Thailand, Veitnam, Malaysia na Singapore zimesisitiza na kuweka mfumo wa elimu unaofikiria siku zote kuleta vitu vipya (*innovative*), ubunifu (*creativity*) na uwezo wa kufanya utafiti (*research management*). Katika nchi hizi rasilimali fedha ni kitu kikubwa ambayo imewekezwa kwenye mafunzo ya ufundi *study* (*vocational training*) na mafunzo ya kitaalamu (*technical training*) na hata mafunzo ya vyuo vikuu (*university training*). Mhe. Mwenyekiti, utajiri wa nchi yoyote upo kwenye rasilimali watu wa nchi ile, hivyo, suala la kuwekeza kwenye elimu halina mjadala na linahitaji kuungwa mkono kwa nguvu na juhudi zote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea kwa ufupi umuhimu wa elimu ambao kila mmoja wetu humu anaufahamu, naomba sasa nije kwenye mswada wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kuletwa kwa mswada huu kipindi hiki kumeibua mawazo na hisia tofauti za wananchi pamoja na wasi wasi kwa baadhi ya makundi na jumuiya zinazohusiana na elimu nchini. Kamati yangu imepata fursa ya kukutana na wananchi kupitia jumuiya zao pamoja na wananchi wengine waliowasilisha maoni yao kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imetumia vyema fursa ya kukutana na wananchi hao ambao walisaidia kamati kuchambua kipengele kimoja baada ya kingine cha mswada na kuibua hoja na maelezo ya kina ambayo kamati imeyapokea, imeyachambua na kuyafanyiakazi. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba niwapongeze wadau na wahusika wengine mbali mbali ambao walipata fursa ya kukutana na kamati na wale ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi. Kamati inaendelea kutoa wito kwa wananchi waendelee kutumia haki yao ya kutoa maoni pale ambapo Baraza lao linapojadili mambo mbali mbali yanayohusu maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Kamati inaishukuru sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa kuwaandalia kamati ziara ya kimafunzo katika taasisi ya *NACTE* (Baraza la Elimu ya Ufundi) na *TCU* (Kamisheni ya Vyuo Vikuu) kule Dar-es-Salaam Tanzania Bara. Kwa kweli safari ile imetupa mafunzo makubwa na imetufungua macho juu ya utaratibu mzima vipi vyuo vya ufundi vinavyosimamiwa na *NACTE* na pia vyuo vikuu vinavyosimamiwa na *TCU*.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kupitia mswada huu haikuwa rahisi hata kidogo, kamati yangu haikuwa na ufahamu wa ndani na wa kina kuhusu mswada huu, tulihitaji sana maoni ya wananchi na taaluma kutoka wizara husika, kusema kweli wananchi waliutendea haki wito wa kamati kuja kutoa maoni, natumia fursa hii kuwashukuru tena na kusema ahsante sana. (*Makofi*)

Pia, nawashukuru wizara hasa Mhe. Waziri wa Elimu na timu yake pamoja na uongozi wa Chuo Kikuu cha *SUZA* kwa kutupa darasa kubwa ya kutuelimisha mpaka tukaufahamu undani wa mswada wenyewe.
Mhe. Mwenyekiti, lazima pia nikiri kuwa mshikamano na umakini wa Wajumbe wa Kamati hii umechangia kwa kiasi kikubwa kupitia mswada huu kuanzia ngazi ya maoni ya wananchi mpaka kukutana na wizara, hatimae kutoa mapendekezo mbali mbali kwa njia ya kuimarisha vifungu vya mswada huu ili marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika mswada huu yawe yenye tija na maslahi katika maendeleo ya elimu ya nchi yetu. Kwa hakika kamati imefanya kazi kubwa ya kutoa hoja zenye mashiko kwa wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba uniruhusu niwataje majina Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Mjumbe
6. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
7. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe na
8. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
9. Ndg. Aziza Waziri Kheri - Katibu
10. Ndg. Khamis Hamadi Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwa niaba ya kamati kuwashukuru Makatibu wetu kwa kazi kubwa wanayofanya kuratibu kazi mbali mbali za kamati yetu kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza. Lakini kwa mswada

huu naomba niwashukuru sana wanasheria kutoka Afisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, najua Mwanasheria Mkuu kwa vile na yeye msomi angependa sana aje kwenye mswada huu lakini alibanwa kidogo na mswada wa mafuta na gesi. Tunakushukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu na nikuhakikishie kwamba uliwakilishwa vyema.

MADHUMUNI YA MSWADA

Mhe. Mwenyekiti, sote tunatambuwa kwamba nchi yetu imeendelea kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya elimu ya juu hasa baada ya Kupitisha Sheria ya Kuanzisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) mwaka 1999. Tokea Kuanzishwa kwa chuo hicho mafaniko makubwa yamepatikana katika maendeleo ya sekta ya elimu nchini. Vijana wengi wemepata fursa pana zaidi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu na mafunzo ya kitaalamu ambapo idadi kubwa ya wataalamu imeongezeka katika fani mbali mbali ambazo hapo awali zilikuwa zikipatikana nje ya Zanzibar katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada ya mwanzo na za juu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu hivi sasa imekuwa na taasisi kadhaa za serikali ambazo zinatoa mafunzo katika fani mbali mbali za utaalamu na taaluma. Taasisi hizi zimekuwa zinafanyakazi nzuri ya kuzalisha wataalamu, pia, zimekuwa ni msaada mkubwa kuwawezesha vijana wetu kufikia ndoto zao za kusomea mambo mali mbali waliyochagua kufanya katika maisha yao na kama nchi zimesaidia kuwa na taasisi zetu wenyewe za kuzalisha wataalamu wetu
Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja kuunga mkono juhudi za taasisi hizo kwa kuziweka katika utaratibu wa kisheria utakaoziwezesha kuwa katika muundo mpya mmoja ndani ya Chuo Kikuu kimoja kitakachokuwa imara, chenye ubora na ufanisi katika matumizi ya rasilimali fedha za nchi.

MAONI YA WANANCHI KATIKA MSWADA

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza hapo awali, kamati kabla ya kuupitia mswada huu, imepata nafasi ya kuwasikiliza watu mbali mbali kutoka vyuo vyenyewe na taasisi binafsi zenye mahusiano ya ukaribu na sekta ya elimu. Taasisi hizo zimeonesha wasi wasi kuhusu mswada huu hasa kwenye madhumuni ya mswada huu ya kuwa na sheria itakayoruhusu taasisi nyengine za elimu za serikali kuunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Taasisi hizi zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa Mhe. Mwenyekiti, kutoa elimu ya ufundi kwa vijana wetu wengi hapa Zanzibar katika nyanja za afya, uongozi wa fedha na utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema; 'wasi wasi ndio akili'. Kamati yangu kwa ujumla imesikiliza hoja za wananchi na kupima mambo mbali mbali waliyoeleza ambayo kwa maoni yao wanahisi yatazamwe vizuri kabla ya kuchukua hatua ya kuunganisha taasisi zilizokusudiwa na Chuo Kikuu cha *SUZA*. Ushirikishwaji wa wanataaluma wengine na serikali za wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuchambua maoni hayo ya wananchi, kamati imebaini kuwa yapo mambo ya msingi yalitakiwa kufanyika katika hatua za awali kabisa kabla ya mswada huu haujaletwa ili wahusika wote wa sekta ya elimu wawe na ufahamu wa dhamira nzuri ya serikali ya kuunganisha vyuo hivi kuwa chuo kikuu kimoja. Miongoni mwa mambo hayo ya msingi ni ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi za chini, mfano Serikali za Wanafunzi wa vyuo au taasisi zinazounganishwa, wemeiambia kamati kuwa hawakupata kuulizwa au kufahamishwa mpango wa kuunganisha vyuo hivyo. Kwa hivyo, wameshindwa kutoa maoni yao. Halikadhalika, ukiacha uongozi wa Chuo Kikuu cha *SUZA*, walimu na wanafunzi wengine hawakupata kabisa nafasi ya kutoa maoni yao. Ile kamati ya serikali ambayo Mhe. Waziri ameisema zaidi imekwenda kwenye uongozi wa vyuo vilivyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa kamati ya wataalamu imeundwa kufanya utafiti wa mpango huu, lakini kamati imejuulishwa kuwa kamati hiyo ya utafiti ilishirikisha wasomi na wataalamu katika ngazi za juu tu za elimu. Jambo ambalo ni jema na zuri, lakini hata hivyo suala la elimu linahusu wahusika katika makundi mengi kama wazazi, wanafunzi, walimu, wahadhiri, asasi za kiraia zinazohusika na elimu na kadhalika, ambao nao walipaswa kushirikishwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ushirikishwaji mdogo wa makundi hayo umesababisha mswada huu kupokelewa kwa hisia tofauti, kwani sehemu kubwa ya wananchi ambao wameonesha hofu kubwa kuwa hatua inayotaka kufanyika ya kuunganishwa vyuo au taasisi hizo na *SUZA* ya haraka na haijafanyiwa utafiti wa kutosha wa kukabili changamoto mbali mbali kama vile ukusanyaji wa rasilimali za kutosha kuendesha chuo kimoja chenye taasisi nyingi. Baya zaidi kamati imebaini kwamba hata hizo taasisi zinazotaka kuunganishwa na *SUZA* hawakupokea vyema shauri hili kwa hofu kubwa ya kwamba wanahisi watamezwa.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi, haya waheshimiwa zaidi ni maoni tuliyopata kutoka kwa wananchi waliokuja kwenye kamati.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi pia wameonesha wasiwasi katika suala la uendeshaji wenye tija uendelezaji wa viwango vya ubora uliokwishapatikana katika baadhi ya taaisisi hizo. Baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikijiendesha kwa mafanikio makubwa mfano Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka na Chuo cha Afya Mbweni ambavyo vimekuwa na mafanikio makubwa katika viwango vya ufundishaji na uwezo wa kujiendesha pamoja na kutoa wataalamu wengi katika ngazi ya cheti na diploma.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wameonesha wasi wasi kama hali hiyo itaendelea kudumishwa kwa ufanisi endapo vitaunganishwa na Chuo Kikuu cha *SUZA*, na kamati imeona kuwa ni vyema suala hili likatolewa maelezo ya kina na Mhe. Waziri, kwa kuwandoa hofu wananchi. Vyuo vikuu kazi yao kubwa ni kutoa wataalamu, pia wanataaluma chini ya usimamizi wa *TCU*, ambapo taasisi zinazounganishwa zinatoa elimu ya ufundi na kuwatayarisha wataalamu katika ngazi ya cheti na stashahada chini ya usimamizi wa *NACTE*.

Katika ziara yetu kwenye Taasisi za *NACTE* na *TCU*, kamati imejuulishwa kwamba zoezi ambalo serikali inalotaka kufanya kisheria na kiutaratibu halina tatizo. Mfano mzuri upo Rwanda katika ukanda wetu wa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wafanyakazi wa taasisi hizo zitakazounganishwa na *SUZA* limejitokeza ambapo kamati pia imeona nalo lielezwe kwa uwazi, mpango gani utafanyika ambao hautaathiri haki na maslahi ya wafanyakazi hao pale ambapo mageuzi ya kimfumo yatakapofanyika. Kamati imezingatia sana hoja hii ya wananchi kwa kuwa masuala ya haki na maslahi ya wafanyakazi yamekuwa na changamoto za kipekee kwa vile yanahusu maisha ya watu katika kujikimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika uzoefu wa mpango kama huu ambao umeshawahi kufanyika hapo awali kama alivyoeleza Mhe. Waziri katika Taasisi kama vile TAKILUKI na Chuo cha Elimu cha N'kuruma kuunganishwa na *SUZA*, hoja mbali mbali zimezuka kama kweli hatua ile imesaidia kuimarisha na kuleta ufanisi uliokuwapo hapo awali kabla ya taasisi hizo hazijaunganishwa na *SUZA*. Wapo wananchi ambao wanahisi kuwa hatua ya kuunganisha TAKILUKI na N'KURUMA haikufikia malengo yaliyokusudiwa kwa vile hadhi ya taasisi hizo imeshuka. Hivyo, ni vyema ufafanuzi mpana na wa kina ukatolewa na Mhe. Waziri, kama hatua hii ya sasa imezingatia vipi changamoto za wakati ule kwa TAKILUKI na N'KURUMA zisijirudie tena hivi sasa kwa vyuo vyengine na taasisi zilizoanzishwa hapo awali na ambazo zinataka kuunganishwa na chuo kikuu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia imezingatia hoja ya wananchi ya matumzi ya rasiliamali hasa fedha za taasisi hizi endao zitaunganishwa na Chuo Kikuu cha *SUZA*. Kamati imefahamishwa kwamba moja ya sababu za mafanikio makubwa ya kiundeshaji ya vyuo kama Chuo cha Afya Mbweni na Chuo cha Uongozi wa Fedha cha Chwakwa ni kujitegemea vyenyewe kifedha kutokana na ada na michango ya huduma mbali mbali kutoka kwa wanafunzi. Vyuo hivi vimekuwa vikijiendesha vyenyewe huku utegemezi wa serikali ukiwepo lakini kwa kiwango cha wastani. Wananchi walisisitiza kuwa endapo mpango wa kuviunganisha vyuo hivi na *SUZA* utafanyika, basi lazima vihakikishiwe uwezo wa kujiendesha kifedha kama ilivyo hivi sasa unabaki, ili ufanisi wa utoaji huduma uendelee kama ulivyo. Kamati inapendekeza skuli hizo ziwe na kasma, yaani *sub-votes* zao maalumu katika masuala ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona umuhimu wa hoja hii kuwa na mpango na majibu ya wazi yanayotekelezeka. Hata hivyo, nieleze kuwa wakati kamati ilipokutana na wizara bado hakukuwa na majibu muafaka juu ya mpango wa usimamizi wa rasilimali fedha baina ya vyuo hivi na *SUZA* utakuwaje, kamati ilielezwa kuwa mpango huo unaendelea kutengenezwa na tayari wataalamu wapo Tanzania Bara kwenda kufanya utafiti na kujifunza.

Kamati pia imezingatia hoja ya wananchi kuwa mpango wa kuunganisha vyuo vyenye kutoa utaalamu uwende sambasamba na kuviimarisha vyuo vya ngazi za chini vinavyotoa elimu ya ufundi (*polytechnics*), ambavyo vinasaidia kudahili wanafunzi wa viwango vya chini ambao hawataweza kupata nafasi ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Taifa. Hata hivyo, baada ya kuendelezwa wanafunzi katika ngazi ya vyeti na stashahada wanawea hata kuchukua mafunzo ya shahada ya mwanzo na kuendelea katika shahada nyengine. Mifano hii ipo katika nchi za Korea, Vietnam, Singapore, Thailand na Northern Ireland kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2008.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla wananchi waliowasilisha maoni yao kwenye Kamati walikuwa na mawazo kuwa Mswada huu ungeweza kuletwa baada ya kutandika au kutayarisha utaratibu mzima wa uendeshaji. Si vyema mipango ya utendaji ikatayarishwa baada ya sheria zilizopo za vyuo hivyo kufutwa na kupelekea kuwa na pengo la mwenendo wa utendaji katika vyuo hivi. Kamati imejuilishwa kwamba hivi sasa Baraza la Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka limemaliza muda wake tokea mwezi wa Agosti na hivi sasa baadhi ya mambo yao ya kitendaji yamekwama.

Wananchi pia wameshauri kwamba, Mswada huu unaweza kuletwa mpaka pale ambapo yatakapokamilika mambo muhimu waliyoainisha ili kuepusha athari

kama zile zilizojitokeza kwa kuunganishwa TAKILUKI na Chuo cha N'kuruma ndani ya SUZA.

MAONI YA KAMATI KWENYE MSWADA

Mhe. Mwenyekti, Kamati yangu imehisi ni vyema iwasilishe hoja hizi za wananchi mbele ya Baraza hili na Waheshimiwa Wajumbe, wazisikie ili wizara itoe majibu ya ufafanuzi wa kina. Kwa hivyo, kamati yangu inashauri wizara kutoa ufafanuzi wa kina wa hoja hizo na zile nyengine ambazo Waheshimiwa Wawakilishi, wataziwasilisha kwa niaba ya wananchi wao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imewasilisha maoni hayo ya wananchi kwa wizara na maelezo ya kina tumepatiwa. Hata hivyo, tunasisitiza mambo muhimu ambayo bado yanahitaji kufanyiwa kazi ili kuondoa wasi wasi wa kiutendaji. Kamati yangu inaiomba wizara kuja na mpango unaotekelezeka wa mgawanyo wa kifedha ili kuhakikisha kuwa taasisi zinazounganishwa na *SUZA* zitaweza kujiendesha kama zilivyo hivi sasa au hata zaidi ya hapa.

Lengo la mswada huu wa kuunganisha taasisi zilizotajwa na Chuo Kikuu cha *SUZA* ni kuleta kasi ya ufanisi katika kuzalisha wataalamu katika ngazi zote kwa kuzingatia changamoto za rasilimali fedha. Kwa kuzingatia si nia ya mswada huu kusitisha mafanikio yaliyopatikana awali katika vyuo vilivyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, mpango huu wa kuunganisha taasisi hizi utahusu mageuzi mbali mbali ya kitaasisi kama vile uendeshaji, ufundishaji na utawala. Kamati yangu inapendekeza kuwapo mpango wa mpito wa kuelekea kuunda upya vyombo mbali mbali vya uendeshaji vilivyoainishwa katika marekebisho ya sheria, muda mfupi baada ya Mswada huu kusainiwa kuwa sheria. Nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri, kwamba mpango huu wa uanzishwaji utakwenda kwa awamu hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inashauri pia wizara itoe maelezo kwa wananchi kuhusu hatua hii inayotaka kufanyika itawagusa vipi wahusika mbali mbali wa vyuo na taasisi zinazotaka kuunganishwa hususani wanafunzi wanaodahaliwa hivi sasa, wanafunzi wanaosubiri kuhitimu na wale ambao mambo mbali yanayohusu maendeleo yao katika vyuo hivyo kwa hivi sasa endapo Mswada huu utakuwa sheria kwa vile sheria zinatawala uendeshaji wa vyuo vyao vitakuwa vimefutwa baada ya sheria kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imepitia vifungu vya mswada huu wa marekebisho na kupendekeza marekebisho mbali mbali ambayo tumeyaweka katika waraka ambao Waheshimiwa Wajumbe, tayari wameshapatiwa. Tunawaomba sana waraka huo wa marekebisho waupitie vifungu vya mswada kifungu kwa kifungu na uwe ni sehemu ya maoni ya kamati na yaingia kwenye *Hansard.*

Kwa kuhitimisha naomba kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi kubwa waliyofanya katika kuupitia Mswda huu, walikuwa wakakamavu, wenye hoja makini na pia kujifunza kwa muda wote, lengo lilikuwa kuhakikisha kwamba nia nzuri ya serikali ya kuja na mswada huu inatekelezwa kwa ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, muda wote wamekuwa wamekuwa wakishirikiana na Kamati hii katika kazi zake za kusimamia uendeshaji wa shughuli za serikali katika Sekta hii muhimu ya elimu. Tunampongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara, naomba tuendelee kushirikiana na kuwa kitu kimoja ili tufanikishe maendeleo ya elimu ya nchi yetu. Suala muhimu sana kwetu lilikuwa kujifunza na kuelimishwa mpaka tukafahamu mambo ya msingi yaliyokusudiwa katika mambo haya ya kitaaluma yaliyotajwa kwenye mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa utulivu wao na umakini wakati wote nikiwasilisha maoni haya ya kamati. Nawaomba Waheshimiwa Wawakishi wote, tuujadili Mswada huu kwa hoja, tutake ufafanuzi pale ambapo hatujafamu, tushauri, tupendekeze, tufanye marekebesho pale tunapoona hapajakaa vizuri na tuhakikishe tunatoa hoja za kusaidia kujenga zaidi ili tutoke hapa na kitu kizuri kwa maslahi ya wananchi na nchi yetu.

Mhe.Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nakushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni haya ya Kamati na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa hotuba yako na michango ambayo umeitoa. Niwapongeze Mwenyekiti pamoja na kamati yake kwa kufanya kazi nzuri. Lakini pia Waheshimiwa Wajumbe, bado naendelea kusisitiza kuwa wachangiaji walete majina yao na sasa hivi tutakuwa na wachangiaji wawili wa mwanzo kuchangia mswada huu, kama

muda utaturuhusu basi ataongezeka na mwengine, lakini kwanza namuomba Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni, aanze kwa kuchangia, akimaliza Mhe. Rashid Makame, Mhe. Ali Suleiman Ali ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo ya kumfunga paka kengele katika kuuchangia mswada huu muhimu wa marekebisho ya sheria inayokihusu Chuo chetu cha Taifa *SUZA*. Lakini nichukue fursa hii kutoa shukurani sana na pongezi kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa uwasilishaji wake mzuri na ripoti ambayo imesheheni kila kitu, ambayo inaweza ikatufanya kukubaliana na kuupitisha mswada huu.

Vile vile, niishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii chini ya uongozi wa Mwenyekiti makini Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini, kwa ripoti yao nzuri sana, wamekwenda kwa kina, wameonesha wasiwasi, wameonesha mapendekezo na kila kitu ambacho kingesaidia serikali hii katika suala zima la maendeleo ya kielimu katika vyuo vyetu. Naishukuru sana kamati kwa kazi yake. (*Makofi*)

Laitani kama sikupata hii nafasi basi pia isingekuwa hasara kutokana na ripoti nzuri ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Lakini kwa sababu nimeipata hii nafasi na mimi ni miongoni mwa wadau wa elimu, basi nichukue fursa hii sasa kuweza na mimi kutoa michango na maoni yangu katika mswada huu ambao uko mbele yetu. Ni ukweli usiofichika kwamba Zanzibar inasifika sana katika kuandaa miswada hata kimataifa, tatizo letu kubwa sana ni utekelezaji wa hizi sheri baada ya kupitishwa kwa miswada hiyo. Ningependa nichukue fursa hii kuiomba serikali yetu tukufu suala la kupitisha mswada hapa halina tatizo, suala ni utekelezaji wa sheria tunazozitunga. Tuwe makini na tuwe wa dhati katika yale ambayo tunayakusudia.

Ripoti au taarifa aliyotupa Mhe. Waziri, imepangika vizuri sana, lakini vile vile tukiitizama kwa upande mwengine wa Ripoti ya Kamati kuna mambo ambayo yanakinzana. Sasa hapa wananchi tutakuwa tunawachanganya, suala zima la ushirikishwaji linakanganya kati ya ripoti ya waziri na ripoti ya kamati, inaonekana kwamba ushirikishwaji wa wananchi katika jamii juu ya masuala yanayowahusu unakuwa ni mdogo. Hili tukubali hata katika mswada uliopita wa mafuta tulisema hivyo, ripoti za mawaziri zinakuwa nzuri lakini ukienda huko chini kwa wananchi hawana taarifa, vyuo vyenyewe havikushirikishwa ipasavyo, wameshirikishwa baadhi tu, huwezi ukapata maoni ambayo yangesaidia katika kuifanya elimu yetu iwe bora.

Mhe. Mwenyekiti, lengo ni zuri, lengo la kuwa na mswada huu na baadae kuviunganisha taasisi na Vyuo vya Elimu ya Juu kwenye Chuo Kikuu cha *SUZA* ni nzuri sana na faida ambazo zimeelezwa zinaingia akilini, lakini wakati mwingi hatutazami suala zima la ubora wa elimu, suala la ubora tunaliweka pembeni kidogo. Wenzetu kamati wamezungumzia athari za kuunganisha Taasisi ya Kiswahili na Lunga za Kigeni kuwa chini ya *SUZA*, wamezungumzia athari baada ya kuunganisha Chuo cha Ualimu N'krumah kuingiza *SUZA*, kinachojitokeza hapa tunaangalia *quantity* na sio *quality* na huu ni wakati pamoja na lengo zuri la kuwa na ubora, lakini tuangalie *quality* ya vijana wetu ambao tutawatoa katika vyuo hivi. Huu ni wakati wa ushindani wa soko, inawezekana kijana au mhitimu katoka ana cheti chenye nembo ya *SUZA* lakini hawezi akaingia katika ushindani. Hili lazima tulitazame, mimi nina challenge, mwanafunzi aliyepata stashahada katika Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni hapo nyuma na ukimuangalia mwanafunzu aliyepata stashahada hiyo hiyo, basi utamkuta mwanafunzi aliyepata stashahada ya enzi hizo ana ubora kuliko mwanafunzi wa hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi vile vile wa mwanafunzi aliyepata stashahada kwa wakati ilipokuwa N'krumah na mwanafunzi anayepata stashahada ambapo N'krumah iko chini ya *SUZA* ni vitu viwili tofauti, ukiwaweka hapa basi utaona kwamba wa enzi hizo *is very competent* kuliko wa hivi sasa. Sasa hili lazima tulitazame *weakness* zetu ziko wapi katika kuunganisha hili. (*Makofi*)

Hivi sasa tumeanzisha stashahada ya uongozi wa elimu, lakini stashahada ya uongozi wa elimu ilikuwepo N'krumah na kama utamchukua mwanafunzi wa *bench* ya mwanzo au ya pili wa stashahada hii ya uongozi wa elimu wa N'krumah, basi ana ubora zaidi kuliko mwanafunzi ambaye ametoka *SUZA* kwa wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa imeanzishwa *course* ya stashahada ya michezo, tusubiri watoke lakini nina imani mwanafunzi aliyetoka kwenye stashahada ya elimu ya michezo ya N'krumah kama atawekwa na mwanafunzi wa stashahada inayoanzishwa hivi sasa ni vitu viwili tofauti. Hivi sasa mwanafunzi huyu wa stashahada ya michezo anasoma Tunguu viwanja viko mjini, hapa bado hatujawa tayari, huo ni usumbufu kwa vijana wetu. Lakini vile vile ni usumbufu kwa wakufunzi, huwezi ukawa wewe unafundisha *campus* ya *SUZA*, *campus* ya N'krumah na *campus* ya Tunguu; mwanafunzi mara yuko N'krumah, mara yuko Tunguu, wanafunzi wetu ni masikini, hali hii kama hatujajipanga tutawasumbua sana wanafunzi na upatikanaji wa elimu ambayo tunatarajia iwe bora basi itakuwa ni ndoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane sana na Ripoti ya Kamati na ningeiomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali isidharau hata kidogo kuweza kuitazama ripoti hiyo kwa kina na kuweza kuifanyia kazi ili tuweze kupata ubora wa mswada huu ambao tunaupitisha.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 14 katika mswada huu, kuna aya ya pili inayosema kwamba:

"Aidha, Mswada huu unakusudia kuweka utaratibu wa kisheria utakaoiwezesha Zanzibar kuwa na Chuo Kikuu kimoja kitakachokuwa imara na chenye ubora na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za nchi".

Ningependa kutoa wazo katika *statement* hii kwamba, utaratibu wa kisheria utakaoiwezesha Zanzibar kuwa na Chuo Kikuu kimoja. Zanzibar itaendelea kuwa na Vyuo Vikuu zaidi ya kimoja kama Zanzibar, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawezekana ikawa na Chuo Kikuu kimoja. Kwa sababu tunavyo vyuo binafsi ambavyo hatuwezi kuviunganisha na *SUZA*. Kwa hiyo, hapa parekebishwe ili ionekane kwamba, utakaoiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na Chuo Kikuu kimoja na sio Zanzibar. Kwa sababu hivi sasa viko vyuo zaidi ya kimoja na vitaendelea kuwepo. Hapo napenda kutoa marekebisho katika hili.

Lakini ninapata mkanganyiko kuna wakati Mhe. Waziri wa Elimu katika hoja mbali mbali zinazohusiana na kuviunganisha vyuo hivi aliwahi kusema kwamba pamoja na kuviunganisha hivi vyuo na Taasisi ya Elimu ya Juu na SUZA, lakini vikija vikipata nguvu vinaweza zikaachiwa.

Sasa ripoti yake inaendana kinyume na hili, sioni kama kutakuwa na nafasi ya vyuo hivi vikija kupata nguvu vikaachiwa. Naomba akija afute hiyo kauli kwa sababu itatuweka pabaya. Hii inaonekana tukishaunganisha tumeunganisha, tuwe na Chuo Kikuu kimoja chenye nguvu na hakutokuwa na sababu nyengine yoyote ambayo itakuja kuruhusu vyuo hivi kujitenga.

Lakini mifano ambayo imetolewa vile vile ni mifano ya nchi mbili hizi za kigeni ambazo zimeendelea sana; kuna Urusi na Finland ,nchi ambayo inalingana lingana ni Ruwanda. Tusilinganishe baada ya mambo na nchi ambazo zimeendelea zaidi kwa sababu wana nyenzo kubwa za rasilimali watu na nyenzi kubwa za rasilimali fedha. Sasa sisi tutizame na uchumi wetu.

Ni ukweli usiofichika kwamba hapa tunataka kuunda gorofa na gorofa lenyewe basi zege yake au jamvi lake ni *SUZA*. Lakini tuitizame hiyo *SUZA* hilo jamvi

ambalo limetandikwa linaweza likahimili kuweka gorofa jengine juu. Hili ni lazima tulitizame, tutizame majengo ya *SUZA* toka *SUZA* iundwe, suala sio kurithi majengo tu ya taasisi hizi ila suala ni kurithi mambo mengi ya uendeshaji. Kwa hiyo, naendelea tu kutoa tahadhari katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 3, kifungu cha 16(3)(e), kinasem;

"Kuzingatia na kutoa mapendekezo..." .Hapa naomba iingie neno "ya", yaani isomeke; "Kuzingatia na kutoa mapendekezo ya upandishaji vyeo..." ikiendelea; "...wafanyakazi wanataaluma na uendeshaji au..." iwe "...wa kada wa kata nyengine" iingie nano "wa".

Lakini vile vile nishauri kwenye ukurasa wa 5 katika suala zima la Bodi ya Ustawi wa wanafunzi. Tutakuwa na taasisi hizi ambazo tunaziunganisha; tuna taasisi iko Maruhubi, kuna Taasisi iko Mbweni, kuna Taasisi iko *SUZA* yenyewe na N'kurumah na kuna Taasisi iko Tunguu.

Hii Bodi ya Ustawishaji wa wanafunzi mimi nahisi kwamba ifanyiwe marekebisho kidogo katika muundo wa hao Wajumbe wake. Ningependekeza kuwe na Wawakilishi wa hizi Taasisi ambazo zitaunganishwa; kuwe na Uwakilishi wa wanafunzi wa ile ambayo tutaiita kama ni Chuo cha Maendeleo ya Utalii, lakini tuwe na Mwakilishi wa ile Taasisi ya Afya na hizi nyengine ambazo zipo. Kwa sababu bila ya kuwa na Uwakilishi huo basi nafikiri Bodi hii haiwezi kutenda haki, inawezekana tukaja tukajikuta tuna *samples* za wanafunzi waliopo tu katika *campus* ile ya Tunguu peke yake bila kuzishirikisha nyengine. Kwa hiyo, inawezekana haki isije kutendeka kuhusiana na ustawi huo wa wanafunzi.

Lakini vile vile nikija katika ukurasa wa 7 katika kifungu cha 14(b), kinasema kwamba:

> "Atakuwa na uzoefu angalau wa miaka mitatu ya kazi katika Chuo kinachotambulika"

Ningependa isimwe "...Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar" Hicho kifungu kitaje hivyo. Lakini ukurasa wa 8 katika kifungu cha 15(2)(a) kimetaja sifa hapa za Mkuu Msaidizi wa Skuli. Kifungu (a), kinasema:-

"Atakuwa angalau na Shahada ya Uzamili"

Lakini ukirudi katika sifa ya Mkuu imesema; "atakuwa na Shahada ya Uzamili".

Lakini hii inasema 'angalau' sasa sijui nafasi iliyokuwa kubwa ni ipi, kwa sababu kama ni angalau basi ingekuwa katika sifa za Mkuu na isingekuwa katika sifa za msaidizi. Kwa hiyo, neno 'angalau' hapo aidha iletwe katika sifa za Mkuu na isiwepo katika sifa za msaidizi kwa sababu Mkuu huyu anatakiwa ikiwezekana basi awe juu zaidi kwa sifa hiyo kuliko huyu msaidizi.

Lakini katika kipengele cha 15 (3), suala zima la huyu Msaidizi wa Skuli, hapa nina suala kwa Waziri aneehusika au kwa Mwanasheria, kwa nini kawekewa ukomo wakati Mkuu wa Skuli hakuwekewa mkomo. Hapa inasema kwamba;

"Msaidizi huyu atashika wadhifa huo kwa kipindi cha miaka 3 kutoka tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu".

Hapa kama kawekewa mkomo lakini yule mkuu hakuwekewa mkomo.

Lakini nikija kifungu cha 16, namba (2) kuna neno hapo mstari wa kwanza "Idara ya Vituo" ningeshauri isomeke "Vituo vya Taaluma" isiwachwe wazi napendekeza ikikubalika. Lakini tukija katika ukurasa wa 9 pana kifungu cha (b) wanasema; "watawakilisha idara zao katika Kamati za Chuo" ningependa hilo neno lisomeweka "Kamati za vyuo" na sio Kamati za Chuo. Kutokana na hata ile ya Kiengereza ambayo inasema; "*University committees"*.

Lakini kifungu cha (e) ambacho kinasema;

"Wataweka kumbukumbu sahihi za idara zao na zinazoenda na wakati".

Ningependa nitoe marekebisho hapa isomeke hivi:

"Wataweka kumbukumbu sahihi na zinazoendana na wakati katika idara zao".

Hata ukiangalia ile *English vision* basi inaweza ikakaa hivyo.
Lakini nikija katika kifungu cha 18(1), kinasema;

"Kutakuwa na Kitengo au Vitengo".

Katika *version* ya Kiengereza nafikiri kilichotajwa ni Vitengo na sio kitengo au vitengo. Kwa hiyo, lichukuliwe moja hapo ambalo litakuwa limesomeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika mchango wangu katika suala zima la Jumuiya ya Wafanyakazi katika ukurasa wa 10, kifungu cha 20, kinasema;

"Jumuiya ya Wafanyakazi wa Uendeshaji wa wataalamu".

Mhe. Mwenyekiti, hizi skuli ambazo zinaingizwa nahisi katika kipengele hichi zinaweza zikakosa nafasi. Kwa hiyo, katika kutazama hizi jumuiya kwanza suala linabaki skuli hizi ni nyingi. Hizi jumuiya zitakuwa kila skuli na vipi zitaweza kujiendesha. Sasa ningependa kwamba muundo huu wa Jumuiya utizame na hizi skuli ambazo tunaziunganisha.

Mwisho, nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hiyo na mimi nasema tu kwamba naukubali mswada huu. Lakini yale ambayo tunahisi yana mapungufu katika mswada huu basi wizara kwa kushirikiana na Mwanasheria basi waweze kukaa kitako na kuweza kuona kwamba mswada huu unatekelezeka vizuri na sio uzuri wa maandishi katika karatasi. Ahsnte sana. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote pamoja na kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri waliofanya na kutuletea hapa katika Baraza lako tukufu mswada huu ili tuuchangie kuhusiana na mambo ambayo yanahusu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa asilimia kubwa sana Mhe. Rashid Makame Shamsi Mwakilishi wa jimbo la Magomeni, kayachukuwa yangu na mimi mara nyingi hutaka ninapochangia niwahi mwanzo, vyenginevyo, huwa nafilisiwa yale ninayoyataka yatakuwa yanapita njia.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, nitapata machache ambayo yatakuwa kama ni masuala au angalizo la mbele tunakokwenda juu ya mswada huu na hatima ya vijana wetu wanaosoma katika vyuo vyetu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Elimu ya Chuo Kikuu ni sifa moja wapo, lakini elimu hiyo unaweza kuipata Chuo Kikuu likawa jina tu lakini sifa halisia ukaikosa kutokana na mazingira ambayo tunayajua. Lakini kwa kuwa umetoka Chuo

Kikuu utahisabika unatoka Chuo Kikuu na mambo mengine yanafata ili kuhakikisha hicho Chuo Kikuu chako umefanya nini na sifa zako ziko vipi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vyuo vyetu ambavyo vitaunganishwa katika Chuo Kikuu *SUZA*. Mimi niseme tu kwamba hilo wazo si baya lakini pia liangaliwe kwa umakini zaidi tunakokwenda. Chuo Kikuu maana yake ni Chuo Kikuu na kuna vyuo hivi vidogo vidogo au Taasisi za Vyuo hizi ni Vyuo ambavyo vinajitegemea na vinaweza kuwa bora zaidi kuliko huyu anaetoka Chuo Kikuu kama atasimamiwa vizuri na atapata zile stahili kwa mwalimu wanaohusika ili wafanye vizuri.

Mimi nina ushauri kama ufuatao: Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Habari, Utalii, Wanawake, Watoto, Wazee na Vijana. Kamati yangu inahusiana na Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Kwa bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, tulitembelea na tulikuta mengi, lakini moja katika wazo ambalo linasita au awe na tahadhari Chuo hichi cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar vijana wetu wengi wanafaidika kutokana na chuo hichi; wanaomaliza darasa la kumi na mbili, wengine darasa la kumi siku nyengine kwa bahati mbaya kutokana na uwezo wake wanabahatika.

Lakini mwanzo huko nyuma tunakotoka chuo hichi mpaka kuendelea leo kinaendelea vizuri. Vijana wengi wamepata taaluma na wanaendelea kuipata taaluma na ukienda katika mahoteli mbali mbali wanafanyakazi nzuri bila ya matatizo. Hofu yangu iko hapa Mhe. Mwenyekiti. Kwa kuzingatia wakati tuliokuwa nao Chuo hichi kinataka kuunganishwa katika *SUZA*, si wazo baya lakini natahadhari huko mbele tunakokwenda kwa sababu unapotaka unakuwa laini kutoa maneno mazuri ili ufanikiwe. Lakini ukishakamata mpini huko mbele mengine yale utaona wale waliokuwepo katika chuo kile utaona hawana maana.

Mimi ushauri wangu naiomba wizara hili suala limeletwa na hapa ndio pahala pake kama litaendelea litaondoka kabisa kupelekwa *SUZA* sina pingamizi, lakini kwa ushauri kama kitaachwa walimu wake wakapewa nyenzo, maslahi mazuri, wakakiboresha kile Chuo kama kinavyotaka kuendelezwa sasa hivi nafikiri itakuwa imejiweka pazuri Mhe. Mwenyekiti na watafanya vizuri zaidi, vijana wetu wengi watapata masomo kuendeleza maisha yao.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika chuo hichi kimetoa wanafunzi wengi mpaka majeshi, wanajeshi wana sehemu za wapishi, wamekwenda kujifunza katika chuo hichi na wamefaulu vizuri na wamekuwa wapishi wazuri huko Jeshini wanasifiwa. Mimi ningeishauri sana wizara bado iwafikirie Chuo cha

Maendeleo ya Utalii wawezeshwe maslahi, kinachogombaniwa hapo maslahi tu na nathubutu kusema kama mafao wanayoyapata Chuo Kikuu *SUZA*, watapewa na hawa Chuo cha Maendeleo ya Utalii watafanya vizuri na maendeleo zaidi yatapatikana kwa wanafunzi wetu hawa. Naishauri wizara hili walizingatie na wajishauri sana kwa sababu vijana wetu wanaokwenda pale wamekata tamaa huko nje.

Lakini nasema kama kitaunganishwa na *SUZA* kitakwenda mwaka mmoja au miwili baadae wote watakuwa hawatambulikani wale watoto pale, watapoteza malengo yao na watakuwa hawatambulikani. Kwa hivyo, ningeishauri wizara lifikiriwe suala hili juu ya maendeleo ya vijana wetu na katika matembezi yangu katika nchi nilizobahatika Mhe. Mwenyekiti, kila nchi yenye utalii wana chuo chao na ndio maana ikaundwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, hichi chuo ni chao.

Sasa sikatai maendeleo zaidi, lakini nakataa yale mengine ambayo pamoja na kwamba kule watapata masoko mengi, watapata kueleweka. Lakini Chuo cha Maendeleo ya Utalii kinaeleweka vizuri, kwa sababu wenye mahoteli wote wanakuja kutafuta vijana wetu hapa hapa na wanafanikiwa vizuri. Naiomba wizara ikae ifikirie Chuo cha Maendeleo ya Utalii kiachwe kama kilivyo, lakini maslahi ya walimu na watendaji wengine yathaminiwe waongezewe tija ili wapate maendeleo yao. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa sababu unaposimama hapa unatafuta rai za kupata kuja kueleza kwa maslahi ya hao wanaotusikiliza. Chuo cha Maendeleo ya Fedha, Chwaka. Mhe. Mwenyekiti, Chuo hichi kizuri sana na Chuo kinatoa wataalamu mbali mbali hivi sasa katika fani za fedha. Lakini niseme tu kwamba Chuo hichi kimejitangaza vizuri zaidi kuliko Vyuo vyetu vidogo vidogo vingi katika nchi yetu nje na ndani ya Tanzania kwa sababu wanafunzi kutoka nje wanasoma na wanakingangania kweli kweli na wanapotoka pale shahada zao zinakubalika.

Ningeomba kama nilivyozungumza mwanzo katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii hawa walimu wakaangaliwa vizuri, wakapewa misaada mizuri kwa sababu Wizara ya Elimu ni Wizara mama, hizi taasisi zote ziko chini yao. Sasa panapokuja wale wahisani wanaotaka kuleta misaada wasielekezwe *SUZA* tu, waelekezwe katika Vyuo hivi ambavyo vinawanufaisha wanafunzi wetu, yaani vijana wetu.

Ombi langu hichi chuo bado kifikiriwe, kiangaliwe, wapewe nyenzo ili maendeleo ya chuo kile yazidi kutangazika huko nje. Naomba Mhe.

Mwenyekiti, hili suala Mhe. Waziri, kupitia wizara yake waliangalie. Lakini niseme tu kwamba Mhe. Mwenyekiti wa kamati pamoja na Mheshimiwa wa Jimbo la Magomeni, walizungumzia suala kubwa sana. Suala walilozungumzia wao wanasema tu kwamba tatizo lililokuwepo taaluma au kufikiwa wale wananchi wetu kutoa maoni yao hawakufikiwa. Mimi nasema walimu asilimia 80 au 90 ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii hawataki kuunganishwa na Chuo Kikuu. Lakini kwa kuburuzwa lazima hawana sauti itakuwa ndio hivyo. Wanaloomba wao bila ya kuficha Mhe. Mwenyekiti, wakati huu unakwenda na maneno ya fedha, wanataka kiende kule kwa kufuata maslahi tu wengine au hao wachache wanaotaka, aah! tukenda kule tutaongezwa mishahara lakini siyo ubora wa masomo. Ningeomba bado wafikiriwe taasisi hizi ambazo zinawachukua watoto wetu ambao wengi wanyonge. Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Chuo cha Uongozi wa Fedha, walimu wake wapatiwe fedha nzuri, wapatiwe maposho mazuri. Watafanya kazi usiku na mchana bila ya kuchoka. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hili tuliangalie sana huko mbele tunakokwenda. Bado Chuo Kikuu kitakusanya mambo mengi, tumeshuhudia walimu leo, tumeshuhudia sehemu nyengine mbali mbali bado kuna mkanganyiko kweli kweli. Mimi niseme Chuo cha Walimu waliokuwa pale N'krumah waliomaliza mwaka 2008 kama sikosei na wengine wanaokwenda sasa hivi kuna tofauti kubwa. Kwa sababu mkanganyiko umeongezeka zaidi. Wakati ule walimu walikuwepo huru, anatoka mtu hapa anakwenda Beit el Ras anasoma vizuri, anaamini akitoka pale ana stakabadhi yake ambayo inamnufaisha kusomesha. Na mpaka hii leo Mhe. Mwenyekiti, bado ile sifa ya Chuo cha Ualimu haipo, imeondoka haijuilikani. Lakini zamani mtu yeyote anakwambia Beit el Ras bwana, kwenye Chuo cha Ualimu. Leo unaambiwa umesoma wapi, aah! nimesoma Chuo cha Kiislamu, siyo mbaya. Lakini ile hadhi na ule mshiko uliokuwepo ipo tofauti sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ningeshauri sana hili suala likaangaliwa. (*Makofi*)

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, suala la Chuo cha Afya. Chuo cha Afya kama watapelekwa *SUZA* hata leo ninaunga mkono, wacha wapelekwe. Kwa sababu tunatafuta nini, wataalamu wa hali ya juu zaidi. Lazima daktari, muuguzi au nesi, sijui wanajua wenyewe majina yao, maana akikaa pale yeyote unamwita daktari, hawa lazima fani yao iwe ya hali ya juu sana, hasa tukizingatia wakati tuliokuwa nao huu. Bila ya taaluma nzuri na ufanisi mzuri inakuwa hatari kwa watu wetu. Kwa hivyo, hili mimi sina pingamizi nalo. Naiomba Wizara ijiandae ikichukue chuo hicho wawe mikononi mwao. (*Makofi*)

Hiyo misaada itakayokuja wapatiwe kweli kweli. Lakini ombi langu wanapofika huko wajulikane wamekifishwa kwa usalama wa maendeleo yao na usalama wa wananchi wetu. Kwa sababu kubeba mzigo wewe unakusanya tu, mwisho wanakuelemea itakuwa hatari. Mimi naomba tu Mhe. Mwenyekiti, kumpa rai Mhe. Waziri, kuna familia zetu hapa mfano, familia ya Shihata ana watoto wanane, mfano. Kuna mwenzangu ana watoto watatu. Sasa huyu mwenye watoto wanane na watatu, kuna tofauti kubwa sana. Mwenye watoto watatu hana mzigo mkubwa kuliko mwenye watoto wanane, hiyo tukiri katika maisha.

Sasa na *SUZA* kukusanya taasisi moja, mbili, tatu, nne, ni mzigo. Tena mzigo mkubwa kweli kweli. Bora *SUZA* ingeachwa peke yake na hii taasisi tuna Serikali yetu ambayo tunapata misaada tukaziombea, yaani jambo zuri kulisimamia. Ukilisimamia jambo lolote Mhe. Mwenyekiti, litafanikiwa lakini unaanza kutoka hawa Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Chuo cha Uongozi wa Fedha wakaunganishwa kule *SUZA*, wakifika hapo Mhe. Mwenyekiti, anakwambia aah! nyinyi si mulikuja kwa hiyari yenu, hatukutambueni tena. Mimi hofu yangu ipo hapo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iangalie kwa busara zake, isimamie vyema, lakini vyenginevyo ninakwambia hofu yangu huko mbele tunakokwenda, kwa sababu leo tupo hapa, kesho tunataka kuongezeka mbele zaidi. Yaani ukishamkabidhi taasisi zako mbili, tatu, nimekuongezea hizo hapo, watakurudieni nyie Wizara ya Elimu kukwambieni ule mzigo muliotupa mkubwa sana hatuuwezi. Hofu yangu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninajua unataka kunikatisha lakini ninataka kusema tu kwamba, mimi sina tatizo. Maoni yangu niliyotoa hayo. Naiomba wizara ikae izingatie, lakini izingatie kwa maslahi ya vijana wetu na izingatie kwa ubora wa elimu yetu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya watu wangu wa Jimbo la Kijitoupele ninaunga mkono kwa asilimia zote. Lakini ushauri wangu upokewe mikono miwili na sina tatizo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali, kwa mchango wako. Sasa nimpitishe Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi angalau ya kuchangia kidogo katika masuala yetu haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa moyo mzuri ambao Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein anajaribu kwa kila hali kuisaidia Zanzibar katika kufanikisha kwenye maendeleo yake. Ninajua mpaka mwaka atakaostaafu akiondoka tutakuwa tumejiweka vizuri sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia, niweze kusema ninatoa pongezi kwa Wizara pamoja na Waziri wa Elimu kwa kuleta Mswada huu pamoja na Naibu Waziri wake. Lakini pia Kamati yenyewe ambayo imepitisha Mswada huu pia ninaipongeza akiwemo Mzee wetu. Lakini masuala ambayo sasa ninataka Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa upeo ni kwamba wenzangu wameshatangulia mengi, ili jadala la Mswada lenyewe limejieleza vizuri sana. Lakini kuna mambo baadhi yanahitajika kidogo angalau tuweze kuyaeleza ili kuchukua hatua au kutahadhari kabla ya kufanya mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwetu sisi hapa tumekuwa ni watu ambao ninaweza kusema ni waanzilishi. Tunapenda kuanzisha jambo, tunapenda kubuni mambo, lakini baadae mambo haya yanatushinda au tunashindwa kuyafuatilia na baadae inabakia historia tu, lakini kile kitu chenyewe kama madhumuni yaliyokuwa yamekusudiwa Mhe. Mwenyekiti, yanashindwa kufikiwa au kutekelezwa masuala yote haya. Sasa ningeshauri sana kutokana na hali halisi kwa mwelekeo huu ambao tumejitayarisha tusirudi nyuma huko tulikotoka.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wetu wengi au Vyuo vyetu vingi vinasomesha watu, vinasomesha taaluma nyingi lakini taaluma zenyewe mara nyingi zikimaliza, wanafunzi wake wote asilimia 90 wanaisubiri Serikali kuajiriwa. Wanashindwa kile walichokisomesha kwa sababu yule ametoka kwamba ni msomi alitakiwa ajitafutie ajira na awatafutie na wenzake. Matokeo yake na yeye anakaa baoni anasubiri Serikali imuajiri. Sasa usomi huu sijui umefikia wapi wakati wewe umekwenda kusomeshwa ili uje usaidie, unasubiri ajira kutoka Serikalini, ajira zenyewe ni kumi katika mia. Sasa sijui tutaajiri wangapi na hili linakuwa wimbi kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri hawa wenye Vyuo kulitazama hili kwa kina wakati wa kusomesha Vyuo vyao ili kuliangalia. Maana yake wameshatangulia kusema hapa kwamba takriban watu wengi waliotoka katika vya N'krumah zamani, pengine labda sijui na Beil el Ras na wapi, ndiyo viongozi ambao wanatuwakilisha leo. Wakitoka wanatoka taaluma. Lakini leo mwanafunzi anakuwa na digrii kumi, lakini akifika hapa anakusubiri hapa anakusubiri wewe. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu kidogo walimu wetu au maelekezo mengi yakatoka kwamba wao wawe ni walimu wa kuweza kutafuta ajira ili kuendelea na mambo yote. Lakini pia niweze kuzungumza kwamba kwa eneo la Vyuo Vikuu vyetu, sasa hivi ningeisema kuwa Wizara anaona mbele yetu kuna mpango wa mafuta na gesi asilia. Haya mambo katika utaratibu wao kwenye somo moja ambalo lingetengenezwa katika mambo haya basi ni mafuta na gesi asilia ili kuweza kupata vijana wa kuanzia na hapa.

Haya mambo yanahitaji vitu vingi. Humu nimeangalia Mswada mambo mengi yamezungumzwa lakini watu wamegawana kwenye nafasi nyingi sana. Nikiangalia nafasi hizi Mheshimiwa, zote ni za kulipana, ni za kuliangalia. Mheshimiwa, ninachokiona bado wasi wasi. Zanzibar mpaka leo Wizara ya Elimu inategemea fungu au inategemea kasma ya Serikali na bado tunaongeza mambo. Bajeti zilizopo hazifikii kiwango, bado tunaongeza mambo. Sijui tumeshakaa tayari au bado, lakini ninahisi kwamba kuna haja kubwa ya Wizara ya Elimu pia kujikita katika kibiashara au katika kutafuta mapato ili kusaidia sekta hii. Hii sekta ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Sarahan, Mswada tunaochangia wa *SUZA*. Sasa nilikuwa ninakuomba sana kutokana na muda. Maelezo yako ni mazuri sana lakini kutokana na muda wetu rudi kwenye hoja zako na michango yako. Nakuomba sana. (*Makofi*)

Mhe. Suleimani Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, yote ni jumla ya mafanikio ya haya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Sarahani, ninachokisema mimi hapa michango yako ni mizuri na yote inamanufaa kwa Mswada kama huu, lakini ninachokuomba ulenge zaidi kutokana na muda tulionao, ili isije ikawa yale ambayo umeyakusudia kuyazungumza katika Mswada huu muda wako ukawa umekwisha. Kwa hivyo, ninakuomba sana kwa hilo.(*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako kwa mambo niliyonayo kwenye Mswada huu, mimi ningeomba kuahirisha kwa *time* niliyoiona pale hanitoshi. Kwa hivyo, bora ukanipangia muda mwengine.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, muda wa dakika kumi na tano niliyokupa ulikuwa unakutosha. Lakini kwa vile umeona haukutoshi, sifikirii kama utapata

muda mwengine wa jioni. Lakini nilikuwa nakuomba ndiyo maana nikakusisitiza kuwa uendelee na mchango wako ulenge pale pahali ambapo ulipopakusudia. Kwa sababu ulikuwa tayari unatoka unasema mambo ya mafuta ya gesi, ulikuwa unazungumza masuala ya bajeti. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nakuomba sana uendelee ili tumalize dakika zilizobaki.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nisubiri niangalie kidogo yale ambayo ninayaona ni muhimu, kwa sababu nilikuwa na mengi nimeyapanga kidogo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nawaombeni Wajumbe makeleleni yenu ya makofi mutulie. Mimi ninachangia Mswada wa maana sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejikita zaidi katika masuala ambayo kwenye vifungu ambavyo kama Kifungu 16(b) kutakuwa na Bodi hizi za kifedha katika mipango ya maendeleo, itakuwa wajumbe hawa ambao wameekwa hapa. Sasa ndiyo lengo langu lilikuwa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilililokuwa ninazungumzia wajumbe na hizi Kamati, wenzangu wamezungumza mambo mengi hapa kuhusiana na hawa wajumbe ambao walizungumza watakuwa kila Vyuo, Chuo kimoja au ile sekta kimoja ambayo ninahisi huu ulipaji pamoja na hizi gharama ambazo kwa kweli Wizara ya Elimu ninaionea huruma. Haya mambo ni mengi ukiyatizama na fedha ninazoziona ndiyo malengo yangu Mhe. Mwenyekiti, niliyokuwa ninapigia kelele. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Sasa nilikuwa Mhe. Waziri, akija hapa aje atufafanulie kidogo hivi vyuo vyetu vinakuwa katika mtiririko wa kampuni moja au kila Chuo kitakuwa na maelekezo mengi kama haya ambayo ninahisi utakuwa ni mzigo mkubwa kwa Wizara ya Elimu. Lakini pia ambacho nilikuwa ninazungumza ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza tumejipangaje katika suala kama mwenzangu alivyozungumza suala la usafiri kwa mambo ya wanachuo. Mhe. Mwenyekiti, bado wanafunzi wetu wanapokuwa katika masuala haya wanakuwa na tabu sana ya usafiri. Sasa na kama ulivyosema mambo ya mjini pamoja na mambo ya shamba yanakuwa tabu. Sijui Mhe. Waziri, atakapokuja kama kutakuwa na tayari ukiachia kwamba sekta hii imeachiwa mambo binafsi, lakini mabasi ya Chuo au vitu gani, sijui itakuwa imejipangaje.

Lakini pia nilikuwa ninazungumza maslahi. Mhe. Mwenyekiti, humu muna maslahi ya watu ambayo yanakwenda kwenye taaluma nyingi ambazo ninahisi

tu kwamba bado tuna ulipaji mdogo wa mishahara katika Bodi zetu au katika walimu wetu. Sasa nilikuwa ninazungumzia tu kwamba je, tunakwenda mwendo wa kasi katika Vyuo vyengine ambavyo vitakuwa katika taaluma hizo. Lakini kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme vitu vyengine, lakini ninataka kutoa mfano mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuunganisha Vyuo vyetu hivi na kuweka maslahi. Nilitaka kuzungumza kuwa je, sasa hivi tutaondokana na viongozi wetu kupeleka watoto wao nje na kuweza kuwa tayari vinakidhi haja katika nchi yetu. Maana yake hii tunaanzisha lakini Mhe. Mwenyekiti, watoto wa viongozi hatuwaoni. Kwa hivyo, inaonekana kwamba taaluma yetu hapa inakuwa ni ya uso tu, lakini ukiambiwa umesoma wapi, nimesoma *SUZA* inakuwa taaluma yako haithamini vizuri. Sijui Mhe. Waziri wa Elimu akija ataniambiaje kuhusu suala hili. (*Makofi*)

Lakini pia nilikuwa ninazungumzia suala la Vyuo. Nilikuwa ninazungumzia Mhe. Mwenyekiti, tunaposoma tunasoma sekta nyingi za afya na kila kitu, lakini wakati wa kurudia vitendo vya kwenda kusoma badala ya vitabu, nikisema *practical*, ukiachia *theory*, bado sioni kwamba Serikali imejipanga wanafunzi hawa wa Mahoteli, wa wizara gani, Wizara ya Afya wanakwenda *practical* ili kuja kuleta manufaa katika manufaa kwenye masuala yetu. Inakuwa mtu anasomea kitabu, halafu anakwenda kumpasua mtu kwa kutumia kitabu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninaliangalia sana ili tuangalie kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona yananitosha hayo. Nakushukuru sana kwa kuchangia.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwa mchango wako mzuri na kwa kukamilisha muda ipasavyo. Lakini na mimi niungane na wenzangu wote waliotangulia kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, pamoja na watendaji, lakini niwapongeze wachangiaji wote waliopata fursa ya kuchangia kwa muda huu. Na ninapenda niwaambie katika kipindi kitakachokuja kabla sijaahirisha tutakuwa na mchangiaji Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akifuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niahirishe kikao mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.52 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi), baada ya hapo atakuja Mhe. Miraji Khamis Mussa. Mhe. Simai Mohamed.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nimejipanga kuwa mtu wa pili, lakini nitasema yale ambayo naamini yataweza kutusaidia katika mswada huu. Awali ya yote nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pia, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuleta mswada huu kwa nia njema kabisa katika kuviunganisha vyuo vyetu na kuhakikisha kwamba suala la elimu kwa upande wa nchi yetu ya Zanzibar na watu wake itachukua sura mpya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii pia kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, rafiki yangu kipenzi chetu Dk. Mwinyihaji Makame na wajumbe wote kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo asubuhi.

Mhe. Naibu Spika, ukiisikiliza hotuba leo ya Mwenyekiti wa Kamati wakati anaitowa leo asubuhi, utaona kabisa vitu ambavyo alikuwa anavizungumza alitoa akikusudia kwamba waziri atakapokuja kufanya majadiliano, basi aweze kujibu hoja kadhaa ambazo inaashiria au inaleta sura kwamba kuna mambo bado Mwenyekiti wa Kamati hajaridhika juu ya mswada huu, kitu ambacho pia kinatutia hofu sisi wajumbe kwa sababu ikiwa kuna mambo ndani ya kamati bado hawajakubaliana, basi ni vyema Mhe. Waziri, atakapokuja hapa ayajibu yale ambayo ameyataja leo asubuhi kwa faida ya wajumbe wote na ili tuweze sisi kupata uhakika juu ya mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme mswada huu una maeneo mawili au matatu nataka niyachangie. Moja nataka nizungumze juu ya hofu ambayo iliyokuwepo nje kwa wananchi wetu, pamoja na wana vyuoni wenzetu. Lakini pia ukiangalia mara nyingi katika *strategy* yoyote inapotaka kuanza, huanza kutoka juu na ikashuka chini na tukahakikisha kwamba wale wote wanakuwa katika sura au picha ya pamoja. Mswada huu kwa kweli bado kuna hofu na ni vizuri atakapokuja Mhe. Waziri, kuja kufanya majumuisho, basi atueleze yale ambayo tunaamini wananchi kwa ujumla wataweza kumsikia.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja, nataka nitowe mfano. Mwaka 1935 Rais wa Marekani ambaye anaitwa Franklin Delano Roosevelt ambaye ni Rais pekee wa Marekani ambaye alikaa kwa vipindi vitatu. Wakati anatia saini ya mswada wa 122 wa *Social Security Act*, namnukuu, alisema;

"*We can never ensure 100% of the population, against 100% of hazard of life and we have to try to frame a law, which will give some measures of the protection to the every citizen, and to his family against the loss of a job, and against poverty ready on all age".*

Wakati analeta mswada huu kwenye *House of Representatives*, pamoja na mbele ya hawa wajumbe wa *senate* wao, palikuwa pana hofu kubwa sana, wengi pia walikuwa hawaamini kama hili jambo litakuwa. Lakini leo miaka zaidi ya 60 wamekuja, ametoka *Franklin Delano Roosevelt,* akaja *Harry S. Truman,* akaja *Dwight Eisenhower,* akaingia *John F. Kennedy,* akaingia *Lyndon B. Johnson,* akaja *Richard Nixon, akaja Gerald Ford,* akaingia *Jimmy Carter,* akaja *Ronald Reagan,* akaingia *George H. W. Bush senior,* akaingia *William J. Bill Clinton,* akaja *George W. Bush junior* na sasa tunaye *Barack Hussein Obama.*

Lakini lile jambo ambalo walikuwa hawaliamini wakati ule, leo miaka 60 kila Rais anayekuja basi anapita njiani analigusa na analiboresha. Chuo hiki Kikuu cha Taifa Zanzibar, kilianza kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1999, chini ya kamanda wetu Rais mstaafu Mhe. Salmin Amour. Akaingia Rais Karume akaboresha kwa mambo ambayo alihisi anataka kuyafanya, na leo Rais wetu na kipenzi chetu Dk. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ana malengo haya haya yenye sura mfanano, lakini bado kuna hofu. Sisi tuna amini hofu hii itaweza kuondoka kutokana na michango wa wajumbe wa Baraza. Najua waziri atakapokuja hapa ataweza kutueleza.

Mhe. Naibu Spika, jambo la mwanzo ambalo lina hofu ni suala la fedha. Mara nyingi unapotaka kuunganisha hivi vyuo, *issue* ya rasilimali zitakavyokwenda. Ukiangalia mfumo wa chuo uliokuwepo wa *ZITO* pamoja na Chuo cha Fedha cha Chwaka, hawa wamekuwa wanajitegemea wenyewe. Sasa kwa mpango huu ambao unataka kupangwa sasa hivi, kuwa wote wawe wamoja, sasa mgawanyo wa fedha utakavyokwenda na ukiangalia na hapa uchache tuliokuwa nao juu ya rasilimali, pamoja na hizi fedha tulizokuwanazo basi hapa nashauri pafanyike *transition period*, yaani pawepo na Sheria za mpito na twende hatua baada ya hatua, hakuna haja ya kwenda kwa haraka, ili malengo ambayo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameyakusudia, basi waziri aweze, hakuna lazima kulazimisha jambo.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukiangalia katika suala zima la suala la fedha, ukiangalia Dar-es-Salaam kwenye suala la vyuo, ukiangalia kwenye masuala ya fedha, ukitaka kuangalia hiki chuo, kule wana vyuo vile vya *DUCE* na *MUSE*, *Dar-es-Salaam University, College Education*, pamoja na ile *MUSE*. Ambapo hawa wako *autonomous* kabisa na *independent* kwa masuala ya fedha na wanatumia kwa mfumo wa *college*. *Ok,* inawezekana kuna hisia kwamba kama utazigeuza kuwa *colleges* hizi, kwamba wanafunzi hawatoshi. Lakini ukiangalia kwenye mtandao suala la idadi ya wanafunzi halipo kwenye hoja, na kama utazifanya hizi ziwe *constituent colleges* ambazo zinajitegemea kifedha na wanapata *vote* yao *independently* kama ni *subvote* wakati wa *budget*, angalau sasa hizi zitakuwa zinasimamia. Hata tukimfanya *VC* wa chuo hiki kazi yake kuangalia hesabu, kuanya *maintenance*, akatafuta badala ya kuangalia mambo makuu ya chuo ambayo yanakuwa kwenye kazi zake, akajikuta yeye moja kwa moja anasimamia masuala ya fedha, huku hizi taasisi nyengine zinaangamia.

Leo Mhe. Naibu Spika, ukienda kule kwenye Chuo cha N'kurumah, watu wanajisaidia baharini, kutokana na ma-*limitations* ya *resources* zilizokuweo. Sasa hii hofu iliyokuwepo lazima tuwe makini sana na lazima tujuwe kwa ujumla vipi tunataka kwenda navyo, na tuangalie kwenye mifano ya nchi ambazo tunazijua kama Vietnam, Corea, Northern Ireland ambazo leo Mhe. Mwenyekiti, alizitaja hapo juu. Lakini ukiangalia suala la *TCU* kwa ujumla kazi zao pamoja na *NACTE*, ukiangalia katika *issue* ya walimu ambao wanatumika hivi sasa, na kama tutaamua kuzi-*merge* hizi zote tuwe moja kwa moja na sheria ikapita, na tukaenda kwa haraka, hawa wanafunzi ambao sasa hivi wako chini ya *NACTE* kwa upande wa Chwaka, hawa wanatakiwa wamalize katika haya masomo yao, halafu tutayarishe wanafunzi watakaokuja, waanze kwa hizo *degrees* kutokana na hizo shabaha na malengo, na kazi ambazo watatajiwa utaratibu watakaopangiwa na *TCU*.

Lakini pia hawa walimu ambao wanaosomesha sasa hivi katika hivi vyuo vya Chwaka na vyengine, kwa mujibu wa taratibu za sheria ambazo wanatakiwa wajuwe *qualification* na *standard* ya *TCU* chini ya *SUZA*, wengine hawa watashindwa kutimiza masharti ya *TCU*, ina maana hapa itabidi kuna walimu wengine tuwapunguze tuwapeleke chini, wakasomeshe kwenye *certificate* na diploma na wengine itabidi tuanze kuwasomesha kutoka sasa, ili waweze kutimiza vigezo na masharti. Kwa sababu utaratibu wa mwalimu kutimiza masharti pale ambapo anasomesha katika Vyuo Vikuu, kwa chini ya usimamizi wa *TCU* inajulikana kabisa.

Sasa hapa Mhe. Waziri, atakapokuja, atueleze katika mpango mzima alioutaja katika vitu viwili, kwenye suala la fedha na juu ya walimu na hawa wanafunzi watakaomaliza katika mpango mzima juu ya hii *transitional period*. Lakini pia nilizungumza suala hili la *management* ya fedha na kwa ujumla juu ya hawa wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika Chuo cha Chwaka, hawa wanasomesha *profession careers.* Ukiangalia kwa upande wa *SUZA* ni *more academic*, unapochukua vyuo viwili hivi moja kwa moja na vyengine kwenda kuviunganisha, lazima uwe na utaratibu ambao utakuwa ni wa uhakika. Utaratibu ambao hautaleta hofu, utaratibu ambao utalinda maslahi ya walimu, utaratibu pia ambao utaleta maslahi ya vijana wetu ambao wanaoendelea sasa hivi kusoma katika hivi vyuo. Hapa nataka niseme, kwa sababu hapa tunaweka misingi leo katika hivi vyuo vyetu, kwa hivyo, lazima tusifanye kwenda kwa haraka sana. Kwanza tuhakikishe wale wote tunawaunganisha, asubuhi wawe wamoja, kesho tunaamka *Assalam Aleykum,* ni kubwa kahawa asubuhi na wali mchana, hapana, twende kidogo kidogo, pole pole ndio mwendo, wazee walisema haya. Ikiwa Rais wetu wa Zanzibar alipitisha sheria, Mhe. Rais Karume tumeona matunda aliyoleta kule kwenye Tunguu *campus,* tumeona Rais wetu wa Zanzibar sasa hivi Dk. Ali Mohamed Shein mengi ambayo anaelekeza na ambayo sasa anayasimamia.

Mhe. Naibu Spika, katika misingi hii, nashauri sana twende katika mwendo, hatua ya Rais wa Zanzibar kuja na malengo haya pamoja na serikali yake kutaka kuviunganisha, ni hatua moja muhimu sana katika historia yetu na ni jambo zuri la kuliunga mkono, lakini lazima haya yote maslahi ambayo tunayazungumza yote tuweze kuyachukua. Mimi niliwahi kuwa mjumbe wa Baraza la Chuo cha Karume, chuo kile ukiingia kule ndani kuna changamoto walizokuwanazo za kifedha, changamoto juu ya rasilimali, changamoto juu ya watu na hawa wao wanapata fungu lao na wanawekewa moja kwa moja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa hivi vyuo kuvipeleka vyote moja kwa moja, hapa lazima tufanye mambo kwa mpango na kwa uhakika. Mpango wote huu nategemea sasa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, yeye atakapokuja, basi ataweza kutuambia moja kwa moja katika mipango yake yote ambayo Mwenyekiti leo asubuhi aliyezungumza na atakuja kutujibu. Lakini nikiangalia katika hiki Chuo cha Utalii cha Maruhubi.

Mhe. Naibu Spika, katika vyuo mara nyingi unapotaka kuviunganisha, lazima kwanza kuna misingi lazima ufike. Kwa mfano, ukiangalia Chuo cha *SUZA State University cha Zanzibar*, wao hawashughuliki na masuala ya *Hospitality Industry*, hawajawahi kufundisha, hawana uzoefu katika suala hilo. Mara

nyingi kama utamchukua yule utamleta huku, basi lazima wewe angalau uwe na uzoefu wa kuweza kuwasimamia. Sasa hapa hiki chuo cha *Hospitality Industry* cha Maruhubi, kinachukuliwa kinapelekwa *SUZA*, ni utaalamu gani *SUZA* waliokuwa nao ambao wataweza kuwasimamia. Sizungumzi suala la *tourism*, nazungumza suala la moja kwa moja la *Hospitality Industry*, ina maana unaangalia katika masuala ya *hotel management*, kama kutakuwa na masuala ya *ticket*, masuala ya *tour operations.* Haya ndio mambo ambayo yanaongoza nchi yetu, haya ndio mambo ambayo vijana wetu wanachukua *courses* tofauti pale Maruhubi na kufaidika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe ni matunda ya pale Chuo cha Maruhubi, nilichukua *Supervisor Record Level*. Lakini katika mfumo huu unaokwenda hata mimi hupata hofu. Mhe. Waziri, utakapokuja hapa, mimi sina mpango wa kuzuwia kifungu, sitegemei nitachangia hata kifungu chochote, sheria umeshaileta nataka muipitishe, nimeona uzoefu wa jana, nimeona hapa jinsi Mwanasheria Mkuu kila mawazo ninayoyatoa anasimama kuyapinga, mimi nilikuwa natoa ya kwangu, alipokuwa na hoja yeye nikamkubali kama ana hoja, nilimuona Waziri wa Nchi ni jinsi gani yeye anavyosimama kutupinga.

Kwa hivyo, Mimi kwa upande wangu sitopinga kitu, kifungu kitapita kifungu baada ya kifungu, moja baada ya moja. Angalau mtupe matumaini haya mawazo yetu sisi wawakilishi wa wananchi tunayoyatoa juu ya jambo hili kubwa la nchi yetu na ni letu sote, kwa hivyo, mtatupa matumaini, mtatueleza ili tukusikieni vizuri na wananchi wametusikia na wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu wananisikia, mawazo yao walionituma nimeyaleta kwa Wazanzibari wote nimeyasema.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe sana kwa nafasi uliyonipa, nimshukuru Mhe. Waziri na Mwenyekiti, kama vile asubuhi. Leo kwa mara yangu ya kwanza sio kama ninavyokaa, wala sina nia ya kuomba muda wa ziada. Mawazo yangu yametosha nafikiria, naamini yamesaidia, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Miraji Khamis Mussa, baada ya Mhe. Miraji Khamis. Waheshimiwa Wajumbe, naomba mzungumzaji awe mmoja tu. Baada ya hapo ni Mhe. Miraji Khamis Mussa, atafuata Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Mhe. Miraji Khamis hayupo, kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba uanze kuchangia.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kutuletea mswada huu leo hii tukaweza kuujadili mswada huu ni muhimu sana wa kuunganisha vyuo vyetu ili kuwa na chuo kimoja ambacho kitakuwa na sifa na hadhi kwa Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ambao ulifanyiwa kazi kubwa, nilikuwa namsikiliza kwa makini Mhe.Waziri wakati anatoa hotuba yake, mswada huu umefanyiwa kazi kubwa na umefanyiwa utafiti na wataalamu waliobobea, wasomi na wameona umuhimu wa kuunganisha vyuo hivi kwa ajili ya kuleta tija kwa Wazanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lengo lao nimelifahamu, nilivyokuwa nasikiliza na niliposoma huu mswada niliona kabisa kwamba tumeona vyuo vya wenzetu kuna umuhimu wa kuweza kuimarisha vitivo vyetu ndani ya Chuo Kikuu, lakini tuwe na Chuo Kikuu ambacho kitatambulika kitaifa na kimataifa, na ili tuweze kutambulika ni lazima sifa yake iweze kufikia vigezo Kwa hivyo, hili nalipongeza sana na wataalamu wale kwa kweli wamefanyakazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, pia sote tukumbuke kwamba, mimi mwenyewe binafsi najivunia sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu ni mdau mkubwa ambaye nimetokea katika maeneo hayo hayo, ambapo elimu yangu mpaka hapa nilipofika basi nilipitia ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naamini kwamba wengi wetu humu tutakiri kwamba tulisoma kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba mswada huu leo ukipitishwa na tukawa na Chuo Kikuu kimoja, ambapo chuo hicho kitakuwa kina hadhi ambayo sisi tunaitegemea. Tunategemea kabisa kutakuwa kuna utumiaji mzuri wa rasilimali. Nalizungumzia suala la utumiaji mzuri wa rasilimali kwa sababu *campus* zitakuwa ziko tofauti, lakini uongozi utakuwa ni mmoja chini ya bodi ambazo zitaundwa. Bodi zile zitakuwa zina-*monitor* zile *activities* za chuo. Lakini katika hili maana yake pia tutaweza kuongeza ule uwajibikaji, lakini tutarahisisha hata kwa watu wetu katika *application,* lakini hata katika kupata urahisi wa shughuli mengine za masomo. Kwa hivyo, hii inaonekana italeta tija sana.

Vile vile katika hili nilikuwa nalitizama kwa upeo wake, tutaongeza pia hadhi ya vyuo vyengine. Kwa mfano, Chuo cha Kilimo cha Kizimbani sasa hivi, ambapo sisi wenyewe tulitokea, chuo kile tulianza na cheti, tumekuja sasa hivi

na diploma, lakini hata tukiingia kwenye hadhi ya vyuo, maana yake tataweza hata kutoa *degrees* za kilimo, mifugo na fedha ndani ya nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo, tutaweza kujitambua, lakini na kujitambulisha pia kwa wenzetu.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia nchi mbali mbali ambazo zimeweza kuunganisha vyuo. Tuchukulie mfano Uholanzi, ukenda pale Wageningen utaona ndani ya *campus,* lakini unaiona Wageningen sehemu moja tu, labda ya *Animal Science*. Lakini ndani ya Wageningen, kuna *departments* tofauti, vitivo vingi na vimekuwa *effective*. Kwa hivyo, mimi naomba nishauri sana katika hili, tuiunge mkono Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tuupitishe leo mswada huu, ili na sisi tuweze kujijengea hadhi kama vyuo vyengine vya kimataifa viliopo. Tumeona kule sehemu za *UK*, wale waliosoma, lakini katika maeneo yale tunaona kabisa na sisi tunatamani siku moja nchi yetu hii ya Zanzibar tufikie pale ambapo tunataka.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwamba serikali yetu kwa kupitia Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein ana nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba mswada huu leo tunaupitisha ili kuhakikisha kwamba hadhi ya elimu ya juu ndani ya nchi yetu basi tunaipa nafasi. Mimi niwaombe sana wajumbe, tuupitishe mswada huu kwa asilimia mia juu ya mia ili tuweze kuwa na Chuo Kikuu kimoja kikubwa kitakachotujengea umaarufu ili na sisi Wazanzibari tuweze kujidai.

Mhe.Spika, naomba kutoa hoja, naunga mkono mia juu ya mia.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja iliyo mbele yetu, nashukua fursa hii kwanza kufafanua baadhi ya hoja katika ujumla wake na itakapokuja katika hoja mahususi Mhe. Waziri, atakuja kufafanua baadae.

Kulikuwa na wasi wasi na maoni ya baadhi ya Wawakilishi kwamba wanadhani kuchukuliwa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni na kuwa skuli katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kilivunja hadhi yake, mimi kwa kutumia udhoefu kwanza ikiwa mwanafunzi wa Taasisi yenyewe, lakini pia baadae nikawa mhadhiri katika Taasisi yenyewe chini ya *SUZA*, ningependa kuto ushuhuda ufuatao kuonyesha kwamba Taasisi ya Kiswahili ilipopelekwa katika *SUZA* imeongeza ubora wake katika maeneo yote. Katika idadi ya wanafunzi, nakumbuka sisi tulikuwa tukisoma wanafunzi 12 mpaka 20 kwa mwaka, baada ya kuunganika wanafunzi wanaosoma pale wanafika 200,300 na kadhalika. Kwa hivyo, idadi ya wananchi wetu waliopata fursa ya kusoma Taasisi ya Kiswahili chini ya *SUZA* imeongezeka.

Pili, napenda kusema kabla hatujaunganisha na *SUZA* tulikuwa tunatoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada ambayo tunaita *Diploma* kwa miaka yote 30, lakini baada ya kuingia katika mfumo wa *SUZA programmes* zimeongezeka, tumeanzisha *Degree* ambayo pamoja na masomo mengine lakini inaunganisha *Degree* ya Kiswahili, tunaita Shahada ya Kiswahili. Lakini pia tukenda mbali zaidi tukaanzisha *Degree* ya Kiswahili kwa Kiswahili, mambo hayo hayakuwepo hapo kabla, baadae tumeanzisha *Master Degree* na Sasa pia tunayo *PhD* ya Kiswahili, je, hayo yanapunguza hadhi ya Taasisi ya Kiswahili, bila ya shaka yameongeza hadhi.

Lakini pia kutokana na mafunzo hayo yameifanya Skuli ya Kiswahili na lugha za Kigeni ambayo sasa hivi tunaita Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, pale awali tukiita Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Kwa hivyo, sasa hivi inajulikana zaidi na imeweza kuanzisha mahusiano na Taasisi nyengine mbali mbali duniani katika kuimarisha masomo ya Kiswahili, pamoja na tafiti nyengine zinazoambatana na Kiswahili.

Lakini kubwa zaidi wakati ule walimu waliokuwa wakifundisha pale walikuwa na Shahada za kawaida, kulikuwa kuna baadhi ya walimu walikuwa na Stashahada, wengine Shahada ya kwanza, na wachache Shahada ya pili. Lakini leo walimu wenye sifa za juu kabisa wanapatikana katika Taasisi hii, kwa hivyo, nadhani tumeifanyia haki yake.

La tatu ambalo ni muhimu sana linaloonyesha ubora wa taasisi hii ni kwamba sasa *Programmes* zake zinahakikiwa na Mamlaka zinazohusika na Elimu ya Juu, kwa lugha nyengine zinahakikiwa na *TCU* ili kuimarisha ubora, na tahakiki zilizopo zinatuonyesha kwamba tuko katika hali bora zaidi, hatufanyi sisi hizo tahakiki wanafanya wao.

Lakini tumeimarisha pia suala la kuwa na watahiniwa nje kwamba hatufanyi mambo peke yetu, pale tunatunga mitihani yetu tukajisainisha wenyewe, hapana, tunao watahini wa nje kutoka Vyuo Vikuu mbali mbali, ambao wanaangalia ubora wetu wakiunganisha na ubora wa vyuo vyengine. Kwa mfano, tunao watahiniwa wa nje kutoka Chuo Kikuu cha Taifa kutoka *University of* Dar-es-Salaam, na vyuo vyengine. Na katika baadhi ya lugha za kigeni tunao watahiniwa wa nje kutoka katika nchi nyengine mbali mbali, kwa hivyo, niwatoe wasi wasi kwamba Taasisi ya Kiswahili ambayo sasa inaitwa Skuli ya Kiswahili ambayo ipo chini ya *SUZA* imefanya vizuri zaidi kuliko wakati mwengine wowote.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Taasisi nyengine ambazo zimeunganishwa na *SUZA* hapo kabla nayo ni Chuo cha Walimu N'kurumah, ingawa mazingira ya kuunganisha N'kurumah na hivi vyuo ambavyo tunatarajia kuviunganisha sasa hivi ni tofauti kidogo, kule hakukuwa na utafiti na *Studies* zilizofanywa, wala hakukuwa na mazungumza, isipokuwa ni uamuzi tu wa kiutawala ambao tulichukua. Lakini hata hivyo, nako pia tumeongeza ubora wa taaluma za ualimu, tumeanzisha *Degree programmes* ambazo zinaendelea, lakini pia tumetoa mafunzo kwa walimu wetu ambao wako katika ngazi mbali mbali, wengine za uzamili na uzamivu, kwa hivyo, bado kabisa uwezo wa eneo lile, uwezo wa kuunganisha na tukaendeleza ubora katika Vyuo vyetu bado upo chini ya *SUZA*.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala hili la mabadiliko, nadhani tuwanasihi na tuwaelimishe wananchi wetu wasiwe na hofu na mabadiliko, mabadiliko katika dhama hizi ni jambo la lazima, ukisita kwa hofu, utachelewa mtoni kwa kuitaka Kibweni. Kwa hivyo, tunahakikishia wananchi wetu kwamba *SUZA* ina uwezo wa kuunganisha Taasisi hizi na bado ubora wake ukanyanyuka zaidi kuliko ilivyo hivi sana. Chuo Kikuu cha Taifa kina uwezo katika ngazi mbali mbali *in put*, kwa maana ya kwamba kusimamia *programmes* za aina zote, za skuli zote, kusimamia ubora wa walimu wa ngazi zote, wa taasisi zote na skuli zote. Kuweka *programme* ya mafunzo wanaita *Training Programme* kwa taasisi zote na skuli zote zitakazounganishwa uwezo huo upo, na upo kutokana na kujifunza katika miaka yote ile ya kuanzishwa kwakwe Chuo Kikuu cha Taifa.

Nataka niwahakikishie wananchi wetu kwamba Chuo Kikuu cha Taifa kinafanya bora zaidi katika miongoni mwa vyuo vikuu vya Tanzania, kina sifa ndani na nje ya nchi na sifa hizi zinatokana na ukweli kwamba katika ngazi za *Programmes* zake, katika ngazi za mikakati yake lakini kubwa zaidi katika ngazi ya wahitimu wake, hawa wanakubalika duniani, wenzetu ambao wanawatumia wahitimu wetu katika Chuo Kikuu cha *SUZA* wanatueleza hivyo, wale ambao wanapata fursa ya kufanya masomo ya juu ya Uzamili na Uzamivu kwa kweli Chuo chetu kinatangazika kupitia kwao. Na wale wengine ambao wanapata fursa ya kufanyakazi katika sehemu nyengine pia taswira yao iko nzuri. Wanaulizana hasa mmesoma wapi nyie, wanaulizana, *SUZA*, kwa hivyo, inapata sifa. Kwa hivyo, napenda kuwahakikishia kwamba uwezo huo upo, wale waliokuwa na mashaka kwamba labda *SUZA* haina *capacity* na *experience*, nadhani wazo hilo kuanzia sasa tulifute, uwezo huo upo.

Lakini pia ina uwezo mwengine wa kuendesha masuala ya tafiri, uwezo na wataalam katika fani hizo pia wapo katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Sasa hofu iliyopo ni ile ya kawaida ya binaadamu kuhofia mabadiliko basi ndio

hofu iliyopo, lakini kubwa zaidi hofu iliyopo ni baadhi ya wafanyakazi wa Taasisi hizo kuona kwamba, labda watapoteza ajira zao au watapoteza hadhi zao basi ndio hofu iliyopo. Lakini si kwamba kuna sababu hasa ambayo inaifanya labda watu wakatae, inawezekana wameelezwa vibaya, tumewaelekeza vibaya, lakini kwa kweli jambo hili ni muhimu sana sana kuunganisha vyuo kwa ajili ya kuimarisha *Programmes* zetu, na tumesema mwanzo na ndio kauli ya Serikali kwamba *Programmes* zilizopo hazitafutwa kama kuna *Certificate* ya *Tourism* hiyo itaendelezwa, kama kuna kozi nyengine ndogo ndogo nazo zitaendelezwa na zaidi kwa kiwango kikuba zaidi.

Mwandishi mmoja anasema karibu ndani, hebu mkavitembelee ndani muvione viko vipi, musitizame kauli zao tu, habu ingieni ndani muvitizame, nina hakika kama mungeingia ndani mukaona namna wanavyoendesha *programmes* zao basi nadhani tungekubaliana kwamba ipo haja ya kujenga uwezo wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana Kamati ya Ustawi wa Jamii imechukua maoni mbali mbali, lakini baadhi ya wadau maoni yao hayakuingizwa katika kamati hiyo, maoni yaliyotawala zaidi ni maoni ya *ZIToD* na *ZIPA*, hatukuona maoni yaliyochukuliwa na Chuo Kikuu chenyewe cha Taifa ambao pia walifanya mazungumzo na Kamati, lakini na sisi Wizara pia tulikuwa na maoni yetu yamewekwa pembeni, lakini kubwa zidi walikwenda safari tulidhani yale waliyojifunza katika safari yangeweza kupata nafasi katika waraka wao.

Hata hivyo, ni kwamba ushirikishaji wa wadau katika zoezi hili umekuwepo na ushirikishaji siku zote si lazima uwe asilimia mia moja, ulikuwepo katika hatua za mwanzo na hatua za awali, nina hakika kwamba na mimi pia wakati nikiwa Mhadhiri *SUZA* nimeshiriki katika kuutolea mawazo mswada huu, na Serikali ilianzisha kamati mbali mbali ambazo zilishirikisha Wajumbe kutoka Vyuo vinavyohusika. Mimi wakati huo nilikuwa ni Mwenyekiti wa wanataaluma *SUZA* kwa niaba ya walimu wenzangu tulishiriki katika mazungumzo mbali mbali.

Kwa hivyo, ile taswira inayojengeka kwamba labda watu hawakushirikishwa nadhani tuibadilishe, ushiriki ulikuwepo tena mkubwa, ni ushiriki wa kawaida, ni ushirikishaji wa kiutafiti, tusitegemee kwamba ushiriki wa wananchi utakuwa mia juu ya mia, huo utakuwa si utafiti tena wala sio maoni tena. Kwa hivyo, taarifa tulizonazo mpaka jana na juzi Vyuo hivi bado walikuwa wanakutana kushauriana namna bora kabisa ya kuweza kuingia katika suala hili, kwa hivyo, nadhani taarifa tulizokuwa nazo Wawakilishi nafikiri ni taarifa

kongwe, yaani za kale, lakini kama tungewarejea tena hivi karibuni nadhani wangekuwa na maoni mengine tofauti.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kusema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inawaomba wawakilishi watafakari katika pande zote, uzuri wa zoezi hili, ubaya wa zoezi hili, halafu kwa kulinganisha mwelekeo wa dunia ulivyo, si kwamba useme tu ubaya, ubaya, hapana, yaani kwa kulinganisha mabadiliko ya dunia yalivyo, tukitilia maanani maagizo ya Serikali kwamba, hakutokuwa na *Programmes* hata moja ambayo itaondolewa, zaidi itaimarishwa kwa viwango vinavyohitajika na kukubalika. Na hii ni tabia na utamaduni wa Vyuo vikuu kuendeshwa kwa viwango na kwa uwazi, kwa hivyo, nadhani tuchangie tukielewa kwamba tunapima, wakati wenzetu wamesimama sisi tunalazimika kwenda mbio, tukibaki nyuma kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki watu katika jamii yetu ya Zanzibar.

Kuhusu taswira ya *SUZA*, *SUZA* ina taswira nzuri kabisa duniani na inafahamika, lakini hapa ndani kidogo hasa tunapohusisha na mswada huu imekuja taswira kama hili ni wazo la *SUZA*, kwamba *SUZA* wamejitia kimbelembele wanataka Vyuo vikuu, si sahihi, hili ni wazo la Serikali, wao kama ni wadau walishirikishwa kama ilivyoshirikishwa *ZIFA*, ilivyoshirikishwa Chuo cha Afya na *ZIToD* ili kuweka mfumo mmoja bora unaotakikana.

Sasa nipende kuwatoa hofu kwamba, suala la ajira na suala la kuunganisha vyuo baada ya sheria kupita kutakuwa na vipindi vya mpito vya kuvijengea uwezo, kwa lugha nyengine kuwajengea uwezo watu ambao sifa zao kidogo zipo chini ili na wao waweze kuwa na sifa zinazohitajika, kama kulikuwa na hofu kwamba watu wataachishwa kazi hofu hiyo iondolewe mara moja, Serikali haitomuachisha mtu kazi mtu yoyote katika vyuo hivi.

Kuhusu Vyeo na mambo mengine hayo yatafuta taratibu za Chuo Kikuu ambazo zinajulikana zipo wazi wazi, mtu anayekamata nafasi fulani basi analazimika kuwa na sifa fulani, hizo zipo, lakini pia kuna utaratibu wake na mara nyingi taratibu za kivyuo zinajulikana kwamba, kwa naafasi nyengine zinaundwa Timu za kutoa maoni au za kupendekeza watu ambao wanadhani wanaweza kushika nafasi fulani, zikishapatikana, zinakwenda hatua kwa hatua mpaka kwenye Baraza la Chuo ndio linaamua kwamba, huyu anaweza kuwa Mkuu wa Skuli au laa, ni taratibu ziko wazi na za kidemokrasia kweli kweli.

Kwa hivyo, nadhani nimalizie mchango wangu kwa kumshukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii, lakini pia niwashukuru sana Wawakilishi wenzangu kwa kuweza kunisikiliza, ahsanteni sana.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na Wajumbe asubuhi ya leo, na muda mfupi uliopita mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu nyote ambao mmepata nafasi ya kuchangia mswada huu wa marekebisho ya Sheria ya *SUZA* Nam. 8 ya mwaka 1999, na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia kwa wakati huu, na pia napenda kuzingatia na maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, napenda niwatambue kwa majina wale wote ambao walichangia kwa kuzungumza na wale ambao walichangia kwa njia ya maandishi, ingawa mchango wao nimepata katika muda si mrefu, lakini natambua michango yao.

Kwanza kabisa napenda kuwashukuru sana wafuatao:

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
Mhe. Rashid Makame Shamsi
Mhe. Ali Suleiman Ali
Mhe. Suleiman Sarahan Said
Mhe. Simai Mohammed Said
Mhe.Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
Mhe. Hidaya Ali Makame
Mhe. Hassan Hamis Khafidh
Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
Mhe. Mnanga Mjengo Mjawiri Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amalil.

Mhe. Naibu Spika, michango ya wajumbe yote ilikuwa ni mizuri na kiudhati kabisa kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunakushukuruni sana kwa michango mliotuchangia asubuhi ya leo. Ni imani yetu thabit kwamba michango ambayo mmetuchangia itaboresha mswada wetu huu ulioko mbele yetu, lakini vile vile michango ambayo mmeitoa italeta mstakbali mzuri

baada ya kuunganishwa kwa vyuo hivi, basi kuona kwamba ile elimu bora ambayo Wizara Elimu inaitoa na kuona kwamba lile lengo la Serikali linafikiwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, michango mbali mbali ilitolewa na wajumbe kama ambavyo nimewataja hapo na nitapenda kuchukua zile hoja ambazo zimejitokeza kwa sana kutoka kwa wajumbe ambazo wamezitoa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala lililojitokeza la usimamizi wa rasilimali fedha, ni suala ambalo limejadiliwa sana na Kamati lakini hata na baadhi ya wajumbe nao wamelizungumza. Kimsingi Mhe. Naibu Spika, usimamizi wa fedha tunakubaliana na pendekezo la marekebisho ya kifungu cha 25 cha mapendekezo ya Kamati ili kutoa usimamizi mzuri wa fedha na kurahisisha uendeshaji.

Aidha, baada ya vyuo vinavyounganishwa kukaa pamoja na kujadiliana kuhusu mambo mbali mbali ikiwemo mambo ya fedha wamekubaliana kuwa baada ya vyuo kuunganishwa Afisa Masul kwa maana ya *Courting Officer* atakuwa ni mmoja. Hata hivyo, sheria na taratibu zinaruhusu kwa Afisa Masul kukasimu madaraka yake kwa Afisa au Maafisa wengine mbali mbali kama itakavyofafanuliwa na kanuni husika.

Kwa hivyo, kwa urahisi na ufanisi anaweza kukasimu muelekezaji, utekelezaji wa masuala ya fedha wakuu wa Skuli na Taasisi za Chuo. Bajeti kama kipengele muhimu cha masuala ya fedha kila skuli itatayarisha bajeti yake na itapitishwa na Baraza la Chuo. Fedha zote pamoja na ruzuku zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Chuo ambapo Skuli na Taasisi zitaingiziwa fedha zao kwa mujibu wa bajeti iliyokubaliwa na Baraza la Chuo.

Aidha, Kanuni za fedha za Chuo itahitaji kupitiwa upya kwa pamoja ili kuweza kukabili mazingira ya kuunganishwa huku. Mambo mengine ambayo vyuo hivi wamejadili na kukubaliana katika uendeshaji wa Chuo kinahusu namna ya kuripoti taarifa za fedha, jinsi ya ukaguzi wa ndani na nje utakavyofanyika na muundo wa kamati za ukaguzi, vile vile, ukusanyaji na mgawanyo wa mapato. Kwa kuanzia na mwaka huu wa fedha vyuo vitakuja na bajeti zao ambazo tayari zimeshapitishwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa msingi huu ni kusema kwamba hapatakuwa na wasiwasi wowote wa suala la fedha, kwa sababu kila Chuo kitakuwa kina bajeti yake kama ambavyo ishapitishwa na bajeti hizo zitaendelea kutumika kama ambavyo zinatumika hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, tulipokea ushauri kwa Mhe. Mwakilishi kwamba, tusimamie kikamilifu utekelezaji wa mswada wa sheria hii baada ya kupitishwa. Ushauri huu umezingatiwa na baada ya Baraza hili Tukufu kupitisha mswada huu wa sheria, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani kwa kushirikiana na Baraza la Chuo watasimamia kwa dhati kabisa utekelezaji wa sheria hii kikamilifu, na kwa kuwa Wizara yangu inawakilisha katika Baraza la Chuo kama ilivyoainshwa katika sheria mama ya Chuo tutahakikisha kwamba utekelezaji wa sheria hii unakuwa ni mzuri na katika hali ya juu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, binafsi yangu lakini na uongozi mzima wa wizara tutakuwa tunafuatilia hatua kwa hatua kuona namna fedha za Serikali zinavyotumika ndani ya Chuo chetu, lakini ndani ya hizi Taasisi nyengine za Chuo ambazo zitakuwa zimeingia ndani ya Chuo.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na wasiwasi vile vile kwa ushirikishwaji mdogo wa wadau. Kamati iliyounda na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, kushauri suala hili ilipita katika Taasisi zote na kutoa taarifa ya Serikali juu ya azma ya uunganishwaji huu wa Taasisi na walitoa maagizo ya kuwaarifu kujitayarisha juu ya suala hili na walifanya hivyo.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi zote husika katika uunganishwaji huu walishirikiana kikamilifu katika zoezi hili. Kwa mfano, vikao mbali mbali viliitishwa na kuwakutanisha watendaji na viongozi wa Taasisi zote husika na baadhi ya wakati vikao hivyo viliamua kutoa maelekezo kwa washiriki wa vikao hivyo kuwasilisha maendeleo ya suala hili katika Taasisi zao wanazotoka. Labda katika hali ya kibinaadamu inawezekana kwamba baadhi ya washiriki hawakuwa wakiwasilisha taarifa ipasavyo kama ambavyo maelezo ya Mhe. Naibu Waziri, alivyoyatoa ni kwamba si kila mtu katika kile Chuo kama kulikuwa kunakuja uwakilishi maalum. Kwa hivyo, kama uwakilishi ulikuwa haufikishi taarifa basi itakuwa hilo ni suala jengine na itakuwa ni mapungufu ya kibinaadamu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala zima la utoaji wa ubora wa elimu. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinaendelea kutoa elimu yenye ubora kwa kuzingatia utaratibu utakaoendeshwa na kitengo maalum kinachoratibu ubora wa elimu. Pia, Chuo kimetoa wahitimu wenye sifa ambao wamekuwa wamefanya vizuri katika elimu ya juu na wameajiriwa katika nafasi mbali mbali hapa Zanzibar na kwengineko.

Mhe. Naibu Spika, imani yangu kwamba hata ndani ya Baraza hili tunao wahitimu ambao wametoka ndani ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, mimi

binafsi nikiwa mmoja wao, lakini hata Mhe. Naibu Waziri, kama ambavyo ameeleza na yeye vile vile ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na sote ni mashahidi tunaona kwamba yale mazao ambayo *SUZA* wametoa basi wametoa mazao mazuri sana. Kwa hivyo, ubora wa elimu unazingatiwa sana ndani ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, ushauri umerekebisha kuongeza neno 'Chuo Kikuu' cha Serkali katika sehemu ya madhumuni na sababu tumeipokea kama hivyo Mhe. Rashid, alipendekeza na tumezingatia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid, katika kuchangia kwake alimuomba Mhe. Waziri, afute kauli yake aliposema kwamba; vyuo hivi baada ya kusimama vinaweza kutangazwa na kuwa Chuo Kikuu. Mhe. Naibu Spika, Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, sifuti kauli hiyo kwa sababu kauli hiyo iko sahihi na kauli hii inapatika ndani ya Mswada wa sheria katika kifungu nambari 24(36)(a), kimeeleza kwamba;

"Mkuu wa Chuo pale ambapo Chuo ama Taasisi ambayo iliunganishwa na Chuo itakuwa imejiweza basi atatangaza kwamba ni Chuo Kikuu kinachojitegemea".

Kwa hivyo, kwa mnasaba huo Mhe. Naibu Spika, kauli yangu bado inabaki kama ilivyo kwa mujibu wa sheria ambayo tutaipitisha hapa leo hii.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna wasiwasi juu ya uwezo wa *SUZA* kuhimili mahitaji ya vyuo vyengine kwa bajeti waliyonayo. Kama ambavyo tulieleza awali ni kwamba kila Chuo kina bajeti yake na bajeti zote hizi zitahamia ndani ya Chuo Kikuu cha *SUZA*. Kwa hivyo, ni kusema kwamba *SUZA* atakuwa watoto, lakini watoto hawa kila mmoja tayari ana chakula ambacho anakula. Kwa hivyo, kwa kuendeleza msingi ule ule ni kwamba, kila mmoja atakula chakula ambacho kipo na haitakuwa kwamba labda *SUZA* labda itoe chakula chengine zaidi ya kile ambacho wale walikuwa wanakula. Kwa sababu idadi ya watoto itakuwa ni wale wale, kwa hivyo, hata idadi ya mlo wao bado itabaki kuwa ni ile ile. Kwa hivyo, kwa msingi huu ni kwamba *SUZA* haitozidiwa na mzigo wowote na mambo yataendelea kama ambavyo yanaendelea sasa.

Mhe. Naibu Spika, tulipewa ushauri vile vile wa kuwepo na wawakilishi wa wanafunzi kutoka kila Taasisi zinazounganishwa na *SUZA* katika Bodi ya Usaili wa Wanafunzi ya Chuo ili kutoa ushiriki sawa wa wananfunzi. Kimsingi Mhe. Naibu Spika, baada ya kuunganishwa kwa Taasisi hizi husika, tutakuwa na Chuo Kikuu kimoja ambacho kitakuwa na Bodi moja ya Usaili wa Wanafunzi, ambao kwa mswada huu umeainisha nafasi 3 za wawakilishi

wanafunzi. Lakini pia Baraza la Chuo Kikuu katika kifungu cha 9(16)(c)(3) cha mswada huu limepewa uwezo wa kuandaa kanuni zitakazohusiana na uendeshaji wa Kamati zote za Chuo na miongoni mwa Kamati zinazohusika ni Kamati za Usaili wa Wanafunzi katika kila Skuli na Taasisi za Chuo.

Hivyo, ushirikishaji wa wanafunzi kutoka katika ngazi ya Skuli na Taasisi za Chuo. Hii inaonesha kwamba ni jinsi gani wanafunzi watapata haki yao ya ushirikishwaji kikamilifu katika shughuli mbali mbali za Chuo. Sisi humu ndani sote ni wawakilishi wa wananchi, kila mmoja ana ukubwa wa jimbo unategemea, lakini kila mmoja wetu amebeba watu hawapungui elfu tano kutokana na jimbo lake. Kwa msingi huo haina maana kwamba tupate wawakilishi wengi ambao watakuwa wanawakilisha kundi moja. Kwa hivyo, tukipata wawakilishi kama atakuwa ni mmoja kutoka katika ile Taasisi, basi ni kwamba huyu atakuwa tayari anawakilisha ile Taasisi yenyewe husika kama ambavyo sisi humu ndani tunawakilisha kundi kubwa la wananchi ambalo liko nyuma yetu.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wa kuongezwa neno “na” Serikali ya Mapinduzi katika kifungu cha 14, 24(b) na kuondosha neno "angalau" ushauri wake umezingatiwa na hilo neno "kuongeza Serikali ya Mapinduzi" tayari litaongezeka. Vile vile, ushauri wa kuainisha muda wa kikomo cha Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi wa Taasisi.

Mhe. Naibu Spika, ukomo huu haukuwekwa katika mswada kwa sababu tayari umeshaainishwa katika sheria mama kifungu 24(2). Kwa mnasaba huu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tayari ukomo huu unaoneshwa, kwa hivyo, hakuna haja ya kurejea katika mswada ambao uko mbele yetu.

Vile vile, wasiwasi wa Mheshimiwa kwamba, neno la Kiswahili na Kiingereza huku kuna neno 'vitengo' na huku kuna neno 'vitengo', nadhani masuala ya uandishi nayo pia yatazingatiwa vizuri.

Jengine ni kuhusu Jumuiya ya Wafanyakazi, je, itaweza kujiendesha kwa kila skuli miongoni mwa Chuo. Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo ya kifungu cha 20 na 26(b)(1) cha mswada huu kutakuwa na Jumuiya moja ya wafanyakazi ya uendeshaji na utaalamu katika Chuo. Hivyo, katika kila Skuli ya Chuo au Taasisi kutakuwa na matawi ya Jumuiya hiyo, Jumuiya hiyo itaratibiwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Katiba itakayotungwa na kuidhinishwa na Baraza la Chuo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, tulipata wasiwasi wa Mhe. Mwakilishi kwamba, je, kila nchi yenye masuala ya utalii huwa na Chuo chake. Kuunganishwa kwa *SUZA*, Chuo cha Utalii hakitosimamisha utoaji wa mafunzo ambayo hivi sasa yanaendelea kutolewa na Chuo kitaendelea kutoa masomo yote ya utalii kama ambavyo yanatolewa sasa, lakini vile vile kuna uwezekano mkubwa wa kuanzisha masomo mengine mapya yatakayoweza kusaidia sekta ya utalii. Kuna baadhi ya nchi zinazoendeleza utalii na hutoa mafunzo ya utalii katika Taasisi ambazo zipo chini ya Chuo Kikuu. Kwa msingi huu ni kwamba si jambo geni vile vile kwamba Chuo cha Utalii kuwa chini ya *SUZA*, lakini bado masomo yataendelea kama kawaida, lakini vile vile hata fani nyengine ambazo zinahusiana na masuala ya utalii zitaweza kuendelea, na kwa kuzingatia kuwa tayari *SUZA* iliweza kutoa *degree* ya Utalii, basi nayo *degree* hii itapata nafasi nzuri ya kuwemo katika Chuo hiki.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilijitokeza kwa Mheshimiwa ni kwamba *ZIFA* kimejitangaza vizuri nje na ndani ya Tanzania na yeye anadhani ni kwamba kibaki kama kilivyo. Vyuo vyote vimesajiliwa *TCU* na *NACTE* ambazo ndizo Taasisi zenye majukumu ya kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa na Taasisi za Elimu ya Juu na vyeti vyake huwa kwa kawaida vinatambulika na kukubalika ulimwenguni kote. Hivyo, *SUZA* kipo chini ya *TCU* na *NACTE* katika kuhakikisha ubora wa elimu inayotolewa nchini. Kwa mnasaba huu Chuo cha *ZIFA* kilikuwa kiko chini ya *NACTE* na kwa mujibu kama ambavyo tulieleza katika hotuba yangu niliyoitoa asubuhi ile ya awali ni kwamba *TCU* tayari imeshatoa masharti kwamba, Chuo chochote ambacho kitakuwa kinaanzisha *degree* basi lazima kifuate masharti ya *TCU* na Chuo cha *ZIFA* kitakuwa kimekosa masharti haya kwa sababu kilikuwa chini ya *NACTE*. Kwa hivyo, kukiunganisha *ZIFA* ndani ya *SUZA* basi ni mwanya mzuri sana wa *ZIFA* kuendelea na hatua nyengine za kutoa *courses* zake, lakini hata *SUZA* kuanzisha *courses* nyengine ambazo zitakuwa zinahusiana na masuala ya pale ya fedha ndani ya tawi la *ZIFA*.

Mhe. Naibu Spika, *ZIToD* na *ZIFA* visiunganishwe na bali Chuo cha Afya ndio kiunganishwe na *SUZA* kwa sababu kinashughulikia afya ya binaadamu.Hata fani za utalii na utawala wa fedha, tunapenda kutanabahisha kwamba nazo zinahitaji kuwa na wataalam wa hali ya juu na sio *ZIFA* peke yake. Kwa msingi huu ni kwamba, kuunganisha hivi vyuo vitatu vyote ni kwamba vitatuwezesha sisi kuweza kutoa wataalam zaidi na wataalam hawa labda ambavyo kama wangeweza kwenda nje ya nchi bali tutakuwa tuna utajiri wa kutoa wataalam hawa ndani ya nchi yetu, ndani ya Chuo Kikuu kimoja cha Serikali ambacho kitakuwa kipo imara na kitakuwa kina nguvu zaidi ya kile ambavyo vilivyo sasa.

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa, mwengine aliuliza juu ya Wajumbe wa Bodi ya Fedha watatoka *SUZA* pekee au na vyuo vyengine vinavyounganishwa. Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, katika kila Taasisi inayounganishwa na *SUZA* itakuwa na Kamati yake ya Fedha, Mipango na Maendeleo na Wajumbe wa Bodi ya Fedha wanachaguliwa na Baraza kama ambavyo sheria imeelekeza. Hivyo, ni kwamba katika kila Chuo kitakuwa kina mjumbe ambaye anatoka ndani ya ile Taasisi na atakuwa anaingia katika hili Baraza na atakuwa tayari kwamba amewakilisha.

Vile vile, katika masuala ya fedha ni kwamba itakuwa tayari Chuo kina kamati yake, kwa hivyo, kitakuwa kinatumia fedha na kupitishwa kwa mujibu wa sheria zilivyo. Lakini suala la *SUZA* kujipanga kwa usafiri kwa wanachuo. Kwa kawaida Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika mfumo wa Vyuo Vikuu vyote vilivyo ni kwamba, mwanafunzi huwa anafuata masomo yake pale yanapotolewa. Hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa kwa kiasi kikubwa wanafunzi wamekuwa wakisoma katika *campus* ambayo masomo yake yanatolewa. Hivyo Vyuo vikiunganishwa wanafunzi hawa wataendelea na utaratibu wao kama ulivyo na si utaratibu wa Chuo kusema inaweka mabasi maalum kwa ajili ya wanafunzi wake.

Hii ni kwa sababu sote ni mashuhuda, Chuo Kikuu hakina utaratibu kwamba kinaanza kipindi kuanzia asubuhi mpaka jioni.Kila mwanafunzi anaingia kwa mujibu wa kipindi chake. Kwa hivyo, hata kama watakuwa wameweka usafiri ina maana usafiri ule zaidi utawafaa wale wanafunzi ambao wanakwenda asubuhi na ambao labda watakuwa wanarudi baadae, lakini kati kati itakuwa ni shida. Kwa hivyo, kwa kuliona hili kupitia Mamlaka ya Usafiri yako mabasi ambayo yanakuwa yana *route* ya kupeleka wanafunzi Chuo Kikuu na kwa hili ni kwamba kila mmoja anakuwa anatoa ile nauli yake kama ilivyo kawaida.

Vile vile, ikazingatiwa kwamba Chuo kina *campus* nyingi na zimegawanyika katika sehemu tofauti. Maana yake ukisema upeleke usafiri inakuwa huo ni mzigo mwengine. Kwa hivyo, juu ya suala hili kwa sababu wote ambao wanakwenda Chuo tayari ni wanafunzi ambao wanajielewa, ni watu wazima, kwa hivyo, kila mmoja huwa anafanya utaratibu wake wa kufika Chuoni kwa mujibu wa kipindi chake husika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda niwatoe hofu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, maamuzi ya Serikali ya kuviunganisha hivi Vyuo si maamuzi ya kutaka kuvimeza hivi vyuo vyengine. Bali ni uamuzi ambao utavipa hadhi hivi vyuo vyengine navyo kupata hadhi kama ambavyo

Vyuo Vikuu vyengine vilivyo. Kwa hivyo, Waheshimiwa, nikuombeni sana kwa mnasaba wa kuimarisha ubora wa elimu yetu ya Zanzibar tukubaliane na tupitishe mswada huu ili tupate nafasi kwa Serikali kupitia Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali tuweze kusimamia ipasavyo utekelezaji wake na kama ambavyo mmetuagiza kufanya basi tutafanya.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho, nisije kusahau ni kwamba katika mapendekezo yote ambayo Kamati ilitupa tumeyapokea, isipokuwa kuna jambo moja tungeomba sana Kamati ikubaliane na sisi katika kifungu nambari 16 ambacho katika mapendekezo ya Kamati kilikuwa na marekebisho. Lakini tungeomba sana kwamba kifungu kile kibaki kama ambavyo kipo, kifungu nambari 16 kama ambavyo mapendekezo ya Kamati yalitoa basi kibakie kama kilivyo katika ule Mswada wa sheria na Kamati ikubali marekebisho yale tumeyazingatia, lakini kwa mujibu wa sheria ilivyo, basi kile kiendelee kubaki kama ambavyo kilivyo sasa.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana na nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwa pamoja tuupitishe mswada huu ili kuipa nafasi Wizara yetu kama hivyo nimeeleza awali iweze kutoa hiyo elimu bora, lakini vile vile itoe nafasi kwa hivi vyuo vyengine vipate hadhi ya kuwa chini ya Chuo Kikuu ili vipate hadhi husika, pia, viweze kutoa elimu iliyo bora na ambayo inatambulika zaidi ya ambavyo ilivyo sasa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mkono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2	Kusomwa

Sehemu ya Pili

Vifungu vya Marekebisho

Kifungu 3	Marekebisho ya kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha 12 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5	Kufuta kifungu cha 14
Kifungu 6	Marekebisho ya kifungu cha 16
Kifungu 7	Kuongeza kifungu kipya cha 16(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8	Kuongeza kifungu kipya cha 16(b) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Kuongeza kifungu kipya cha 16(c) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10	Kuongeza kifungu kipya cha 16(d) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11	Marekebisho ya kifungu cha 20 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12	Marekebisho ya kifungu cha 21 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13	Kuongeza kifungu kipya cha 24(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Kuongeza kifungu kipya cha 24(b) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15	Kuongeza kifungu kipya cha 24(c) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16	Kuongeza kifungu kipya cha 24(d)
Kifungu 17	Kuongeza kifungu kipya cha 24(e)
Kifungu 18	Marekebisho ya kifungu cha 26 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19	Kuongeza kifungu kipya cha 26(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20	Kuongeza kifungu kipya cha 24(a) pamoja na marekebisho yake

Kifungu 21	Kuongeza kifungu kipya cha 28(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22	Kuongeza kifungu kipya cha 29(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23	Kuongeza kifungu kipya cha 29(b) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24	Kuongeza kifungu kipya cha 36(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 25	Marekebisho ya kifungu cha 57 pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ametoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja imejadiliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Marekebisho) ya 2016

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Marekebisho) ya 2016 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ametoa hoja wale wanaokubaliana na hoja, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana na niwapongeze vile vile, kwa kupitisha mswada huu na nimpongeze pia, Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wa wizara hii kwa kupitisha mswada bila ya kupigwa buti hata moja. Lakini tuwaombee kheri waweze kutekeleza wajibu wao pamoja sasa na kuitekeleza vizuri kabisa sheria hii ambayo tumeipitisha hivi leo.*(Makofi)*

Baada ya kusema hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, sasa naahirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:05 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 29/09/2016 saa 3:00 asubuhi)